# Nipashe

Alhamisi Novemba 14, 2019 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580075

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710 LIKE & FOLLOW US




## Lugola asema hakuna Mtanzania kufungiwa laini ya simu Des. 31

UKURASA 3



ama

ALHAMISI NOVEMBA 14, 2019

AFYA NA MAZINGIRA

Ukurasa 14 Kinamama 'mashoto' wana uwezo ziada

Ilianzia kule na sasa iko hapa Ukurasa 19

Ukurasa 18 Ilikojificha saikolojia afya ya mtoto, urithi baba na mama

MOJA KWA MOJA MWANZA...

Mratibu Afya: Mti shamba yaua sana wajawazito, kuiacha ubishi mkubwa

UKURASA 13

# Kila kona Mkapa

• **Wabunge**, wanaharakati wampongeza, wasema kitabu chake kimetoa mwongozo wa kitaifa, Zitto amsifu kwa kuanika ukweli... *Endelea ukurasa 2*









Distributed via ippmedia

**"Amekuwa mkweli, nampongeza kwa kuwa ameamua kufanya jambo la ujasiri litakazoanzisha mjadala, kuamua maoni yake yajadiliwe. Nina imani hata Mzee Mwinyi na Kikwete wataiga mfano huu."**

**JANUARY MAKAMBA**

**"Mkapa ameonyesha hisia kwamba nafsi yake inamsuta kutokana na uamuzi aliowahi kuuchukua wakati akiwa madarakani... Nampongeza kwa unyeyekevu wake akiwa hai, matendo mema aliyoyafanya, yamekuwa sauti huru akiwa hai na akiwa hayupo duniani."**

**JAMES MBATIA**

**"Nampongeza Mkapa amelitendea haki taifa. Uongozi wa juu alioshika ni uzoefu mkubwa aliotengeneza, hivyo kupitia kitabu hiki Kinachoelezea mema na mabaya aliyofanya, itasaidia kupunguza makosa ambayo yangefanywa na viongozi wanaokuja.**

**ANNA HENGA**

**"Mkapa anaeleza makosa yaliyowahi kufanyika na majuto yake, hivyo ni funzo kwa jamii kuwa watu wanakosea na wajifunze kutorudia makosa.**

**DK. RUGEMELEZA NSHALA**




Scan Hapa

Fungua App ya QR code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store


## Wataka Waziri Jafo kusuka au kunyoa

• **Kutokana** na wingu zito uchaguzi mitaa, Chadema yakoleza chumvi... *Uk.2*

## Usajili wa wanachama NSSF sasa kwa Nida

UKURASA 3


**MICHEZO** **NDAYIRAGIJE, SAMATTA WAISHTUKIA E' GUINEA** UK.32

**MAONI, KATUNI** UK.6

# ...Zitto amsifia kusema ukweli

**Na Salome Kitomari**

MBUNGE wa Kigoma Mjini, Zitto Kabwe, amesema wakati akiwa mbunge hakuwahi kumuelewa Rais mstaafu, Benjamin Mkapa, na kwamba kupitia kitabu hicho amemuelewa.

Aidha, alisema kitabu hicho kimempa majawabu ya baadhi ya mambo ambayo alikuwa akijiuliza wakati ule. Kwa mfano suala la ubinafsishaji wa mashirika ya umma na namna ulivyotekelezwa.

Kwa mujibu wa uchambuzi wake wa kitabu hicho kilichozinduliwa juzi jijini Dar es Salaam, alisema Mkapa ameandika na amejitahidi kuwa mkweli wa nafsi yake.

"Watu wanaweza kuwa na tafsiri tofauti, lakini kama alivyosema mwenyewe mengi ni kuibua mjadala. Naamini mjadala utakuwapo tu," alisema Zitto.

Alisema akiwa kijana mdogo wa miaka miaka 29, alichaguliwa kuwa Mbunge, na akiwa humo alikuwa ni mwenye hasira kulingana na namna nchi ilivyokuwa inaongozwa.

"Niliona utawala wa Rais Mkapa kama mmoja ya tawala za rushwa kuliko zote kupata kutokea. Nilikuwa naumizwa sana na hali ya umasikini nchini na namna rasilimali madini zilivyokuwa zinaporwa.

Kwa hiyo nilikuwa nikimtazama Mkapa kama kiongozi asiyejali watu maskini na aliyeuza nchi kwa wageni," alisema Zitto.

Zitto ambaye pia ni Kiongozi Mkuu wa ACT-Wazalendo, alisema Mkapa ameeleza mageuzi makubwa aliyoyafanya kwenye uchumi.

"Nimeridhika na maelezo yake mazuri, lakini sikubaliani naye kuhusu ulazima wa kubinafsisha mashirika namna ile," alibainisha.

Mbunge huyo ambaye wakati huo alikuwa mbunge wa Kigoma Kaskazini, alisema Mkapa anasema hapakuwa na mbadala kwenye ubinafsishaji lakini . ulikuwepo kwa kuwa Rais Ali Hassan Mwinyi alishafungua Uchumi.

Alisema alipaswa kuachia sekta binafsi kushindana na mashirika ya umma badala ya kuwauzia watu kwa bei ya kutupwa na mashirika kutoendelezwa. Alisema serikali ya Mkapa ilijielekeza kwenye ubinafsishaji kama tafsiri ya kujikwamua kiuchumi na kwamba China hawakuuza mashirika bali waliruhusu sekta binafsi kushindana na mashirika na matokeo yake yakawa chanya sana.

Alisema kuhusu fedha za kodi kuendesha mashirika, Rais Mkapa angekuwa wazi zaidi kuwa kutoyapa fedha mashirika na kuruhusu sekta binafsi kuanza kushindana nayo, kungekuwa na viwanda vya nguo, korosho na vinginevyo.

Kwa mujibu wa Zitto, Mkapa ameonyesha kukiri kuhusu wizi wa EPA, na kwamba anafurahi kwa kuwa alikuwa mbunge pekee niliyeamua kuzuia jambo kama EPA kutokea tena kwa kuweka sheria ya vyama vya siasa kukaguliwa na CAG.

"Katika hili Mkapa ametendea haki nchi, lakini alipaswa kwenda hatua ya pili na kuomba radhi kwa kuruhusu wizi wa namna ile ambayo ulikuwa na madhara makubwa kwa nchi yetu," alisema.

INAENDELEA UK. 8



Naibu Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson (kushoto), akizungumza na Waziri Mkuu mstaafu na Mwenyekiti wa Bodi ya Agri Thamani Foundation, Mizengo Pinda, alipomtembelea ofisini kwake, Bungeni jijini Dodoma jana. **PICHA: BUNGE**

# Mkapa apongezwa kila kona

Distributed via ippmedia

**Na Waandishi Wetu**

WASOMI na wanaharakati nchini wamempongeza Rais mstaafu wa Awamu ya Tatu, Benjamin Mkapa, kwa kuandika kitabu na kuelezea maisha yake binafsi pamoja na mambo mazuri na mabaya aliyowafanya wakati wa uongozi wake.

Wamesema kitabu hicho kitakuwa mwongozo kwa viongozi waliopo na watakaoingia madarakani kwa maslahi mapana ya taifa.

Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Anna Henga, alisema Mkapa amelitendea haki taifa kwa kueleza vizuri uzoefu wake kwa mambo mazuri na mabaya aliyofanya na yanayofanyika.

Alisema kitabu hicho kitasaidia kupunguza makosa ambayo yangefanywa na viongozi wajao na kuwa darasa kwa serikali katika utekelezaji wa shughuli mbalimbali.

"Nampongeza sana Rais Mkapa kwa kuandika kitabu hiki, amelitendea haki taifa. Uongozi wa juu alioshika ni uzoefu mkubwa aliotengeneza, hivyo kupitia kitabu hiki kinachoelezea mema na mabaya aliyofanya, itasaidia kupunguza makosa ambayo yangefanywa na viongozi wanaokuja," alisema.

Mkurugenzi huyo alisema Mkapa anastahili pongezi kwa kuwa ndani ya kitabu chake hicho amekuwa wazi na mkweli katika kuelezea maisha yake hata kwa mambo ambayo ni mabaya kwake.

Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Dk. George Kahangwa, alimpongeza Mkapa kwa kuandika kitabu hicho, akieleza kuwa uamuzi huo unapaswa kuigwa na viongozi wengine na watu mashuhuri nchini kwa manufaa ya taifa.

Alisema kuna haja viongozi wa serikali kukisoma kitabu hicho ili kufanyia kazi baadhi ya mambo yaliyoandikwa na kiongozi huyo wa ngazi ya juu.

"Wananchi wanaweza kununua kwa ajili ya kujisomea, lakini serikali inapaswa kukisoma ili kufanyia kazi mambo mbalimbali katika uongozi na kuondoa ajenda za kulaumu na kunyoosheana vidole," alishauri Dk. Kahangwa.

Alisema baada ya kuzinduliwa kitabu

INAENDELEA UK. 8

# Wamtaka Waziri Jafo kusuka au kunyoa

**Na Waandishi Wetu**

CHAMA cha National League for Democracy (NLD) kimetangaza rasmi kujitoa katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, huku kikimtaka Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo, ajiuzulu.

Uamuzi wa chama hicho umeongeza idadi ya vyama vya siasa vya upinzani vilivyofikia uamuzi wa kujitoa kushiriki uchaguzi huo kufikia vinane. Vingine ni ACT-Wazalendo, Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Chauma, NCCR-Mageuzi, UPDP, Chama cha Wananchi (CUF) na Chama cha Kijamii (CCK).

Kwa mujibu wa taarifa ya NLD iliyotolewa jana na Mwenyekiti wa chama hicho, Oscar Makaidi, kinamtaka Jafo kujiuzulu mara moja kwa madai kuwa ameshindwa kusimamia uchaguzi huo na kulitia taifa hasara.

"NLD hatuna imani naye licha ya kuagiza kuwa wagombea wote walioenguliwa, warudishwe, agizo ambalo hana mamlaka nalo kikanuni wala kisheria," Makaidi alisema.

Katika taarifa yake hiyo, NLD kimeamua kujitoa katika uchaguzi huo kwa kuwa una kasoro kubwa na haziwezi kurekebishika katika muda uliobaki.

Chama hicho kimemwomba Rais John Magufuli kusitisha uchaguzi huo unaotarajiwa kufanyika Novemba 24 na mchakato wake wote uanze upya.

"Kwa kuwa Tamisemi imeshindwa kusimamia uchaguzi huu wa Serikali za Mitaa, tunataka usimamiwe na tume huru ya taifa ya uchaguzi," alisema.

Makaidi pia alisema NLD haikubaliani na uamuzi wa Jafo kuwa amefuta uamuzi wote uliofanywa na wasimamizi wasaidizi wa kuwa hana mamlaka hayo kikanuni na kisheria.

"Tunaamini kwamba kuendelea na uchaguzi chini ya usimamizi ule ule ni kuhalalisha upungufu wote uliojitokeza, mwingi ukiwa ni wa makusudi.

"Kuendelea na uchaguzi huu ni kuendelea kutegemea makosa mengine huko mbeleni hasa wakati wa upigaji kura na utangazwaji wa matokeo yake.

"Tumepokea malalamiko mbalimbali kutoka kwa wagombea wetu yanazothibitisha ukiukwaji na ubakwaji wa demokrasia kwa kiwango cha kutisha kiasi cha kuufanya uchaguzi huu kuwa kituko.

"Kwa ujumla, uchaguzi umepoteza sifa ya kuitwa uchaguzi, hivyo tumeazimia kujitoa," Makaidi alieleza zaidi katika taarifa yake hiyo.

Kiongozi huyo wa NLD aliwataka wanachama na wagombea wao wote nchi nzima kuwa watulivu na kutojihusisha kwa lolote kuhusiana na uchaguzi huo mpaka hapo watakapotaarifiwa vinginevyo.

INAENDELEA UK. 8

HABARI KITAIFA

# Dawa ya waathirika 'kubeti' yaja

**Na Gwamaka Alipipi,** DODOMA

SERIKALI imesema inaandaa utaratibu wa kuanza kutoa tiba kwa Watanzania ambao wamepata uraibu kutokana na kujihusisha kupita kiasi na michezo ya kubahatisha, maarufu kama kubeti.

Pia imesema imeshaanza kuchukua hatua ya kujenga mfumo wa teknolojia ya habari na mawasiliano (Tehama) utakaotumika katika kusimamia mapato yatokanayo na michezo hiyo pamoja na kuratibu mienendo ya wachezaji kwa nia ya kukabiliana na uraibu wa michezo hiyo.

Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Ashatu Kijaji, alisema hayo jana bungeni mjini Dodoma wakati akijibu swali la Mbunge wa Ileje (CCM), Janet Mbene, aliyetaka kujua athari zitokanazo na michezo ya kubahatisha.

Mbene pia alitaka kujua mipango ya serikali katika kuchukua tahadhari za kuhakikisha michezo ya kubahatisha inashirikisha watu wenye ufahamu wa athari za kutegemea michezo hiyo, hali inayoweza kuwaletea athari kubwa za kiuchumi, kijamii hadi ndani ya familia na taifa.

Dk. Kijaji alisema: "Serikali inaandaa utaratibu wa kuanza kutoa tiba kwa wachezaji ambao wamepata uraibu kutokana na kujihusisha kupita kiasi kwenye michezo ya kubahatisha."

Aliongeza kuwa serikali imeshaanza kutoa elimu kwa umma kuhusu athari hasi zitokanazo na michezo ya kubahatisha, kudhibiti uagizaji na uendeshaji holela wa michezo hiyo hususani ya mitandaoni. Pia alisema serikali nimeshaanza kuboresha sheria ya michezo ya kubahatisha kwa lengo la kukabiliana na athari za michezo hiyo.

Dk. Kijaji alisema athari zilizochukuliwa na serikali zinalenga kupunguza ushawishi wa kushiriki michezo ya kubahatisha kupita kiasi na hivyo kupunguza athari hasi zitokanazo na michezo ya kubahatisha kwa jamii.

Alisema hivi sasa kuna changamoto ya kusimamia wachezaji wa michezo ya kubahatisha, hususani wachezaji wa michezo isiyohusisha mfumo wa Tehama.

Kwa mujibu wa Kijaji, serikali iko mbioni kuunganisha michezo yote kwenye mfumo huo unaoendelea kujengwa, utaanza kutumika Januari, mwakani.

"Mfumo huu utaiwezesha serikali kuratibu mienendo ya kila mchezaji na kuchukua hatua dhidi ya wale wanaokiuka sheria na kanuni za michezo ya kubahatisha. Mfumo huo utatumika pia kudhibiti uchezaji uliokithiri kwa kuweka viwango vya fedha za kuchezwa," alisema.

# Lugola asema hakuna atakayezimiwa simu

**Na Gwamaka Alipipi,** DODOMA

WAZIRI wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Kangi Lugola, amewaondoa hofu Watanzania kwa kueleza kuwa hakuna laini ya simu ya mtu itakayofungwa kwa kukosa kitambulisho cha taifa.

Kauli hiyo inakinzana na zile zinazotolewa mara kwa mara na maofisa wa sekta ya mawasiliano kuwa laini zote ambazo hazitasajiliwa kwa alama za vidole na kwa kutumia kitambulisho cha mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (Nida), zitafungwa ifikapo Desemba 31, mwaka huu.

Hata baadhi ya watumiaji wa simu ambazo laini hazijasaliwa wakati wa kupiga simu wamekuwa wakihimizwa kusajili kabla ya muda uliowekwa kwa kuwa kushindwa kufanya hivyo, laini zao zitafungwa.

Lugola alitoa kauli hiyo jana bungeni mjini Dodoma wakati akijibu mwongozo wa Mbunge wa Kavuu (CCM), Dk. Pudenciana Kikwembe, ambaye alitaka kupata majibu ya serikali kuhusu wananchi ambao bado hawajapata vitambulisho vya taifa pamoja na kusajili laini za simu.

Alisema lengo la usajili na utambuzi ilikuwa kuwafikia watu milioni 23.3 lakini hadi sasa Watanzania milioni 20.5 wameshasajiliwa, zimezalishwa namba za vitambulisho kwa Watanzania milioni 15.5.

"Naomba niwatoe hofu Watanzania kwamba hakuna mtu yoyote ambaye laini yake ya simu itafungwa kisa hajasajili kwa sababu hana kitambulisho cha taifa," alisema Lugola.

Lugola alisema kazi ya utambuzi, usajili na utoaji wa vitambulisho kwa wananchi ambao wana sifa za kupata vitambulisho ni endelevu na haina mwisho.

Kwenye mwongozo wake, Kimwembe alisema: "Kwa sasa tunaandikisha vitambulisho vya Nida, Mheshimiwa Mwenyekiti tatizo limekuwa kubwa hasa katika majimbo yetu ya vijijini hususani jimbo langu la Kavuu na Mlele." "Uandikishaji umekuwa shida na kama tunavyojua mwisho ni Desemba. Naomba kauli ya serikali nini kinafanyika ili kupata vitambulisho?" Alihoji Kikwembe.

Kutokana na mwongozo huo, Lugola alisema: "Naomba niwaondolee wasiwasi Watanzania wote kwamba utambuzi na usajili na utoaji wa vitambulisho kwa wananchi ambao wana sifa za kupata vitambulisho ni endelevu na haina mwisho wala haina tarehe. Si kweli kwamba ikifika tarehe fulani kama Mtanzania hajapata kitambulisho basi hatapata kitambulisho tena."

"Kwa hiyo Watanzania wasiwe na wasiwasi ni kazi endelevu na ndio maana kila mwaka kuna Watanzania ambao wanafikisha miaka 18. Niwatoe wasiwasi Watanzania wote kwamba maelekezo ya Rais John Magufuli hakuna Mtanzania ambaye simu yake itazuiwa kutumika eti kwa sababu hana kitambulisho cha taifa," alisisitiza.

Lugola alimwagiza Mkurugenzi Mkuu wa Nida, Dk. Anord Kihaule na maofisa wake katika wilaya zote kuhakikisha namba ambazo zinatolewa wazipeleke kwa wahusika.




Meneja Uhusiano na Elimu kwa Umma wa Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii (NSSF), Lulu Mengele (kushoto), akifafanua jambo wakati wa uzinduzi wa Kampeni ya Boresha Taarifa za NSSF, jijini Dar es Salaam jana. Katikati ni Meneja Matekelezo na Uandikishaji wa shirika hilo, Joseph Fungo na Ofisa Uhusiano Mwandamizi, Janet Ezekiel. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Usajili wanachama NSSF wa vitambulisho vya Nida

**Na Salome Kitomari**

SHIRIKA la Taifa la Hifadhi ya Jamii (NSSF), limezindua kampeni ya kuwasajili wanachama wake kwa kutumbia vitambulisho vya taifa ili kuboresha huduma na taarifa za kila mwanachama.

Meneja Matekelezo na Uandikishaji wa NSSF, Joseph Fungo, alisema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati akitambulisha kampeni ya 'Boresha Taarifa na NSSF.'

Alisema wameamua kutumia kitambulisho cha taifa kufanya usahili wa wanachama na kwamba waajiri wanapaswa kuwasilisha orodha ya wafanyakazi wao pamoja na namba zao za vitambulisho.

Alisema namba hizo zitahusishwa na taarifa zilizoko NSSF ili mwanachama anapokwenda sehemu yoyote nchini, taarifa zake zitambulike kwa urahisi.

"Tumeboresha mifumo ya uandikishaji, awali ilikuwa inachukua muda mrefu sasa mwanachama akiwa na kitambulisho cha taifa atakuwa na taarifa chache anazotakiwa kujijaza. Nyingi tunazipata kutoka Nida," alisema.

Alisema kuanzia sasa wanachama wapya watatumia namba zao za Nida (Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa) kufanya usahili, tofauti na zamani hazikuhitajika.

Kwa mujibu wa Meneja huyo, NSSF imeunganisha taarifa zake na mifumo ya Nida na kwamba watapata taarifa zote za mwanachama kutoka mamlaka hiyo na kwa maboresho hayo, mwanachama anaweza kupata kitambulisho na namba ya usajili kwa muda mfupi.

"Zamani mwanachama alikuwa anazunguka kwa muda mrefu kupata namba yake ya uanachama. Sasa hivi ni muda mfupi sana namba umepata ili mradi uwe na namba ya Nida," alisema.

Kuhusu wanachama wa zamani, alisema mtumishi anapaswa kwenda kwa mwajiri wake na kupeleka namba ya kitambulisho cha Nida kisha mwajiri atawasilisha na shirika.

Alisema lengo la shirika ni kuendelea kumhudumia mwanachama kwa ubora zaidi na kwamba sasa taarifa zao zitakuwa moja zilizoko kwenye kitambulisho cha taifa.

Pia alisema kwa waajiri wapya inabidi wajaze fomu mpya ambayo ina ukurasa mmoja na kwamba atajaza taarifa chache tu.

Naye Meneja Kiongozi, Uhusiano, Elimu kwa Umma wa NSSF, Lulu Mengele, alisema kampeni hiyo itakuwa endelevu na inalenga kuwapa huduma bora na kwa wakati wanachama wapya.

Alisema ili kurahisisha uandikishaji hasa kwa wanachama wapya, wawashauri wafike na namba za Nida.

# Wanufaika wa kaya maskini watengeneza barabara kilomita 7

**Na Elizabeth Zaya,**
WANGING'OMBE

WANUFAIKA wa Mpango wa Kunusuru Kaya masikini unaosimamiwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (Tasaf), katika kijiji cha Itambo katika Halmashauri ya Wanging'ombe wamegeuka kuwa kivutio baada ya kutengeneza barabara za urefu wa kilomita 7.3 kuelekea katika maeneo ya mashamba ya wakazi wa kijiji hicho.

Mwenyekiti wa kamati ya wasimamizi wa wanufaika wa Tasaf katika kijiji hicho, David Ngole, alisema mradi huo wa kuchimba barabara uliibuliwa na wanufaika wenyewe baada ya kuona tabu waliyokuwa wakipata wananchi wa kijiji hicho ya kusafirisha mazao yao.

Alisema wananchi wengi walikuwa wakilazimika kusafirisha mazao yao kichwani, hivyo kuchukua muda mrefu kufanya kazi hiyo, huku mazao mengine yakiharibikiwa shambani.

"Sisi hapa kwetu tunalima sana vitunguu, karoti, hoho, nyanya na viazi. Kwa kipindi kirefu tulikuwa tunahangaika, unakuta mtu amevuna vitunguu vyake, lakini wakati mwingine vinaozea shambani kwa sababu vinasafirishwa kidogo kidogo kichwani kwa sababu hakupitiki na gari,"alisema Ngole.

Aliongeza: "Kwa hiyo Tasaf kupitia miradi ya kuboresha miundombinu inayofadhiliwa na Umoja wa nchi zinaozalisha na kusambaza mafuta duniani ( OPEC) waliwaomba wananchi kuibua miradi ambayo wanaona inatija kwa jamii ndio wakaomba kutengeneza Barabara."

Mariam Mgaya, mnufaika wa Tasaf, alisema walitumia miezi mitano kuchimba barabara hiyo, na kwamba walifanya kazi hiyo kwa ushirikiano na kwa ali kubwa kwa sababu ya taabu waliyokuwa wakipata ni kubwa.

"Na watu walikuwa hawaamini kama tutaweza kutengeneza barabara ikapendeza kwa jembe la mkono, walikuwa wanakuja wanatushangaa, lakini kwa sasa wanatuelewa," alisema Mariam.

Diwali wa Kata ya Mdandu, Annaupendo Gombera, alisema walengwa hao wamekuwa tija kwa wanakijiji kwa kuwa kwa sasa wanasafirisha mazao yao kwa urahisi kwa kutumia magari kutoka shambani.

Ofisa Ufuatiliaji wa miradi ya Tasaf Halmashauri ya Wanging'ombe, Edwin Mlowe, alisema mbali na barabara hizo, kuwanufaisha wananchi wa eneo hilo, lakini pia walengwa walipata ajira za muda na kujipatia kipato.



Vijana wakishirikiana kuhamisha kibanda cha kufanyia biashara katika eneo la Africana Sinza, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Udhuru wakwamisha kesi ya Mbowe

**Na Hellen Mwango**

KESI inayomkabili Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe na wenzake wanane, itaendelea kesho kusikilizwa utetezi wa washtakiwa baada ya mawakili wa utetezi kuwa na kesi nyingine Mahakama Kuu.

Wakili Dickson Matata, alidai kuwa Profesa Safari na Kibatala wako Mahakama Kuu wana kesi nyingine wanaendesha kwa siku mbili. Matata alitoa madai hayo jana mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Thomas Simba anayesikiliza kesi hiyo.

Kutokana na sababu hizo, alidai kuwa mawakili hao wameomba kesi hiyo iahirishwe hadi Novemba 26 hadi 29, mwaka huu, kuendelea na utetezi.

Wakili wa Serikali Mkuu, Faraja Nchimbi, alipinga ahirisho la kesi hiyo kwa madai kuwa sababu zilizotolewa si za msingi na mawakili wanaodaiwa kuwa Mahakama Kuu wawasilishe uthibitisho.

Alidai kama mahakama itaridhia wakili Matata aendelee kuendesha shauri hilo au liendelee leo, kwa sababu washtakiwa hao wanawakilishwa na mawakili wengi.

Alitaja miongoni mwa mawakili hao kuwa ni John Mallya, Jeremiah Mtobesya, Marwa Magau na Omary Msemo na mahakama haijaelezwa mahali waliko.

Hakimu alimhoji wakili Matata aeleze waliko mawakili Mtobesya, Mallya, Magau na Msemo na akadai ana taarifa za mawakili watatu tu ambao ndiyo wanawawakilisha washtakiwa. Mbali na Mbowe, washtakiwa wengine katika kesi hiyo ni Katibu Mkuu Dk. Vincent Mashinji; Mbunge wa Iringa Mjini, Peter Msigwa; Naibu Katibu Mkuu Zanzibar, Salum Mwalimu; Mbunge wa Kibamba, John Mnyika; na Mbunge wa Kawe, Halima Mdee.

Wengine ni Mbunge wa Tarime Vijijini, John Heche; Mbunge wa Tarime Mjini, Esther Matiko na Mbunge wa Bunda, Ester Bulaya.

Washtakiwa hao wanakabiliwa na mashtaka 13 likiwamo la kula njama kwa madai kuwa kati ya Februari 1 na 16, mwaka jana jijini Dar es Salaam, walikula njama ya kutenda kosa la kufanya mkusanyiko usio halali na kukiuka tamko kutawanyika.

Hakimu Simba alisema kesi hiyo itaendelea kusikilizwa ushahidi wa utetezi na kwamba Mbowe ataendelea kuhojiwa na Jamhuri kesho.

# Ujenzi gati la magari Dar wakamilika

**Na Mary Geofrey**

MAMLAKA ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA), imekamilisha ujenzi wa gati maalumu la kuhudumia meli za magari maarufu kama (RoRo) lenye urefu wa mita 327 ikiwa ni sehemu ya maboresho yanayoendelea katika Bandari ya Dar es Salaam.

Kadhalika, mamlaka inaendelea na ujenzi wa eneo lenye uwezo wa kuhifadhi magari 7,500 kwa wakati mmoja kwa lengo la kupunguza muda wa kuhudumia meli za magari bandarini hapo.

Kaimu Mkurugenzi wa Bandari ya Dar es Salaam, Elihuruma Lema, alisema juzi kuwa lengo la kujenga eneo la kuhifadhia magari karibu na gati hilo ni kurahisisha kazi ya ushushaji wa magari ili kuongeza ufanisi.

Aidha, alisema baada ya kukamilika kwa ujenzi wa gati hilo Septemba, mwaka huu, idadi ya shehena ya magari yaliyoshushwa katika gati hilo imeongezeka hadi kufikia magari 45,000 kwa kipindi cha miezi mitatu tu.

Alisema kwa mwaka wa fedha 2018/19, Bandari ya Dar es Salaam ilihudumia magari 160,000 kutokana na kukamilika kwa ujenzi huo ambao utaongeza ufanisi na imejipanga kuhudumia zaidi ya magari 180,000 kwa mwaka 2019/20.

"Tunaishukuru serikali kuruhusu ujenzi huu wa uboreshaji wa bandari kwani kukamilika kwa ujenzi wa gati hili, kumesaidia kuongeza idadi ya shehena hiyo bandarini na kusaidia ongezeko la mapato," alisema Lema. Alisema awali Bandari ya Dar es Salaam ilikuwa na uwezo wa kuhudumia meli zenye urefu wa mita 260 zinazobeba makontena 4,500, lakini baada ya kukamilika kwa maboresho hayo, itakuwa na uwezo wa kuhudumia meli kubwa hadi za urefu wa mita 305 ambazo zina uwezo wa kubeba makontena kati ya 7,000 na 8,000. Kadhalika alisema katika kuhakikisha ulinzi na usalama katika bandari hiyo unaboreka zaidi, wamefunga kamera maalumu za kiulinzi zipatazo 420 kwa ajili ya kudhibiti matukio ya wizi bandarini hapo.

Mbali na uwapo wa kamera hizo, pia wanashirikiana na vyombo vya ulinzi na usalama kwa ajili ya kuboresha ulinzi katika bandari hiyo.

"Kila kinachoendelea kwenye meli tunakiona na kikitokea kitu watu wa usalama wanachukua hatua na kuna ulinzi wa askari wa kwenye maji wanaofanya doria kwa saa 24 katika lango la kuingia bandarini na maeneo yote ya bandari hadi Bagamoyo," alisema.

Mbali na ulinzi kuimarishwa pia kuna ukaguzi mkubwa wa mizigo ambao hufanywa magati sita iliyopo bandarini hapo. Alisema kwamba kila Kontena linalopita katika Bandari ya Dar es Salaam linafanyiwa ukaguzi wa kina.

HABARI KITAIFA

# Waziri ashtukia tena balaa mifuko plastiki

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), George Simbachawene, amewaonya wafanyabiashara wanaoingiza mifuko mbadala isiyokidhi viwango.

Pia, amewaonya wamiliki wa viwanda vinavyozalisha mifuko laini ya plastiki kwa kificho na kuiingiza sokoni kwa magendo kuwa watachukuliwa hatua za kisheria.

Akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake jijini Dodoma jana, Simbachawene alisema pamoja katazo la mifuko ya plastiki kuibua fursa za kuwekeza katika kuzalisha mifuko mbadala, wapo baadhi ya watu wanaingiza na kuzalisha mifuko mbadala aina ya non-woven ambayo haikidhi mwongozo wa viwango vilivyowekwa na Shirika la Viwango (TBS).

Aliagiza Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), TBS kwa kushirikiana na kikosi kazi cha kitaifa cha katazo la mifuko ya plastiki, kufanya ufuatiliaji na kuwabaini wazalishaji hao na hatua zichukuliwe dhidi yao, ikiwa ni pamoja na kuteketeza bidhaa hizo ili iwe fundisho kwa wengine. Waziri huyo alisema wapo baadhi watu wanageuza matumizi ya vifungashio vya mifuko laini ya plastiki (plastic tubings) kama vibebeo vya bidhaa mbalimbali kama vile nyanya, karoti, njegere pamoja na uingizaji wa magazeti yaliyotumika kwa ajili ya kufungashia bidhaa katika maeneo ya masoko, maduka na maeneo mengine ya biashara.

"Hali hii ni makosa kisheria, hivyo naelekeza NEMC, TBS pamoja na kikosi-kazi cha kitaifa washirikiane kwa karibu na kamati za ulinzi na usalama za mikoa, wilaya na mitaa nchini, kuendelea kufanya kazi bila kuonea mtu yeyote katika kudhibiti matumizi ya mifuko mbadala aina ya non-woven na kudhibiti uingizaji, uzalishaji na usambazaji wa mifuko ya non-woven isiyokidhi vigezo vinavyokubalika kisheria," alisema.

Simbachawene alibainisha kuwa NEMC kwa kushirikiana na TBS wameendesha ukaguzi katika mikoa ya Mwanza na Dar es Salaam na kufanikiwa kukamata mifuko ya Non-Woven isiyokidhi viwango zaidi ya vipande milioni mbili na rollers zaidi ya 200 kwa ajili ya kutengeneza mifuko hiyo na kwamba mifuko hiyo imezuiliwa kuingia sokoni na hatua za kisheria zinaendelea.

Aliongeza kuwa mifuko laini ya plastiki (plastic tubings) vipande 9,600 vimekamatwa Mwanza zikiwa kwenye magunia manane ambayo na akapongeza juhudi zinazofanywa na mamlaka mbalimbali za serikali ikiwamo NEMC, TBS na vyombo vya ulinzi na usalama katika kudhibiti wimbi la uingizaji wa mifuko hiyo isiyokidhi viwango.



Mwenyekiti Ngome ya Wanawake Taifa ACT- Wazalendo, Chiku Aflah (katikati), akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, kuhusu ngome hiyo, kumtaka Rais John Magufuli, kukutana na viongozi wa vyama vya siasa nchini, ili kufikia maridhiano na mwafaka wa kisiasa kwa maslahi ya taifa. Kushoto ni Naibu Katibu Zanzibar, Zahra Ali na Makamu Mwenyekiti Ngome Taifa, Elizabeth Magwaja. **PICHA: MIRAJI MSALA**

Distributed via ippmedia




# DPP aomba kutaifishwa nyumba za mshtakiwa

**Na Hellen Mwango**

MKURUGENZI wa Mashtaka nchini (DPP), amewasilisha maombi Mahakama Kuu ya Tanzania, Divisheni ya Uhujumu Uchumi na Rushwa, maarufu kama Mahakama ya Mafisadi, kutaka kutaifisha mali zikiwamo nyumba 7 za mke wa aliyekuwa miongoni mwa Wakurugenzi wa Kampuni ya Superior Financing Solutions, Aloysius Gonzaga, Magreth Gonzaga.

Maombi hayo namba 1/2019 yanatarajia kuanza kusikilizwa mbele ya Jaji Sirilius Matupa, Novemba 26, mwaka huu.

Katika maombi hayo, DPP anaomba kutaifisha ploti namba 199, Block D, namba 121302 iliyoko Tegeta, Ploti namba 200 Block D namba 39021 iliyoko Tegeta.

Zingine ni ploti namba 1378, Block, E Tegeta ikiwa namba za hati 41275 na ploti namba 176 Block B iliyoko Aman Gomvu ikiwa na hati namba 138598, ploti namba 191, Block B iliyoko Aman Gomvu ikiwa na hati namba 132797 na namba 174 Block B iliyoko Aman Gomvu ikiwa na hati namba 138597.

Mapema mwaka huu, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) ilitangaza kumsaka Magreth anayedaiwa kumiliki nyumba tatu za kifahari jijini Dar es Salaam huku akituhumiwa kutakatisha fedha haramu kinyume cha Kifungu Na. 12(d) na 13(a) cha Sheria ya Utakatishaji Fedha Haramu Na. 12 ya Mwaka 2006.

Katika mkutano wake na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam, Mkurugenzi Mkuu wa Takukuru (wakati huo), Diwani Athumani, alisema wanamsaka Magreth kupitia tangazo lililotolewa kwa amri ya Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu inayosikiliza shauri la jinai namba 28 la mwaka 2019.

Alidai Gonzaga ambaye kwa sasa anadaiwa kukimbilia nje ya nchi, anatafutwa na Takukuru kwa tuhuma za kutakatisha fedha haramu na kujipatia mali kupitia Superior Financing Solution Limited (SFS) inayodaiwa kufanya biashara bila kulipa kodi ya serikali.

Gonzaga na mwenzake Isaack Kasanga wanakabiliwa na kesi ya uhujumu uchumi namba 5/2019 katika Mahakama Kuu Kitengo cha Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi.

Washtakiwa wanakabiliwa na mashtaka 45 ambayo ni kula njama, kutenda kosa moja, kughushi (12), kuwasilisha nyaraka za uongo (tisa), kushindwa kulipa kodi na utakatishaji fedha mashtaka 30.

Inadaiwa kati ya Machi 2, 2010 na Aprili 26, 2016 katika maeneo tofauti ndani ya Jiji la Dar es Salaam washtakiwa hao walikula njama kwa kughushi, kukwepa kulipa kodi na kutakatisha.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Upinzani, CCM tunahitaji ufumbuzi kabla ya kampeni

**WAKATI** kampeni za uchaguzi wa serikali za mitaa na vijiji zinaanza wiki hii, ushindani wa kisiasa baina ya CCM na upinzani wakati huu unaelekea kujenga mazingira ya sintofahamu hasa kuhusu hatima ya uchaguzi huu.

Ni kwa sababu watu wengi hawafahamu mustakibali wa uchaguzi huo kwa vile vyama vya upinzani, CCM na serikali vinaendelea kuvutana kuhusu ushiriki kwenye kuwachagua viongozi wa ngazi hizo za vitongoji, vijiji na mitaa.

Mazingira yaliyoko sasa yanaonyesha kuwa huenda watu wengi hawatashiriki katika kupiga kura, kwani wanaona kama hakuna msukumo zaidi wa siasa za kiushindani kufuatia wagombea wote wa upinzani kujiondoa kwenye kinyang'anyiro hicho.

Tunaona kuwa ni lazima wadau wawahimize viongozi wa pande zinazopingana kupata ufumbuzi wa suala la ushiriki wa wananchama wao kwenye uchaguzi huu ambao kampeni zake zinaanza keshokutwa Novemba 17.

Tunatoa wito kwa wahusika kumaliza mkwamo huo ili kuwawezesha wagombea kuanza kampeni za uchaguzi huo utakaofanyika Jumapili ya Novemba 24 mwaka huu.

Tutahadharishe tu kuwa si vyema watu wachache hasa wa chama kimoja wakashiriki katika kuchagua viongozi wa umma takribani 1,000 wakiwamo wenyeviti wa vijiji, vitongoji na mitaa pamoja na wajumbe wengine wengi.

Tunaamini kuwa wapinzani kuendelea kususia uchaguzi na kuiachia CCM pekee si jambo lenye afya kwa taifa letu.

Ni ukweli kuwa pamoja na CCM kuwa na wagombea ambao wako tayari kusimama kupigiwa kura, suala la haki ya kikatiba ya kutaka kuwapo na vyama vingi na wagombea wake kushiriki kwenye uchaguzi ni ya muhimu na haki yao ni suala linalotakiwa kuwa msingi wa uchaguzi wetu.

Kila mara viongozi wamekuwa wakizungumzia kuhusu amani na utulivu lakini ni muhimu kuongezea kuwa pamoja na amani hiyo, kutenda haki kuwe msingi, kwa sababu hakuna amani bila wapinzani nao kuwa na haki na kushiriki haki yao ya kugombea na kuchaguliwa kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa na vijiji bila kuvutana.

Kwa hiyo tunasisitiza wito wa haki na amani kwa pamoja katika uchaguzi huu hasa kipindi hiki ambacho kampeni zake zinatarajiwa kuanza wiki hii.

Tutakubaliana kuwa baadhi ya viashiria vinavyoonekana ni pamoja na watu kuwa na manung'uniko dhidi ya vyama vyao na wakati mwingine dhidi ya maamuzi yanayofanywa na vyombo vinavyosimamia uchaguzi huo wa serikali za mitaa na vijiji.

Licha ya watu kuhamasishwa kujiandikishwa kwa wingi ili kuwachagua viongozi hao, na pia kuitikia wito na kujitokeza, haitakuwa na tija kama mazingira ya kupiga kura ili kuwachagua viongozi wanaowataka yatakuwa na sintofahamu inayotokana na kambi ya upinzani kujitoa.


Ikumbukwe kuwa thamani ya kura ya kila mtu ni muhimu katika kudumisha demokrasia.

Ili kuendeleza demokrasia tunahitaji kuwa na uchaguzi wenye amani, uhuru na haki lakini wenye msisimko mkubwa na ushindani mkali kati ya vyama vinavyoshiriki.

Tunaamini kuwa na wapigakura wenye furaha na matumaini ambao watawachagua viongozi wanaowapenda, lakini pia wananchi ambao wana imani na mamlaka zinazosimamia uchaguzi huo.

Ndiyo maana tunakumbushana tena kuwa wakati huu tunapokwenda kwenye wiki mbili za kampeni za uchaguzi ni lazima tukubaliane kuwa kama taifa tunahitaji kupata ufumbuzi wa haraka wa sintofahamu hii ya wapinzani kukataa kushiriki kwenye uchaguzi huu muhimu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Kibiti wanapojivunia mageuzi 'umwinyi' basi, mapato juu

Na Yasmine Protace

Distributed via ippmedia

**MARA** zote mapato yanaposimamiwa katika sehemu yoyote, iwe binfasi ya kiserikali, kuna mafanikio lazima kushuhudiwa.

Na mapato hayo yanapopatikana na katumika vizuri, basi ni dhahiri yanatoa matokeo chanya, kwani yanasaidia uboreshaji kwa namna nyingi.

Hiyo ndio maana kuna Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), ambayo mbali na kukusanya mapato ya ushuru na kodi za kiserikali, pia mapato mengineyo, kwani ni wakala mkuu wa serikali katika jambo hilo.

Tumekuwa tukisikia na kujionea serikali inavyosema kuwa inaboresha mambo na majukumu yake katika eneo fulani. Nyuma ya pazia ni matokeo ya usimamizi mzuri wa mapato ya kiserikali na kodi. Rais Dk. John Magufuli, mchana kwa asubuhi huwa ni mhubiri wa hilo. Anaeleza mafanikio ya serikali yake kufanikisha mengi, tena mazito. Yote ni zao la usimamizi wa mapato ya umma.

Dhana ya mapato hata kuangukia ngazi ya mtu binfasi, asipokuwa makini binafsi na kibishara, katika kujisimamia anaweza asifike mbali katika masuala ya kimaendeleo.

Atabaki kuwa shuhuda wa kuwahi kushika fedha au kuwa karibu nazo bila ya mafanikio. Hivyo, inatakiwa mtu ajifunze suala la kusimamia mapato yake aweze kunufaika nayo.

Yapo mashirika ambayo yamekuwa yakifundisha jamii juu ya kusimamia mapato. Lengo ni kuiwezesha jamii imudu kujitambua katika suala zima la usimamizi wa mapato.

Kama mapato yasiposimamiwa kikamilifu, ukiuwaji katika eneo hilo unakuwa wa shida. Mara nyingi mapato yanaposimiwa kikamilifu, kunachangia kuwapo maendeleo mazuri katika eneo hilo. Ndio tunda maendeleo linapozaliwa.

> **Anaongeza kwamba, halmashauri ina vyanzo mbalimbali vya mapato, ikiwamo mapato ya korosho na kiwanda cha samaki aina ya 'pronzi' ambacho kilifungwa miaka minane iliyopita na sasa kinatarajiwa kufunguliwa mwezi huu.**

Hivi karibuni Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya Kibiti mkoani Pwani, Khatibu Chaulembo, alisema wamejipanga kimkakati kuviinua vyanzo vyoye vya mapato.

Anasema, kwa miaka ya nyuma hawakuwa wanafanya vizuri katika suala zima la ukusanyaji mapato, akitamka:" Tumepata Mkurugenzi (Mtendaji) mpya, Mohamed Mavula, ambaye ana uwezo katika kusimamia ukusanyaji wa mapato."

Anaongeza kwamba, halmashauri ina vyanzo mbalimbali vya mapato, ikiwamo mapato ya korosho na kiwanda cha samaki aina ya 'pronzi' ambacho kilifungwa miaka minane iliyopita na sasa kinatarajiwa kufunguliwa mwezi huu.

Chaulembo anasema awali katika soko la Kibiti hawakukusanya mapato kutokana na adha aliyowaita 'Mungu mtu', lakini kwa sasa Mkurugenzi huyo kaondoa ukiritimba uliokuwapo sokoni katika masuala ya ukusanyaji mapato.

Anasema, awali walikukutana na changamoto kubwa pale waliposanya mapato na sasa mkurugenzi mpya amesaidia kuondoa 'umwinyi' katika soko hilo, halmashauri ikifunguliwa kukusanya vyake.

Chaulembo anasema mapato ya Kibiti yanatokana na bajeti na kuongeza kuwa malengo ambayo wamejiwekea ni kuongezeka ukusanyaji wa mapato.

Kwa sasa anasema, wameweka vibarua wapya kwa ajili ya kukusanya mapato.

BARUA & MJADALA

# Baada plastiki, sasa magazeti

*Mhariri,*

*BAADA ya kutolewa nina-chokiita 'uamuzi mgumu' kuhusiana na marufuku ya matumizi ya mifuko ya plastiki, ni jambo lililopokewa kwa hisia nyingi tofauti.*

*Nasema 'namna tofauti' kwa maana ya kwamba kuna sura moja mifuko hiyo ilikuwa biashara kubwa katika jamii zetu, wapo walioitwa wafanyabiashara wakubwa, ama kupitia uwakala, kumiliki viwanda na hata kuuza kwa kiwango cha 'mabando.'*

*Pia hata wachuuzi na watumiaji wadogo kila mmoja alikuwa katika darasa la mnufaika. Kwa kifupi mifuko ya plastiki ndio 'mpango wa mjini.'*

*Ukijumuisha kundi hilo la wanufaika kupitia mantiki hiyo, hawakuitolea tabasamu hata kidogo uamuzi huo mgumu wa kiserikali.*

*Nikirudi katika upande wa pili wa shilingi, hakuna anayeweza kubisha mifuko hiyo iliyoenea kila mahali mjini kwa vijijini, imechafua sana mazingira.*


*Wataalamu hao wanaenda mbali zaidi, hata kuharibika kwake ni mtihani mkubwa inachukua zaidi ya karne kutoweka. Hiyo nayo ni hatari kubwa ya kimazingira.*

*Sasa katika mitaa yetu, mijini kwa vijijini ambako kuna uchuuzi wa maandazi, chapati, mihogo inayotumika zaidi kufungia ni makaratasi ya magazeti na menginyo.*

*Nayo ikifuatilia kuanzia mazingira ya biashara hiyo na vifungasho vyenyewe sio visafi hata kidogo jamani. Hapo ndipo natoa mkazo wa hatua inapaswa kuchukuliwa kukabili hali hiyo isiyoridhisha kiafya.*

**Abdul Kassim,**
**Pangani.**

# Dereva anapomvalisha abiria kofia za ujenzi, ni nini hasa?




**Na Yasmine Protace,**

TUNAPOZUNGUMZIA usalama barabarani, inabeba maana kubwa sana kwa jamii na hasa watumiaji wa vyombo vya moto, hata kwa watembea kwa miguu.

Usalama barabarani unapozingatiwa na jamii, hali hiyo inasaidia kuepesha ajali katika jamii.

Mtu anapokuja awe na gari la abiria au mengineyo, mara zote watumiaji wa vyombo hivyo wamekuwa wakitakiwa kufunga mkanda, ili kuwasaidia wasidhurike pale ajali inapotokea.

Nikirejea kwa ndugu zangu wa bodaboda waliotawanyika kila mahali nchini, wamelemaaa mno na tabia ya kulazimisha kubeba abiria wa ziada kupitia mtindo maarufu 'mshikaki.'

Wanaingia katika kosa hilo, wakati kuna ukweli unaoendelea kuwapo hudumu kwamba, bado hawajakidhi kigezo cha kisheria kinachowataka wavae kofia ngumu, kwa ajili ya usalama wao.

Kigezo kikuu cha kofia hizo maalum, ni kwamba panapotokea ajali, mtu anaweza kunusurika madhara ya kichwani.

Ukiangalia katika jiji letu la Mwanza, baadhi ya madereva wa bodaboda wamejenga mazoea ya kuvaa kofia zinazotumiwa kwenye 'saiti' za ujenzi wakiwapatia wateja wao kuvaa.

Dereva mmojawapo wa kituo cha bodaboda maeneo ya Makoroboi, anajitetea kwamba wanakumbana na changamoto kubwa katika kazi hiyo, kutokana na kukabidhiwa bodaboda bila ya kupatiwa kofia.

Anasema, wanatumia vyombo hivyo vya usafiri walivyokabidhiwa wakipeleka hesabu ya siku Sh. 7,000 na wale walioajiriwa kwa siku Sh. 10,000.

Mwendesha pikipiki huyo, anasema pamoja na kupeleka kiasi hicho cha fedha kwa wamiliki, bado wanashindwa kuwanunulia kofia ngumu, hali hiyo inawafanya watumie kofia zisizo rasmi.

Anasema, mtu anakabidhiwa pikipiki bila ya kofia na wakati huohuo anapokabidhiwa haina kofia kulazimika kutumia kofia za wajenzi kuwapa wateja wao.

Anasema, kofia moja mpya inauzwa Sh. 15,000, lakini wao wananunua mitaani zilizotumika kwa bei kati ya Sh. 7,000 na Sh. 8,000 kwa kofia za ujenzi.

Kuhusu upakiaji mtindo wa 'mshikaki' kwa abiria wa kawaida na watoto wa shule, anasema wazazi wenye vipato vidogo wanashindwa kumudu gharama za usafiri wa mabasi ya shule, hivyo inawalazimu kutumia usafiri wa bodaboda kuwapeleka watoto shule.

Anasema, ndicho ambacho baadhi ya abiria wanalazimika kupanda wakiwa hivyo, kuendana na uwezo wa mahitaji yao wakati wanahitaji huduma ya usafiri.

Kiongozi wa juu katika Kamati ya Taifa ya Usalama Barabarani, Foutunatus Sokoni, anasema sheria zinakataza kofia za kujengea kutumika katika bodaboda na kila bodaboda inatakiwa kuwa na kofia ngumu mahsusi kwa usafiri huo na sio zinazotumika kwenye ujenzi, ndio anapewa abiria.

Anakumbusha kuwa ni kosa la kisheria, kwa abiria kuvaa kofia za ujenzi anapokuiwa kwenye bodaboda, vivyo hivyo katika bodaboda, ni marufuku mtoto mwenye umri chini ya miaka tisa kupanda.

Anasema umri huo haufai mtoto kupakiwa katika bodaboda na anataja athari kubwa iliyopo, ni pamoja na za kiafya na katika kukabilian ana upungufu huo, Jeshi la Polisi, Kikosi cha Usalama Barabarani, kimeshatoa elimu kwa waendesha bodaboda katika baadhi ya mikoa.

Sokoni anataja baadhi ya mikoa husika ni Morogoro na Dodoma, kwamba elimu iliyotolewa imejikita zaidi kwa madereva kutovunja sheria za usalama barabarani, wanapokuwa kwenye vyombo vya moto.

**WASILIANA NASI:**

TUNAKARIBISHA BARUA NA MAONI YA MSOMAJI, UNAWEZA KUTUMA KUPITIA KWA MHARIRI S.L.P. 31042, DAR ES SALAAM AU mhariri@nipashe.co.tz

**KABWELA** Na Fadhili Mohammed



# Wamtaka Waziri Jafo kusuka au kunyoa

INATOKA UK. 2

**CHADEMA YAKOLEZA CHUMVI**

Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) kisisitiza kuwa hakitashiriki kama kilivyotangaza na kwamba kujitoa kwake kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa uliopangwa, hakumaanishi kutoshiriki uchaguzi mkuu mwakani.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Mkurugenzi wa Mafunzo wa Taifa wa chama hicho, Benson Kigaila, alisema wanakwenda kupanga mikakati kwa ajili ya ushiriki wa uchaguzi mkuu mwakani ili kupata ushindi wa kishindo.

"CCM wasitarajie kukosa upinzani katika uchaguzi mkuu. Tumejitoa kwa ajili ya kuwenda kuweka mikakati ambayo tutakuja nayo katika uchaguzi huo," alisema Kigaila.

Alisema hawatakubali kuona makosa kama hayo yanayojitokeza katika uchaguzi mkuu ujao na kuwataka wanachama wao kutohofia kujitoa kwao ili kutaka haki itendeke.

"Sisi tuko 'field' (kwenye eneo la tukio) lakini Waziri yuko ofisi ndiyo maana hajui wagombea wetu walichofanyiwa. Msimamo wetu ni ule ule kwamba hatutashiriki na hata wale waliobahatika kupata nafasi za kuwania nafasi mbalimbali za uongozi hawatashiriki," alisema.

Naye Ofisa Uchaguzi wa Kanda ya Kati wa chama hicho, Justine William, alisema wagombea wote wanapaswa kuheshimu kauli ya chama ambayo imewataka kutoshiriki katika uchaguzi huo na watakaoshiriki watakuwa wasaliti,

**TAMKO ACT WAZALENDO**

Ngome ya Wanawake wa chama ACT-Wazalendo, imemtaka Rais John Magufuli kukutana na viongozi wa vyama vya siasa ili kupata maridhiano na muafaka wa kisiasa kwa maslahi ya taifa.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, Mwenyekiti Chiku Abwao, alitaja mambo 12 wanayotaka yafanyike ili kuwa na uchaguzi huru na haki.

Alisema wanaunga mkono msimamo wa chama na kwamba kushiriki uchaguzi huo ni kubaka demokrasia kwa kuwa si wa haki, huru, wazi na hauna uwanja sawa wa kisiasa kwa vyama vyote.

Abwao alisema wanashangazwa na Waziri Jaffo, kwa kauli mbili mbili na kuonyesha kuwa anatumika kuvuruga uchaguzi.

"Historia itamhukumu kwa kuchezea usalama na amani ya nchi. Kwa kauli yake tunahoji kwani mgombea binafsi ameruhusiwa?" alisema.

Kwa mujibu wa Mwenyekiti huyo, inahitajika amani, uhuru, usawa wa kufanya shughuli za kisiasa nchini urejeshwe kama ilivyokuwa kwa awamu zilizopita kwa kile alichodai utawala wa vitisho hauwezi kuwa suluhisho la matatizo ya Watanzania ikiwamo ukosefu wa ajira, umasikini, ukosefu wa dawa hospitalini na miundombinu mibovu.

Alisema vitisho haviwezi kutunyamazisha, tutaendelea kuikosoa serikali ya CCM na kudai Haki zetu za Kikatiba kwa mujibu wa sheria.

**CCM WANENA**

Chama Cha Mapinduzi (CCM) kimesema mchakato wa uchaguzi huo upo sawa na kutoa safu namna ambavyo kimewapanga watu wake kushiriki kuanzia ngazi ya chini hadi juu.

Akizungumza jana na waandishi wa habari, Katibu wa Itikadi na Uenezi wa chama hicho, Humphrey Polepole, alisema kama wapinzani waliona wameonewa walipaswa kukata rufani.

Alisema CCM itashiriki katika uchaguzi huo kupongeza msimamo uliotolewa hadi sasa na serikali.

**● Imeandikwa na Salome Kitomari, Romana Malya (DAR) na Renatha Msungu (DODOMA)**

# Mkapa apongezwa kila kona



Distributed via ippmedia

INATOKA UK. 2

hicho juzi, kumeibuka mijadala kwenye mitandao ya kijamii kuhusu kiongozi huyo kutoyaongelea hadharani baadhi ya mambo hadi amesubiri kuyazungumzia kwenye kitabu.

Dk. Kahangwa alisema kuibuka kwa mijadala hiyo kunaonyesha kuwa kitabu hicho kitaisaidia serikali kuchukua hatua juu ya mambo mbalimbali yanayotokea.

Rais wa Chama cha Wanasheria Tanganyika (TLS), Dk. Rugemeleza Nshala, pia alimpongeza Mkapa (pichani) kwa kuandika kitabu hicho na kusema ni jambo linalowatia watu moyo.

Alisema ndani ya kitabu hicho, Mkapa anaeleza makosa yaliyowahi kufanyika na majuto yake, hivyo ni funzo kwa jamii kuwa watu wanakosea na wajifunze kutorudia makosa.

**WABUNGE WAMPONGEZA**

Bungeni jijini Dodoma, baadhi ya wabunge wamempongeza Mkapa kutoa kitabu kinachohusu maisha yake, wabunge wamemmiminia sifa kiongozi huyo kwa kusema amefanya jambo la ujasiri.

Wakizungumza na Nipashe kwenye viwanja vya Bunge jana, watunga sheria hao walimwelezea Mkapa kuwa ni shujaa na jasiri kwa uamuzi wake wa kuweka wazi mambo yaliyojificha, ambayo Watanzania wengi walikuwa hawayajui.

Mbunge wa Bumbuli, January Makamba (CCM), alisema Rais Mkapa ameandika historia ambayo itabaki kwa vizazi na vizazi.

"Ninampongeza kwa uamuzi wa kuandika kitabu, viongozi wengi wa Afrika wanapomaliza muda wao wa madaraka, huwa hawana utaratibu wa kuandika kitabu," alisema Makamba.

"Amekuwa mkweli, nampongeza kwa kuwa ameamua kufanya jambo la ujasiri litakazoanzisha mjadala, kuamua maoni yake yajadiliwe. Nina imani hata Mzee (Ali Hassan) Mwinyi na (Jakaya) Kikwete wataiga mfano huu."

Mbunge wa Vunjo, James Mbatia (NCCR-Mageuzi), alisema: "Kitabu cha Mkapa kimechukua falsafa ya 'Dunia ni kijiji' na Tanzania ni tone ndani ya Dunia, mabadiliko ya kasi ya Dunia tangu ilipoumbwa ni makubwa, kila kilichokuwa kwenye giza, kesho kitakuwa kwenye nuru."

Mbatia alisema kikubwa cha kujifunza kupitia kitabu hicho cha Mpaka ni unyenyekevu na kuwa na tahadhari katika kufanya uamuzi, akieleza kuwa kiongozi huyo amewafundisha Watanzania kuwa makosa yaliyotokea katika utawala wake, hatarajii yatokee katika utawala wa sasa na ujao.

"Mkapa anatuambia ni lazima tujirudi, hisia, kunuia, kunena kwetu kufanane na matendo yetu, anatufanya tuwe chanya kuliko 'negative' (hasi)," alisema Mbatia.

Aliongeza kuwa kupitia kitabu hicho, Mkapa ameonyesha hisia kwamba nafsi yake inamsuta kutokana na uamuzi aliowahi kuuchukua wakati akiwa madarakani, akitolea mfano machafuko ya Zanzibar.

"Nampongeza kwa unyenyekevu wake akiwa hai, matendo mema aliyoyafanya, yamekuwa sauti huru akiwa hai na akiwa hayupo duniani. Ninamtakia kila la heri ya kuishi maisha mengi zaidi ya miaka 81 aliyotimiza sasa," alisema Mbatia.

Mbunge wa Busokelo, Atupele Mwakibete (CCM), alisema Rais Mkapa amefanya jambo la kiungwana na kizalendo kwa kuandika kitabu hicho. Alisema viongozi wengine wanapaswa kumuiga.

"Inatufundisha viongozi waliopo na waliostaafu kufanya hivyo, ni wakati mwafaka kwani itaacha alama kwa vizazi vya baadaye kufahamu mambo yaliyofanywa, ni njia sahihi ya kuhifadhi matukio," alisema.

Mbunge wa Rombo, Joseph Selasini (Chadema) alisema: "Mambo mengi aliyoyaandika yamekuwa ni mafunzo kwa kizazi kijacho, ni mafundisho kwa viongozi na namna ya kufanya mambo yetu. Jambo lililonifurahisha ni kukiri kuwa kulikuwa na upungufu katika utawala wake."

Mbunge wa Ndada, Cecil Mwambe (Chadema), alisema Mkapa amefanya jambo la busara, lakini amechelewa.

Alisema Mkapa alikuwa Rais wa Tanzania miaka 15 iliyopita, hivyo alipaswa kuandika mapema zaidi ili viongozi waliompokea madaraka, wawe na tahadhari kuhusu mambo aliyoyaandika katika kitabu chake hicho.

Mbunge wa Viti Maalum, Hawa Mwaifunga (Chadema), alisema: "Nampongeza kwa uamuzi wake, ni jambo la ujasiri, limeshtua wengi kwa uamuzi wa kuweka wazi maisha yake, suala la EPA limenishtua hata mimi."

Juzi, Mkapa alizindua kitabu chake hicho alichokiita 'My Life, My Purpose' (Maisha Yangu, Kusudi Langu), akieleza mambo mbalimbali hasi na chanya yaliyotokea katika maisha yake pamoja na alipokuwa madarakani kuanzia mwaka 1995 hadi 2005.

**●Imeandikwa na Gwamaka Alipipi (DODOMA) na Mary Geofrey (DAR).**

# ...Zitto amsifia kusema ukweli

INATOKA UK. 2

Mambo mapya

Kwa mujibu wa Zitto, wasomaji wa kitabu hicho watafurahia historia ya nchi kwa kuwa Mkapa alifanya kazi karibu na Hayati Mwalimu Julius Nyerere. Kadhalika, alisema katika kitabu hicho kuna mambo mapya unayapata kuhusu Nyerere kama wakati wa vita ya Uganda, alikuja Rais wa Sudan, Jaffar Nimeiry kujaribu kusuluhisha.

"Mwalimu alimwambia Mkapa, yaani hata huyu anaongelea demokrasia, ameingiaje madarakani? Mwalimu alimpotezea Rais huyo. Kuna simulizi tele kuhusu ukombozi wa Afrika na namna sera yetu ya mambo ya nje ilivyokuwa inatekekezwa," alisema Zitto.

Alisema Mkapa ametoa mafunzo kwa viongozi wa sasa na wa baadaye kuhusu msingi wa maamuzi mengi ya nchi yetu.

Kwa mujibu wa Zitto, kuna mambo Mkapa hakusema na ingetupa maarifa sana, akitolea mfano vita ya uasi Jimbo la Biafra nchini Nigeria na maamuzi ya Mwalimu kuunga mkono waasi Biafra.

Alisema Mkapa anaeleza kuhusu yeye kuwa balozi nchini humo baada ya vita na ziara ya Mwalimu Nigeria, lakini haelezi kwa undani hali ulikuwaje?

"Alipofika Nigeria watu walikuwaje? Mzee Obasanjo alipata kunihadithia kuwa ilibidi amsindikize Mwalimu kila mahala kwenye ziara ile kwa sababu wa Nigeria walikuwa na hasira na Tanzania, Zambia, Gabon na Ivory Coast kwa kutambua uasi wa watu wa kabila la Igbo," alisema na kuongeza:

"Nilitaraji Rais Mkapa angesema zaidi eneo hili. Hapa ametunyima uhondo."

**MKAPA AKEMEE YANAYOENDELEA**

Kwa mujibu wa Zitto, Rais Mkapa anapaswa kukemea yanayoendelea nchini haswa ukandamizaji wa demokrasia na kuwatenga wapinzani.

Zitto alisema Mkapa ameonyesha kuhusu kuumizwa na mambo hayo kwenye kitabu, lakini hakemei hadharani.

"Sura ya mwisho ya kitabu chake ni malalamiko ya namna Afrika inaendeshwa na haswa Tanzania na mambo mengi asiyoyapenda hayasemi hadharani. Kama Rais mstaafu anapaswa kusema na kuonya. Wasipoonya sasa wasionye nchi ikiwa kwenye machafuko," alisisitiza Zitto.

Aidha, alisema amefurahishwa na jinsi Mkapa alivyoeleza maisha yake ya utoto na makuzi, ikiwamo maisha yake ya ujana pale Chuo Kikuu cha Makerere.

"Sikujua kuwa Rais Mkapa alikuwa na 'demu' wa Kimarekani akiitwa Hilary. Pia alipenda sana dansi na siasa za wanafunzi. Mungu ampe maisha marefu zaidi Mzee Mkapa," alimalizia Zitto.

# Shehena mifuko mbadala chini kiwango yateketezwa

**Na Mwandishi Wetu,**
MWANZA

BARAZA la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) limeteketeza zaidi ya mifuko mbadala milioni mbili iliyotengenezwa chini ya kiwango na kiwanda cha Jin Yuan Investment kilichopo jijini Mwanza na gunia nane ya vifungashio viliyoingizwa nchini kwa njia za magendo.

Akizungumza baada ya kufanya zoezi la uteketezaji wa mifuko hiyo jijini Mwanza, Mkurugenzi Mkuu wa NEMC, Dk. Samuel Gwamaka alisema zoezi hilo liwe onyo kwa wazalishaji wengine ambao hawafuati utaratibu na kanuni za viwango zilivyoweka za 70 gsm ili kulinda soko la ndani la bidhaa hizo.

"Lengo letu ni kulinda viwanda vya ndani ili vipande masoko ya bidhaa Wanazozalisha, lakini imekuwa ni kinyume kwa wawekezaji kuzalisha mifuko iliyochini ya kiwango cha gsm 70 ambayo imepitishwa na Shirika la Viwango nchini (TBS)," alisema Dk.Gwamaka.

Alisema hali hiyo inachangia udhibiti wa mifuko inayotoka nje ya nchi kuwa mgumu, hivyo Baraza kuanzisha ukaguzi nchi nzima kwa lengo la kubaini wazalishaji wa ndani wasiofuata taratibu na kuwachukulia hatua ikiwamo kuteketeza bidhaa na kuwapiga faini.

"Wazalishaji wakifuata sheria na viwango vilivyowekwa vya 70 gsm na uwekaji nembo ya mzalishaji kwenye mifuko inayozalishwa nchini itasaidia kubaini mifuko iliyochini ya kiwango na kufanya wepesi kwa mamlaka kushukua hatua," alisema Dk. Gwamaka.

Aliongezea kuwa azma ya serikali ya awamu ya tano inayoongozwa na Rais John Magufuli ni kujenga uchumi wa kati na viwanda, hivyo NEMC ipo katika kutekeleza azma hiyo kwa kushirikiana na wawekezaji kwa kutoa elimu na miongozo mbalimbali juu ya umuhimu wa utunzaji wa mazingira.

"Niwaombe wafanyabiashara kuacha kuingiza mifuko mbadala kutoka nje ya nchi iliyochini ya kiwango kwa kufanya hivyo wanakuwa wanahujumu uchumi wa nchi pamoja na wawekezaji wa ndani kwa kuleta bidhaa zilizochini ya kiwango," alisema.

Alisema NEMC itaendelea na ukaguzi ili kuhakikisha bidhaa za mifuko mbadala inayozalishwa nchini inafuata sheria na viwango vilivyowekwa ikiwa ni pamoja na kuweka nembo na anwani ya mzalishaji, uzito unaoweza kubebwa na mfuko huo.

Alitoa rai kwa wananchi kuachana na matumizi ya mifuko isiyo na nembo ya mzalishaji kwani inapeleka kuua soko la mifuko mbadala inayozalishwa nchini na kwa kufanya hivyo watakuwa wanashiriki katika uhujumu uchumi na kuendelea kutumia mifuko hiyo toa taarifa kwa wazalishaji wanaokwenda kinyume cha sheria.

Aidha, baraza limewataka wazalishaji wote walipigwa faini kwa kosa la kuzalisha mifuko iliyochini ya kiwango kuzilipa faini hizo ndani ya muda uliowekwa pamoja na kuteketeza kwa moto bidhaa au kuzirejeleza na kufanya uzalishaji unaofuata viwango na kanuni zilizowekwa.

Mjumbe wa Bodi ya NEMC, Damas Masologo, alisema baraza lipo katika kutekeleza sheria za nchi katika kutunza mazingira na sio kuvifungia viwanda tutaendelea kutoa elimu kwa wawekezaji nchini ili waendane na kanuni na sheria za nchi.

"Tunashukuru uongozi wa kiwanda cha Nyakato Steel Mills kwa kutoa nafasi katika kiwanda chake ili kuteketeza mifuko hiyo pasipo kuathiri mazingira katika zoezi la uteketezaji," alisema Masologo.



Mratibu wa Shirika linalotetea haki za wazee la Tawlae, Eliasenya Nnko, akiwasilisha mada ya kutetea haki za wazee ikiwamo kutokomeza mauaji ya wazee kwa wakuu wa wilaya za Bukombe, Magu, Busega na Shinyanga wakiwamo pia wakuu wa Jeshi la Polisi kutoka wilaya hizo, katika kikao kilichofanyika Shinyanga Mjini jana. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Ushirika wapokea bil. 9.3/- kuwalipa wakulima korosho

**Na Hamisi Nasiri,** MASASI

CHAMA Kikuu cha Ushirika wa Wakulima Mtwara-Masasi (MAMCU) kimesema kimeshapokea fedha za wakulima zaidi ya Sh. bilioni 9.3 kutoka kwa wafanyabiashara walionunua korosho za mnada wa kwanza ili wakulima walipwe.

Aidha, fedha hizo MAMCU imeshaziingiza kwenye akaunti za vyama vya msingi (AMCOS) vya Masasi Mji, Masasi Vijiji na Nanyumbu ili ziwafikie wakulima.

Hayo yalibainishwa jana na Kaimu Meneja wa MAMCU tawi la Masasi, Jafari Mkata, alipokuwa akizungumza na Nipashe kuhusu malipo ya korosho za mnada wa kwanza uliofanyika Oktoba 31, mwaka huu.

Alisema MAMCU hadi juzi imeshapokea Sh. bilioni 9.3 kwa ajili ya malipo ya wakulima kupitia mnada wa kwanza uliofanyika katika Kijiji cha Chiungutwa Masasi na fedha hizo watalipwa wakulima kuanzia muda wowote kutoka sasa. Alisema katika msimu huu wa korosho wa mwaka 2019/2020, fedha za wakulima waliouza korosho mnada wa kwanza zimeshafika na bàadhi ya vyama vya msingi vimeanza kupokea.

Mkata alisema katika mnada wa kwanza uliofanyika katika kijiji cha Chiungutwa Masasi, MAMCU kiliuza jumla ya kilo za korosho 3,642,559.

Alisema bei ya juu katika mnada huo ilikuwa Sh. 2,559 na bei ya chini Sh. 2,409, na kueleza kuwa katika mnada wa kwanza jumla ya maombi ya kununua korosho yaliyowasilishwa yalikuwa 27.

Aliongeza kuwa katika mnada wa pili ambao fedha zake wanunuzi hawajalipa hadi sasa uliofanyika katika kijiji cha Michiga wilayani Nanyumbu, jumla ya kilo 9,368,810 ziliuzwa, huku bei ya juu ikiwa Sh. 2,712 na bei ya chini ilikuwa Sh. 2,510.

"Sh. bilioni 9.3 ambazo tumezipokea ni za wakulima wa Masasi Mji, Masasi Vijijini na Nanyumbu, na vyama vya msingi tumeshaanza kuviingizia fedha ili walipwe wakulima," alisema Mkata.

Iman Suya kiongozi wa Chama cha Msingi Mumbaka ( AMCOS) Halmashauri ya Mji Masasi, alithibitisha chama chake kupokea fedha za wakulima kwa ajili ya malipo.

Naye Ajili Issa, mwenyekiti wa Chama cha Msingi Nanyindwa (AMCOS), alisema iwapo fedha za korosho za wakulima zikiwa zinalipwa mapema kama hivi, itasaidia kupunguza malalamiko.

# Mashamba, mirathi chanzo mauaji wazee

**Na Marco Maduhu,**
SHINYANGA

MIGOGORO ya mashamba na mirathi, imetajwa kuwa changamoto kubwa ambayo imekuwa ikisababisha kuendelea kuwapo na mauaji ya wazee kwenye maeneo mengi nchini.

Hayo yalibainishwa jana na wakuu wa Jeshi la Polisi kutoka wilaya za Bukombe, Magu na Shinyanga, kwenye kikao cha Shirika la Tawlae linalotetea haki za wazee nchini, kilichoshirikisha pia wakuu wa wilaya hizo, kwa lengo la kujadili na kubadilishana mbinu za kutokomeza mauaji ya wazee.

Wakuu hao wa Jeshi la Polisi kutoka wilaya hizo, walisema licha ya mauaji ya wazee kupungua kutokana na imani potofu za kishirikina, sasa vimeibuka vyanzo vipya vya kutekeleza mauaji hayo ambavyo ni migogoro ya mashamba na mirathi.

Mkuu wa Polisi kutoka Wilaya ya Bukombe, Elisha Kusulla, alisema hivi sasa wanashughulika na kesi ya kijana mmoja, ambaye alikuwa amepanga njama za kumuua mama yake ambaye ni mzee, ili apate kurithi ng'ombe 30 ambazo zilinunuliwa na mama huyo.

"Bukombe tumefanikiwa kupunguza mauaji ya wazee kwa kupeleka askari kila kata, na wanaishi huko huko na jamii, na ndio maana hata taarifa hizi za kijana huyo kupanga njama tuliipata mapema," aliongeza.

Naye mwakilishi wa mkuu wa Jeshi la Polisi wilayani Magu, Vedasto Erasto, alitaja takwimu za mauaji ya wazee wilayani humo kuwa mwaka (2018) waliuawa wazee wawili, na mwaka huu (2019) mpaka sasa ameuawa mmoja.

Aidha, Mkuu wa Jeshi la Polisi Wilaya ya Shinyanga, John Kafumu, alitaja takwimu za mauaji ya wazee wilayani humo kuwa mwaka jana (2018) waliuawa watatu, na mwaka huu (2019) mpaka sasa ameuawa mmoja.

Mratibu wa Tawlae, Eliasenya Nnko, alisema wamefanya kikao na wakuu wa wilaya na polisi ambayo wanatekeleza mradi wa kupigania haki za wazee ikiwamo kutokomeza mauaji dhidi yao.

## 'Hakuna kulipia nguzo'

WAZIRI wa Nishati, Dk. Medard Kalemani, ameliambia Bunge kuwa mteja yeyote awe wa mjini au kijijini hapaswi kutozwa gharama ya nguzo na yeyote atakayetozwa atoe taarifa kwa mamlaka husika ili wahusika wachukuliwe hatua.

Dk. Kalemani aliitoa kauli ya msisitizo wa katazo hilo jana wakati akijibu mwongozo wa Mbunge wa Ulanga (CCM), Goodluck Mlinga, uliotokana na swali la msingi la Mbunge wa Kibiti (CCM), Ally Ugando ambaye alidai kuwa wananchi wa Jimbo la Kibiti maeneo yaliyofikiwa na umeme baadhi yao wamekuwa na adha kubwa kwa kuwa wamelipa nguzo na mita kwa fedha zao lakini Tanesco wameshindwa kutimiza wajibu wao.

Akiomba mwongozo huo, Mlinga alisema serikali imetangaza wananchi hawapaswi kulipia nguzo wala kulipia mita na waya.

"Wananchi walipokea taarifa hiyo kwa vifijo na nderemo na matokeo yao wakaruhusu maeneo yao nguzo zipite bila kulipwa fidia, Mwenyekit, Rais wetu ametangaza ni Sh. 27,000 kuunganishiwa umeme, Waziri Mkuu ametangaza pia na Waziri wa Nishati ametangaza umeme ni Sh. 27,000," alisema.

Alibainisha kuwa wananchi wanapokwenda kukutana na watendaji wa Tanesco wanapotaka kuunganishiwa umeme wanatozwa Sh.100,000 hadi Sh. 1,000,000 na kuhoji Mtanzania anapaswa kulipa kiasi gani.

Akijibu mwongozo huo, Waziri Kalemani alisema kauli ya serikali ni kuwa malipo yote ya kuunganisha wateja vijijini ni kiasi cha Sh. 27,000 tu nchi nzima na kuwatahadharisha watumishi Tanesco, kuwa atakayebainika anatoza fedha kubwa kwenye uunganishaji umeme nchini atafukuzwa kazi.

"Kwa mantiki hiyo, meneja yeyote haruhusiwi kwa namna yoyote kutoza zaidi ya Sh. 27,000, na mtaalamu yeyote atakayebainika amefanya kitendo hicho atachukuliwa hatua kali za kinidhamu ikiwamo kusimamishwa kazi," alisema.

Aidha, alisema kutoza nguzo wateja wote hawaruhusiwi kutozwa gharama za nguzo iwe mijini ama vijijini.

Awali, akijibu swali la Mbunge wa Kibiti, Naibu Waziri, Subira Mgalu, alisema awali Tanesco ilikuwa inategemea kupata nguzo kutoka kwa mzabuni mmoja tu ambaye hakuwa na uwezo wa kukidhi mahitaji yote ya nguzo kwa wakati.

"Hivi sasa kuna viwanda tisa vya nguzo hapa nchini, kwa upande wa mita jumla ya viwanda vitatu vipya vimeanzishwa vyenye uwezo wa kuzalisha mita 2,000,000 wakati mahitaji ya mita kwa miradi ya Tanesco na REA ni mita 1,090,000," alisema.

Alisema baada ya kuongeza uwezo wa upatikanaji wa vifaa vya kuunganishia huduma ya umeme nchini, Serikali imeiagiza Tanesco kuhakikisha kuwa wateja wote wanaolipia huduma ya umeme wanaunganishwa katika kipindi cha mwezi mmoja.

"Aidha, kupitia mgawo wa nguzo wa mwezi Oktoba, 2019, nguzo zimeanza kusambazwa kwa kila mkoa na kupelekwa katika maeneo ya Wilaya mbalimbali nchini. Hivyo, Wilaya ya Kibiti ni miongoni mwa wilaya iliyopelekewa nguzo kwa ajili ya kuunganisha wateja wote waliolipia hadi kufikia tarehe 31/11/2019," alisema.

# Bashe aagiza kurejeshwa bil. 4.5/- viuatilifu korosho

NAIBU Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, amemwagiza Mtendaji wa Kampuni ya Bajuta kurudisha kiasi cha Sh. bilioni 4.5 za viuatilifu vya zao la korosho zilizotolewa na Ofisi ya Hazina kwenda kampuni ya Mbolea Tanzania (TFC).

Agizo hilo alilitoa jana alipokuwa akijibu swali la nyongeza la Mbunge wa Lupa (CCM), Victor Mwambalaswa, ambaye alisema tatizo la viuatilifu na pembejeo za zao la korosho kufika kwa wananchi kwa wakati limekuwa changamoto kubwa.

"Serikali ina kauli gani kuhusiana na suala hilo na kwanini pembejeo hizo zimechelewa?" Alihoji. Akijibu swali hilo, Bashe alikiri kuna changamoto hiyo na kwamba hatua zilizochukuliwa na serikali ni pamoja na kumsimamisha Mtendaji Mkuu wa TFC kama hatua ya awali kwa uzembe huo.

"Baada ya kumsimamisha tulimwagiza mfanyabiashara aliyepewa fedha za umma Sh. bilioni 4.5 kati ya Sh. bilioni 10 kinyume cha maelekezo ya serikali arudishe fedha hizo serikalini na naomba kupitia Bunge lako kuwaonya watendaji wa wizara kuwa yeyote atakayetumia vibaya fedha za umma katika nafasi yoyote alipo hatavumiliwa," alisema.

Aidha, alisema wameshaanza kuchukua hatua kama wizara kwa ajili ya kutoa pembejeo hizo bandarini kwa kuongeza na Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA) na wamekubali kuondoa gharama zote.

"Pamoja na TPA kukubali pia kampuni ya Azam imekubali kutuondolea gharama za uhifadhi na sasa hivi tupo hatua za mwisho kufanya mchakato wa kuvitoa viuatilifu hivyo kabla havijaharibika ili kuwagawia wakulima wa korosho kwenye msimu ujao," alisema.

Bashe alifafanua kuwa Septemba mwaka huu akikagua kontena zaidi ya 350 za mbolea na viuatilifu, aliiagiza Bodi ya Korosho nchini kuhakikisha Sh. bilioni 10 kutoka Hazina zilizotolewa kwa ajili ya kununua mbolea na viuatilifu kwenye zao la korosho zinarejeshwa Hazina, baada ya bodi hiyo kuzitumia kinyume na maelekezo ya serikali.

Septemba mwaka huu akiwa katika ziara hiyo, Bashe alisema kuna kampuni inaitwa Bajuta imepewa Sh. bilioni 4.5 kati ya Sh. bilioni 10 na Bodi ya Korosho zilizotolewa na hazina kwenda kwa TFC, wakati Bodi ya Korosho inafanya maamuzi hayo hayakuwa ni maamuzi ya serikali.

"Naagiza ufanyike ukaguzi maalum na ukaguzi wa uwezo kwa kampuni ya pembejeo na viuatilifu ya Bajuta, juu ya mnyororo wa usambazaji pamoja na usambazaji wa pembejeo katika sekta ya kilimo na ukaguzi huo usifanywe na Wizara ya Kilimo bali ufanywe na Hazina ili viongozi wote waliobadilisha matumizi ya Sh. bilioni 10 zilizoelekezwa kwenda Kampuni ya Mbolea wachukuliwe hatua mara moja."



Distributed via ippmedia

Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, akizungumza na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Dk. Edalardus Kilangi, bungeni jijini Dodoma, jana. **PICHA: OWM**

# Tanzania yasaini mikataba kimataifa 12 bila kuridhia

IMEELEZWA kuwa serikali ina jumla ya mikataba ya kimataifa 42 ambayo imesaini, lakini haijaridhiwa na Bunge kwa sababu inaendelea kufanyiwa tathmini ya kina ili kubaini athari zinazoweza kujitokeza katika utekelezaji wake.

Aidha, hadi hivi sasa Tanzania imesaini na kuridhia mikataba ya kimataifa 39.

Hayo yalielezwa jana Bungeni na Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Dk. Damas Ndumbaro, alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Mafinga Mjini (CCM), Cosato Chumi.


Mbunge huyo alihoji mikataba mingapi ya kimataifa ambayo nchi imesaini, lakini haijaridhiwa na kama kuna athari zozote kwa nchi kutoridhia mikataba ambayo tayari nchi imesaini.Akijibu, Naibu Waziri huyo alisema Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki ina jukumu la kuratibu na kusimamia mikataba na makubaliano ya kimataifa inayohusisha ushirikiano kati ya nchi yetu na nchi nyingine (Bilateral Agreements), taasisi za kikanda na kimataifa (Regional and International Treaties and Conventions).

Alifafanua mikataba hiyo inatofautiana kwa maudhui na umuhimu lengo na madhumuni ya mikataba hii ni kuiwezesha nchi kudumisha na kuimarisha ushirikiano uliopo na nchi nyingine, jumuiya za kikanda na kimataifa kwa maslahi ya Taifa.


"Kupitia mikataba hiyo Tanzania imeweza kusimamia majukumu mbalimbali ya kimataifa kwa kushirikiana na nchi nyingine na taasisi mbalimbali na kunufaika na fursa za kiuchumi, kisiasa na kijamii, nchi yetu inatumia utaratibu wa kisheria wa kutobanwa moja kwa moja na mikataba ya kimataifa mara tu inaposainiwa (Dualism)," alisema.

Aidha, alisema utaratibu huo unatoa nafasi kwa nchi kuanza mchakato wa ndani ambao ni shirikishi kwa sekta husika kuandaa waraka wa Baraza la Mawaziri kuhusu mkataba huo kwa ajili ya kuridhiwa ndani ya serikali kabla ya kuidhinishwa na Bunge.

"Hivyo, hakuna athari zozote kwa nchi yetu kutoridhia mikataba ambayo tayari tumesaini kwa kuwa nchi yetu inafungwa na mikataba ya kimataifa baada ya kuridhiwa na Bunge," alisema.




**Habari zote na Augusta Njoji,** DODOMA





Waongoza watalii katika milima, wakionyesha namna ya kumsaidia mgonjwa aliyepata tatizo la uti wa mgongo, wakati wa mafunzo ya namna ya kutoa huduma ya kwanza kwa wageni yaliyotolewa na wataalamu kutoka kampuni ya utafutaji ya uokoaji ya Kilimanjaro SAR, jijini Arusha juzi. **PICHA: DIXON BUSAGAGA**

# Mpango wa kupanga ardhi, matumizi waja

Distributed via ippmedia

**Na Allan Isack,** ARUSHA

WIZARA wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi imesema hadi kufikia mwaka 2030, itakuwa imekamilisha mpango wa upimaji wa ardhi hapa nchini sambamba na kutoa hati miliki ili kupunguza migogoro na kuiongezea thamani.

Mpango huo utaendana na hatua ya kupanga matumizi sahihi ya ardhi, sambamba na kuoanisha sera ya watumiaji wa rasilimali mbalimbali zilizopo kwenye jamii ikiwamo misitu, maji na madini.

Akizungumza jijini Arusha wakati wa mkutano wa majadiliano, maridhiano ya matumizi sahihi ya ardhi kwa nchi za Afrika, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, alisema mkutano huo ni muhimu kwani umekuja muda mwafaka wakati serikali ikiwa kwenye mchakato wa kuandaa mpango wa upimaji wa ardhi nchini. Alisema mkutano huo, umeshirikisha zaidi ya nchi 20, kutoka Bara la Afrika na mpango ukiwa ni kuweka matumizi sahihi ya ardhi. "Tumefanikiwa kupima ardhi kwenye wilaya tatu za Mkoa wa Morogoro ambazo ni Malinyi, Ulanga na kutoa hati zaidi ya laki tano za kimila kwa kipindi cha miaka minne, ajenda inayoendelea kwa sasa ni kupanga, kupima na kumilikisha ardhi yetu," alisema Lukuvi.

Mkurugenzi wa Tume ya Taifa Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi chini ya Wizara hiyo, Dk .Steven Nindi, alisema eneo la Tanzania lina ukubwa wa takribani kilomita za mraba milioni moja, hivyo katika mkutano huo wataangalia namna ya kupata rasilimali fedha na rasilimali watu ili kuharakisha zoezi zima la upangaji, usimamizi na utekelezaji wa matumizi bora ya ardhi. Alisema lengo la mkutano huo, ni kuhakikisha ardhi yote nchini, inapimwa, kupangwa na kuwekewa matumizi bora na endelevu kwa maendeleo ya rasilimali za nchi ikiwamo misitu, maji na madini.

Alisema serikali itahakikisha inaweka sera ambayo itasaidia kuongeza wigo na kuhimiza fursa ya matumizi bora ya rasilimali mbalimbali za ardhi.

Mwenyekiti wa Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi, Wakili Fidelis Mutakyamilwa, alisema kwa kipindi cha miaka kumi ijayo Tanzania itakuwa imekamilisha mpango wa matumizi bora ya ardhi ambapo itasaidia kuondoa migogoro ya muda mrefu nchini.

Alisema mikoa ya Morogoro na Arusha inaongoza kwa migogoro ya ardhi, alisema kwa mikoa hiyo kuna ongezeko la mifugo jambo ambalo limepelekea migorogoro ya wafugaji na wakulima wakigombea malisho, wengine wakiwa ndani ya hifadhi.

# Vigogo madini Tanzanite sasa wakubali yaishe

**Na Allan Isack,** MIRERANI

WAFANYABIASHARA 28, wa madini ya Tanzanite wakiwamo kutoka katika bara la Asia na baadhi ya wamiliki wa migodi ya madini hayo, wameitwa katika ofisi ya madini Mirerani wilayani Simanjiro mkoani Manyara ili wakatoe taarifa ya kiasi cha madini wanayomiliki.

Kwa mujibu wa barua ya Ofisa Madini Mkazi wa Mkoa wa Kimadini wa Simanjiro, Daudi Ntalima, imewataka wamiliki hao wa migodi, madalali na wanunuzi wa madini hayo kufika ofisini kwake kuanzia Novemba 12 hadi 14 mwaka huu.

Ntalima alisema shughuli hiyo itafanyika ofisi kwake kwa siku tatu mfululizo kuanzia Novemba 12 hadi Novemba 14.

Alisema wahusika wote wameshaandikiwa barua wakiwamo ambao siyo wanachama wa chama cha wafanyabiashara wa madini nchini (Tamida).

Aliwataka wahusika wote kuhudhuria ili kutoa taarifa kamili ya madini waliyonayo pamoja na mwenendo wa biashara ya madini hayo kwa lengo la kujenga taifa bora.

Wafanyabiashara hao walioandikiwa barua na kutakiwa kutii wito huo ni Hussein Lemali, Emmanuel Wado (Sunda), Saitoti, Tarimo, Bima, Hamad Mjaluo, Manesh Kotog, Edward Mollel na George Kivuyo.

Wengine ni Ben Nkya, Peter Periera, Sam Mollel, Rakesh, Vinal, Reno, Bima, Rajan, Saran, Sailesh, Sidor, Faisal, Jitu, Muller, Shah, Sumil na Frizble.

Oktoba 29, mwaka huu Ntalima, alitaja majina ya vigogo wenye kumiliki madini ya Tanzanite ofisini kwao na aliwataka wafike ofisini kwake ili watoe taarifa zao.

Mmoja kati ya wakazi wa Mji mdogo wa Mirerani, Hawa Athuman, alisema baadhi ya watu hawakuamini kama serikali ingeweza kuwaita wafanyabiashara hao na wakatii amri hiyo.

Naye Hamis Hamza, alisema tukio hilo ni zuri kwa serikali kwani inapokuwa na mashaka juu ya suala lolote hufanya mahojiano na watu ili kujiridhisha.

# RC aagiza kuezuliwa paa la shule

**Na Allan Isack,** MANYARA

MKUU wa Mkoa wa Manyara, Alexander Mnyeti, ameagiza kung'olewa paa la madarasa ya shule mpya ya sekondari Hangoni katika Kata ya Babati, iliyojengwa na wananchi kwa kushirikiana na serikali.

Mnyeti alitoa agizo hilo, baada ya kuwapo kwa mgogoro na mvutano baina ya wananchi wa mtaa wa Hangoni na Halmashauri ya Wilaya ya Babati.

Awali wananchi wa eneo hilo, waliamua kuanzisha ujenzi wa shule hiyo ili kupunguza adha ya wanafunzi wa eneo hilo kutembea umbali mrefu kufuata huduma ya elimu kwenye vijiji vya jirani.

Hali hiyo, imetokea baada ya wananchi wa eneo hilo kudai kulipwa fidia ya maeneo yao, yaliyotumika kujenga miundombinu ya shule hiyo ya sekondari. Mnyeti alisema lengo la kujengwa kwa shule hiyo, ni kupunguza adha ya wanafunzi kutembea umbali mrefu kufuata huduma ya elimu, lakini ameshangazwa na madai ya wananchi kutaka kulipwa fidia wakati ujenzi wa shule hiyo ni kwa manufaa yao.

Eneo lililotolewa na wananchi hao, lina ukubwa wa hekari saba na tayari vyumba vya madarasa sita pamoja na ofisi moja ya walimu vimeshajengwa baada ya wananchi hao kuomba kujengewa shule kwa ajili ya watoto kutatua changamoto inayowakabili watoto wao. Awali wananchi hao walifanya makubaliano na halmashauri hiyo, kuwapa maeneo mengine kutokana na halmashauri hiyo kutokuwa na fedha za kununua eneo hilo la ujenzi wa shule.

Hata hivyo, wameshaonyeshwa maeneo yao na halmashauri hiyo katika Kata ya Maisaka maarufu kwa jina la Makatanini, lakini wananchi hao walikataa maeneo hayo, kwa kile walichokidai kuwa maeneo waliyopewa yapo kwenye makorongo na hayana thamani sawa na maeneo waliyotoa.

"Mkuu wa Mkoa sisi tumetoa eneo hili kwa moyo wote na kwa makubaliano baina ya wanakijiji na halmashauri sasa kwanini tunaenda kupewa maeneo kwenye makorongo, pia hayapo sawa na yale tuliyotoa, kwa mfano mimi nimetoa eneo lenye ukubwa wa nusu heka kule, lakini halmashauri wamenipa eneo lenye ukubwa wa robo heka, kwa kweli siwezi kukubali tena maeneo hayo yapo mbali mno na tunapoishi," alisema Jamali Issa.

"Kwanini watupeleke mbali hivyo, wakati sisi tumetoa maeneo mazuri na tulikuwa tunalima mazao ya chakula ambayo tulikuwa tukula mwaka mzima," Isaa alisema.

Kutokana wananchi hao kutokuridhika na maeneo waliyopewa Mnyeti, aliwauliza uamuzi wa kujenga sekondari hiyo ulifanywa na nani, ambapo walimweleza kuwa ni halmashauri kwa kushirikiana na wananchi.

"Kama ni halmashauri kwa kushirikiana na wananchi ina maana nyie ndio mliosema shule ijengwe hapa, sasa kwa nini mnalalamika na sijui mnamlalamikia nani? kwa sababu nyie ndio mliotoa eneo hili," aliongeza Mnyeti. "Labda niwaambie tu nchi nzima kunapojengwa shule au ishu yoyote ya huduma za kijamii wananchi ndio wanatoa maeneo ya ujenzi, sasa mimi nawashangaa nyie mnamdai fidia," alisema Mnyeti.

"Mkurugenzi kama hawataki shule hii tusiwalazimishe ezueni mabati, toeni madirisha, milango na tofali pelekeni sehemu wanayotaka kujenga shule, haya ndio maamuzi yangu," alisema Mnyeti.

Mnyeti alimwagiza mhandisi wa halmashauri hiyo kuchukua vifaa vyote vilivyokuwa vitumike katika ujenzi huo.

# Wananchi wakumbushwa kupanda miti msimu huu

**Na Mary Mosha,** MWANGA

WANANCHI wametakiwa kupanda miti na kuitunza kipindi hiki cha mvua ikiwa ni jitihada za kulinda mazingira pamoja na kuondokana na tatizo la ukame.

Hayo yalibainishwa na Rais wa Klabu ya Rotary inayojihusisha na masuala ya utunzaji wa mazingira wilayani Mwanga, Lucy Samba, jana mara baada ya kumaliza kupanda miti katika kituo cha Afya cha Kisangara kilichopo kata ya Lembeni wilayani Mwanga mkoani Kilimanjaro.

Alisema kuwa, wananchi wengi hususani wa Wilaya ya Mwanga wamehamasika kupanda miti lakini hawaimwagilii hivyo kufa na kushindwa kufikia lengo walilojiwekea la kuondoa ukame

"Wananchi wameelewa kupanda miti lakini tatizo lipo katika uangalizi na kuihudumia miti hiyo ambapo hilo limekuwa halifanyiki hali inayopelekea miti hiyo kufa," alisema Lucy.

Alisema kuwa, klabu hiyo mwaka jana walipanda miti zaidi ya 3,000 lakini baada ya kupita na kukagua maendeleo yake walikuta mingi takribani 1,300 imekufa kutokana na uangalizi mdogo jambo ambalo linaweza kusababisha jangwa.

Aliongeza kuwa, kwa mwaka huu wamejiwekea malengo ya kupanda miti zaidi ya miti 4,000 katika maeneo mbali mbali ya Wilaya ya Mwanga ikiwamo Shule ya Sekondari Kisangara, Shule ya Msingi Kisangara pamoja na Kagongo na bwawa la Nyumba ya Mungu.

"Katika kuhamasisha upandaji wa miti Wilaya ya Mwanga sisi Rotary Klab tumejipanga kupanda miti 4,000 ndani ya wilaya yetu ambapo leo tumepanda miti 150 katika kituo cha Afya cha Kisangara," alisema Lucy.

Kwa upande wake, Mkurungenzi wa Halmashauri ya Mwanga, Zefrin Lubavu, alilishukuru shirika lisilo la kiserikali la Terre sans frontiers (TSF) kwa kushirikiana na Klabu ya Rotary kutoka nchini Canada pamoja Mwanga kuwekeza katika kulinda mazingira ikiwamo katika sekta ya afya katika wilaya hiyo.

Mratibu wa (TSF) Tanzania, Adkadi Urassa, alisema ndani ya wiki mbili wamewapima macho wananchi zaidi ya 1,000 na baadhi yao kuwapatia miwani bure pamoja na upimaji wa afya ya kinywa na meno.

# Wapinzani waonywa kulilia kuhurumiwa

**Na Paul William,** MOSHI

CHAMA Cha Mapinduzi Mkoa wa Kilimanjaro, kimewataka viongozi wa vyama vya upinzani kushiriki katika uchaguzi wa serikali za mitaa na kuacha kutafuta huruma za wananchi kwa kutoa kauli za uongo, za kuituhumu na kuilaumu serikali.

Hayo yalisemwa jana na Katibu wa CCM Mkoa, Jonathan Mabihya, wakati akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake kuelezea jinsi chama hicho kilivyojipanga kuhakikisha kinashinda kwa kishindo katika chaguzi za serikali za mitaa na vijiji.

Mabihya alisema kuwa, CCM mkoani humo, imejiandaa kushinda kwa kishindo ambapo alisema kuwa uwezo, nia na makusudio ya kushinda yapo kutokana na chama hicho kuteua wagombea bora na wenye sifa za kuwatumikia wananchi.

"Tumejipanga kushinda kwa kishindo na nia hiyo tunayo na hili limejidhihirisha katika mchakato wetu wa kura za maoni za kuwapata wagombea tumezingatia matakwa ya wananchi kwa kuwapa wagombea wanaowataka wao ni sio vinginevyo," alitamba Mabihya.

Katibu huyo alisema kuwa, viongozi wa vyama vya upinzani wanapaswa kujipanga kikamilifu kupambana na CCM katika kura na sio kususia uchaguzi na kukimbia kwa wananchi na kutoa maneno ya uongo ya kuikashifu serikali kwani huo si busara na uungwana. Alisema kuwa, kwa sasa CCM mpya imejidhihirisha kwa wananchi kwa kusema na kutenda kwa vitendo kile ambacho wananchi wanahitaji hali ambayo imepelekea chama hicho kupendwa na Watanzania wengi. Katika hatua nyingine, Mabihya aliwataka wananchi wa Mkoa wa Kilimanjaro kujitokeza kwa wingi katika mikutano ya kampeni za wagombea wa nafasi za wenyeviti wa vijiji na vitongoji itakayoanza Novemba 17 mwaka huu ili kupata fursa za kusikiliza sera za wagombea.

Alisema kitendo cha wao kujitokeza katika mikutano mbalimbali kitawapa fursa ya kufanya maamuzi ya kuwachagua viongozi bora watakaowaongoza na kuwatumikia katika kipindi cha miaka mitano pamoja na kutatua chagamoto zinazowakabili.




Washindi wa droo ya Maji ya Kilimanjaro kwa mikoa ya Dar es Salaam, Pwani na Morogoro, wakiwa na zawadi zao za Pikipiki, Televisheni na katoni za maji, katika sherehe iliyofanyika jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: SELEMANI MPOCHI**

# Same yajitengenezea wajasiriamali viwanda

**Na Mary Mosha,** SAME

KATIKA kutimiza ndoto za kuifanya Tanzania kufikia uchumi wa kati na wa viwanda ifikapo mwaka 2025, Mkuu wa Wilaya ya Same, Rosemary Senyamule, ameanza kufundisha wajasiriamali ambao wataanzisha miradi ya kiuchumi katika maeneo mbalimbali

Mkuu huyo wa wilaya ametamba kutengeneza mamilionea wanaotokana na sekta ndogo ya ujasiriamali wilayani humo kwa kutoa mafunzo kwa wajasirimali zaidi ya 154.

Mafunzo hayo yaliyodhaminiwa na ofisi ya mkuu wa wilaya hiyo, yatawasaidia wajasiriamali hao kutengeneza bidhaa zaidi 25 ambazo zitanyanya uchumi wa viwanda.

Akizungunza mara baada ya mafunzo hayo, Sinyamule alisema kwa kuhitimu mafunzo hayo wataweza kuwasaidia wananchi wa Wilaya ya Same kujikwamua kiuchumi kwani wataanzisha miradi ya kiuchumi kwenye maeneo mbalimbali.

Alisema, ikiwa wajasiliamali hao watafanikiwa kama ilivyokusudiwa, wanayalenga wastani wa magari 720 yanayopita kwa siku na abiria zaidi ya 10,000 ambao hao wote ni wateja wao , hali hii itakuza vipato vya mmoja mmoja, wilaya na hata taifa kwa ujumla.

Aidha, baadhi ya wajasiliamali hao, Asha Mzava, alisema licha ya serikali kuwapatia mafunzo hayo kwa ajili ya kukuza uchumi wa viwanda lakini pia ni vyema ikaangalia suala la miundombinu.

" Tunaomba serikali ituangalie suala la miundombinu ya barabara hasa za vijijini ili wateja wetu waweze kufika na kupata huduma, pia taasisi za mikopo ziangalie namna ya kutupa mikopo ya kwa mashariti nafuu ili tuweze kukopa na kuendeleza uzalishaji," alisema Mzava.

Ofisa Maendeleo ya Jamii wilayani hapo, Victor Kabuje, aliwataka wajasiriamali hao kuhakikisha wanafanyia kazi mafunzo waliyopata huku akiwaahidi mafunzo mengine. " Endapo mtafanya vizuri tutaandaa mafunzo mengine ikiwa ni pamoja na kutafuta masoko ndani na nje ya wilaya yetu," alisema Kabuje.

Mwezeshaji Said Akubali, aliwataka washiriki hao waliopata mafunzo kujituma na kufika kiwandani kwake kwa ajili ya kujifunza zaidi.

# ama

ALHAMISI NOVEMBA 14, 2019

AFYA NA MAZINGIRA



Ukurasa 14

**Kinamama 'mashoto' wana uwezo ziada**




Ilianzia kule na sasa iko hapa

Ukurasa 19



Ukurasa 18

**Ilikojificha saikolojia afya ya mtoto, urithi baba na mama**





Distributed via ippmedia

## MOJA KWA MOJA MWANZA...

# Mratibu Afya: Mti shamba yaua sana wajawazito, kuiacha ubishi mkubwa

Ukurasa 16



Mwanamke atumiaye mkono wa kushoto. **PICHA: MAKTABA.**

## Kinamama 'mashoto' wana uwezo ziada kunusa

**Na Mwandishi Wetu**

WANASANYANSI wamebaini cha kipekee katika baiolojia ya mwanadamu na hisia za harufu, kwamba kinamama wanatotumia mkono wa kushoto wana cha ziada katika nguvu ya kunusa.

Jarida la kisanyasi liitwalo Journal of Neuron, linasema baadhi ya kinamama ambao hata wakikosa nguvu za mishipa fulani katika ubongo, uwezo wao katika kunusa hauna shaka.

Ugunduzi wa watafiti unaenda mbali, kwamba hilo kamwe halijaonekana kwa wanaume, bali kinamama pekee yao.

Baadhi ya viashiria vilivyotumika kupima uwezo wa kunusa ni kinywaji cha kahawa, maua yenye harufu nzuri na nepi ya mtoto iliyochafuliwa, ama kwa mkojo au kinyesi kikubwa. Namna harufu hiyo inavyosafiri ni kwamba, pua inaponusa, inasafiri hadi katika ubongo ambako kuna mishipa iitwayo 'olfactory bulbs' na ikifanyiwa kazi, ujumbe unarudi tena puani, ndio inapopatikana tendo la kunusa

Kuna watafiti wengine nchini Israel, katika asasi inayoitwa 'Weizmann Institute of Science' wamegundua watu kuwa na uwezo wa kawaida kunusa, hata kama mishipa yao ya fahamu inayowawezesha kunusa (katika ubongo) haifanyi kazi.

Mwanazuoni, Profesa Noam Sobel, anaweka maswali kadhaa ili kuweza kuithibitisha hoja hiyo, kwamba kuna tafiti zingine na marejeo ya kitaaluma yanaeleza hayo.

AFYA

# Nidhamu ya kliniki, kujifungua nyumbani shida kuu Shinyanga

• Mitishamba yapasua vizazi, muuaji mkuu • Hospitali Kahama imeelemewa majirani • Wagonjwa 1000 kwa siku; Tabora, Geita • Upanuzi bn 3.2/-; zahanati mpya kibao



Mwonekano wa mbele wa Hospitali ya Halmashauri ya Mji Kahama.

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

UTUMIAJI mitishamba kwa wajawazito hasa walioko katika maeneo mbali na huduma rasmi, pindi wanaponuia kutibu ugonjwa kama wa minyoo katika kipindi cha ujauzito, unasababisha kupasuka mfuko wa uzazi na kuvuja damu nyingi, inayompoteza maisha mtoto na hata mama yake.

Wengi wamekuwa wakitumia dawa hizo katika dhana ya 'kuongeza uchungu' wakati anapokaribia siku ya kujifungua, lakini kuna madhara nayo kwa mtoto tumboni. Dawa hizo ni kali na inamsababishia mtoto kupoteza maisha kabla ya kuzaliwa.

Mjamzito anapotumia dawa aina yoyote bila ya kuruhusiwa na daktari, ni tendo la kuhatarisha maisha ya mama na mtoto. Kuna dawa mjamzito anaweza kuzitumia katika kipindi chake, hasa pale anapofika kiliniki na kupewa ushauri na uangalizi wa kitalaamu.

> **"Kuna wakati wodi ya watoto wadogo, wanalazimika kulala watatu hadi wanne kwenye kitanda kimoja na wagonjwa wanapopungua, hulala wawili.**

Pia, kuna wengine wamepoteza maisha kutokana na uamuzi wa kujifungua nyumbani na anahudumiwa katika mchakato huo na mtu ambaye sio mtalaamu.

Daima anaishia kuvuja damu nyingi na wakati mwingine mtoto anayezaliwa anakunywa maji ya mama machafu na kuishia kupoteza maisha.

Mwanamke mjamzito anapozalishwa na mtu asiye mtalaamu, huambukizwa ugonjwa kupitia bakteria (Puerperal Sepsis), unaosababishwa na kushikwa na mtu huyo anayemzalisha.

Hata hivyo, ni ugonjwa unaotibika, endapo mama huyo anawahi kufika hospitalini kwa matibabu dhidi ya madhara hayo.

Kutokana na vifo vya wajazito na watoto kuongezeka kila mwaka, serikali kupitia Mpango wa Maendeleo wa Afya (MMAM), imechukua jukumu la kujenga vituo vya afya, zahanati na hospitali nchi nzima, lengo ni kusogezea huduma walipo wananchi, waondokewe na adha ya kutembea umbali mrefu kwenda kujifungua.

### MITI SHAMBA

Caroline Maliseli ni Mratibu wa huduma ya uzazi na mtoto kutoka Halmashauri ya Mji Kahama, anasema matumizi ya dawa za miti shamba kwa kinamama wajawazito wanapotibu ugonjwa wa minyoo husababisha kupasuka kwa mfuko wa uzazi na kuvuja damu nyingi.

Anasema, wajawazito wengi wanapoteza maisha na watoto wao, wanapotumia dawa hizo, kwa lengo la kuongeza uchungu wakati anapokaribia muda wa kujifungua na kusababaisha mfuko wa uzazi kupasuka, mtoto anakunywa maji machafu.

"Dawa za miti shamba ambazo zinatumiwa na baadhi ya kinamama wajawazito kutibu minyoo au kuongeza uchungu ni kali sana na hazifai kuendelea kutumiwa. Zinafanya mfuko wa uzazi kupasuka haraka sana na mtoto kunywa maji machafu tumboni," anaeleza.

Maliseli anasema, kinamama wengi Kahama wanajifungulia majumbani na kuhudumiwa na mtu ambaye si mtalaamu rasmi wa utabibu na baadaye wanapata maambukizi kupitia bakteria yanayosababishwa na kushikwa na kumfunga mtoto kitovu vibaya.

"Mwaka jana kuna mama aliletwa hospitalini akiwa tayari mkono wa mtoto umekatika...ulikatika wakati akijifungua na mtoto kutanguliza mkono ukavutwa na mtu aliyekuwa akimzalisha ambaye hana ujuzi wowote wa kitabibu," anasema Maliseli.

"Tulimfanyia oparesheni na kumtoa mtoto akiwa ameshafia tumboni na mama huyo alipona, japo alipata maambukizi ya bakteria (Puerperal Sepsis) baada ya kushikwa na asiye na utalaamu.

### VIFO KAHAMA MJI

Maliseli anasema hali ya vifo vya kinamama wajazito na watoto, kwa sasa imepungua tangu mwaka 2017, kutoka vifo vya wajawazito 18 hadi wanane mwaka huu, kati ya Januari na Oktoba.

Anarejea takwimu za vifo mwaka 2015, vifo wajawazitio 16; watoto wachanga 312; chini ya mwaka mmoja 461; na chini ya miaka mitano vilikuwa 840, huku vizazi hai vikiwa 11,142.

Pia, anasema mwaka 2016 vifo vya kinamama vilikuwa 23; watoto wachanga 463; wenye umri chini ya mwaka mmoja, 121 na chini ya miaka mitano vilikuwa 298; huku vizazi hai vilikuwa 12,062.

Maliseli anaendelea kusema kuwa, mwaka 2017 vifo vya akinamama vilikuwa 18, watoto wachanga vilikuwa 334, watoto chini ya mwaka mmoja vilikuwa 213 na watoto chini ya miaka mitano vilikuwa 483 na vizazi hai vilikuwa 13,047.

Vilevile anasema, mwaka 2018 vifo vya akinamama vilikuwa 15, watoto wachanga vilikuwa 309, watoto chini ya mwaka mmoja vilikuwa 178 na watoto chini ya miaka mitano vilikuwa 236 na vizazi hai vilikuwa 18,360.

AFYA

# Nidhamu ya kliniki, kujifungua nyumbani shida kuu Shinyanga

Aidha, Maliseli anasema huu kati ya Januari na mwezi uliopita, kulikuwapo vifo vya kinamama wanane; watoto wachanga 281; chini ya mwaka mmoja 35; na watoto chini ya miaka mitano 189; na vizazi hai vilikuwa 16,320.

**WAUME NA KLINIKI**

Maliseli anasema, bado kinababa kwenye familia wana uelewa mdogo kutoshiriki kliniki na wake zao na wanashindwa kuzitambua changamoto au dalili mbaya zinazoweza kutokea wakati wa ujauzito na namna ya kukabiliana nazo.

Analalamika, asilimia kubwa ya wajawazito wanahudhuria kliniki wenyewe bila ya waume zao, hali inayotoa changamoto wakati wa kuwahudumia, hasa wakati wa upimaji wa virusi vya Ukimwi na Ukimwi.

Vilevile, anasema wajawazito kutoka katika Halmashauri za Msalala na Ushetu, wana kawaida ya kuchelewa kuanza kliniki na hufika katika vituo vya afya kujifungua, bila ya hata ya kadi inayoonyesha maendeleo ya mtoto kabla ya kujifungua.

Pia, anasema, vituo vya afya vya Halmashauri za Msalala, Ushetu, Nzega, Tabora Ishishimula, ni kawaida kinamama kuchelewa kuwahudumia wajawazito na wanawaleta katika Hospitali ya Mji wa Kahama wakiwa na hali mbaya.



Distributed via ippmedia

Mwandishi wa gazeti hili akizungumza na Mratibu wa huduma ya uzazi na mtoto kutoka Halmashauri ya Mji wa Kahama, Caroline Maliseli, ofisini kwake. **NA MPIGAPICHA WETU.**

**SHIDA WAHUDUMIAJI**

Maliseli anasema, upungufu wa watoa huduma kwenye wodi ya wajazito na watoto, pia inachangia kuongezeka vifo na anaiomba serikali kuongeza watoa huduma katika eneo hilo.

Anasema, katika Hospitali ya Mji wa Kahama, wajawazito wanaojifungua ni wengi, kila siku kuna watoto 45 hadi 60 na kuwapa wakati mgumu watoa huduma kushindwa kutoa huduma kutekeleza majukumo yao.

Maliseli anasema, ili kutokomeza vifo vya kinamama wajawazito na watoto ni kuacha tabia ya kujifungulia majumbani na kuanza kliniki mapema hasa pale unapojihisi mjauzito na kujifungulia katika vituo vya afya.

Anasema kuna baadhi ya kata za Halmashauri ya Mji Kahama, imekuwa kawaida matukio ya kinamama wajawazito hujifungulia majumbani na kuhatarisha usalama wa maisha yao na mtoto.

Maliseli anazitaja kata hizo ni: Malunga, Nyihogo na Mhungula. Inaelezwa wanafika hospitalini wakiwa hawajapatiwa chanjo na watoto wao, hawana kadi za kliniki, wengine ni siku chache kujifungua.

**MKURUGENZI MJI**

Anderson Msumba ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Kahama, anasema katika kupambana na vifo hivyo, wamejenga vituo viwili vya afya; Iyenze na Mwendakulima na zahanati 13 katika maeneo yaliyo pembezoni mwa mji, lengo ni kuwasogezea huduma wananchi waliko.

> **Tulimfanyia oparesheni na kumtoa mtoto akiwa ameshafia tumboni na mama huyo alipona, japo alipata maambukizi ya bakteria (Puerperal Sepsis) baada ya kushikwa na asiye na utalaamu.**



Jengo la kupumzikia wagonjwa wa nje (OPD) linalojengwa na Halmashauri ya Mji Kahama.

Pia, anasema wanatarajia kujenga zahanati katika kata za Nyasubi, Chapulwa na Ngulu zitakazokuwa na huduma ya mama na mtoto na kuwataka wagonjwa kuanza kupatiwa huduma ngazi ya zahanati na kituo cha afya, kabla ya hawajafika wilayani.

Msumba anasema, Hospitali ya Wilaya ya Ushetu itakapokamilika, itasaidia kupunguza wimbi la wagonjwa wanaotoka katika Halmashauri za Urambo na Kaliua mkoani Tabora, kwani watapatiwa huduma mahali hapo.

Aidha, anafafanua lengo la ujenzi wa vituo vya afya na zahanati ni kuwaondolea adha wajawazito kutembea umbali mrefu kuifuata hospitali ya wilaya na wakati huo huo, inapunguza msongamano wa wagonjwa, ambao kwa siku Hospitali ya Mji Kahama, inahudumia wagonjwa 800 hadi 1000.

**OPD YAELEMEWA**

Msumba anasema, kwa sasa wanajenga jengo la kupumzikia wagonjwa wa nje (OPD) linalogharimu kiasi cha Sh. bilioni 3.2, ni fedha kutoka mapato ya ndani ya halmashauri na inatarajia kukamilka Februari mwakani, kwa kumhudumia mama na mtoto.

Anasema, Hospitali ya Mji wa Kahama inahudumia wagonjwa kutoka Halmashauri za Msalala, Ushetu, Mbogwe, Shinyanga Vijijini, Geita, Nyang'wale, Samuye, Urambo na Kaliua mkoani Tabora na mkoa Geita, hali inayosababisha msongamano mkubwa.

"Mazingira yaliyopo sio mazuri, wagonjwa wanalundikana, hakuna nafasi na endapo mvua ikinyesha wagonjwa wanaosubiria huduma wanaweza kunyeshewa. Hii ndio imetusukuma kujenga jengo jipya la kupumzika wagonjwa wa nje," anasema Msumba

Vilevile Msumba, anafafanua kuna wakati wodi ya watoto wadogo, wanalazimika kulala watatu hadi wanne kwenye kitanda kimoja na wagonjwa wanapopungua, hulala wawili.

Mtazamo mkuu unaosimama ni kwamba, ili kutokomeza vifo vya kinamama na watoto, ni vyema wajawazito kujifungua katika vituo vya kutoa huduma, kuhudhuria kliniki, hasa mtu anapojihisi mjamzito na kuacha kutumia dawa za kienyeji kutibu magonjwa mbalimbali, hasa kwa mjamzito.

*Soma zaidi uk. 16*

AFYA

MOJA KWA MOJA MWANZA...

# Mratibu Afya: Mti shamba yaua sana wajawazito, kuiacha ubishi mkubwa

• Watafuna, kupeana kwa siri wodini • Majani bangi...;chanzo wakunga, bibi
• Sasa? Operesheni upekuzi, kutajana • Elimu yaanzia wodini hadi mazikoni



Sehemu ya Wodi ya Kinamama katika Hospitali ya Rufani Sekou Toure, jijini Mwanza katika picha tofauti. **PICHA: MTANDAO.**

Distributed via ippmedia

**Na Anthony Gervas,** MWANZA

"MIMEA wanayotumia kutengeneza dawa za kuongeza uchungu wajawazito, wanataja kuwa ni mizizi ya bangi na majani yake, mmea wa mgagani pamoja na magome ya miti shamba na wakati mwingine huweka sehemu za siri," anatamka Mratibu wa Huduma za Afya ya Uzazi na Mtoto, Mkoa wa Mwanza, Secilia Mrema.

Ni mazungumzo maalum na Nipashe katika Ofisi za Mganga Mkuu wa Mkoa Mwanza, ilipofahamishwa kwamba dawa za kienyeji ni tatizo linalochangia madhara makubwa kwa wajawazito wakati wa kujifungua hospitalini.

Simulizi hiyo ya undani wenye madhara, Inataja mlolongo wa mambo, ikiwamo uelewa mdogo kuhusu kufahamu wa hatari za dawa hizo, ambao Secilia anadadavua kwa kina kuanzia hali halisi hadi picha kamili iliyokoo mkoani humo.

**MADHARA YAKOJE?**

"Tunapompima mama mjamzito wakati wa kujifungua tunakuta amechanika mfuko wa kizazi, anatokwa damu nyingi na mtoto amefia tumboni, wakati vipimo vinaonyesha hana magonjwa ya aina yeyote yaliyoweza kusababisha madhara hayo,

"Lakini, tunapomkamata na kumhoji, anakiri kutumia dawa za kienyeji ambazo hazina kipimo na kusema wanatumia mizizi na majani ya mmea wa bangi, mmea wa mgagani na magome ya miti shamba,kwa madai zinaongeza uchungu aweze kujifungua haraka," anaeleza hali inayotawala.

> Kwa sasa asilimia 93 ya kinamama wajawazito wanakwenda katika vituo vya kuhudhuria kliniki zao, lakini wanaofuata taratibu hadi mwisho ni asilimia 76.



Robi Samwel akiwa na watoto wanaolelewa katika kituo chake.

Pia, anasema baadhi ya kinamama hao, wamekuwa wakikamatwa na wataalamu wa afya katika vituo vya afya na hospitali wakiwa na dawa hizo, wanaozitumia kwa kificho wakati wanapolazwa wodini kusubirii kujifungua.

"Katika Mkoa wa Mwanza tangu Januari mwaka huu hadi sasa, idadi ya kinamama 139 wamefariki dunia kutokana na sababu za madhara ya dawa hizo wakati wa kujifungua," anasema na kuongeza:

"Kati yao, kinamama 39 wamefariki dunia kwa kutokwa damu nyingi na kinamama 10 wamefariki dunia kutokana na kuchanika mfuko wa kizazi."

Mratibu Secilia anasema, watoto waliofia tumboni wakati wa kujifungua, mama zao ni zaidi ya 500 na magonjwa mengine nayo yanayochangia madhara hayo, akiyataja baadhi yanayohusiana na zinaa, shinikizo la damu, malaria na kisukari.

**WANAOKIRI WODINI**

"Tunapowakamata wodini wakiwa na dawa hizo, wanakiri. Hapohapo tunachukua hatua ya kuwanyang'anya na kuanza kuwaelimisha kufuata taratibu za huduma bora za afya, ikiwamo kuhudhuria kliniki katika vituo vyetu vya afya.

"Wakati mwingine tunapowakamata wodini wamelazwa wakisubiri kujifungua, wanatajana kuwa wanagawiana kwa siri na wenzao ndani ya wodi, huku wakitumia kwa siri kupitia chai. Staili zingine, wengine huziweka sehemu za siri, lengo wanadai zinawahisha uchungu kujifungua haraka," anaeleza.

Secilia anaeleza kwa sasa wamekuwa wakichungana wodini wenyewe na wanapobaini jambo wanatoa taarifa kwa wauguzi, baada ya kupata elimu kuhusiana na madhara husika.

Mratibu huyo anaeleza kwamba, wajawazito hao wanapokamatwa wodini na kuhojiwa walikozipata,huwataja ndugu wa karibu wenye nafasuiza uzazi na ulezi; bibi, shangazi, wakunga wa asili na waganga wa kienyeji, ambao ndio chanzo kikuu.

**MADARASA**

Secilia anasema uchungu wa kutumia dawa za kitaalamu kwa mjamzito wakati wa kujifungua, inapokuwa mimba ya kwanza huchukua muda wa saa 12, lakini inapokuwa mimba ya pili, huchukua muda kuanzia saa sita hadi nane.

Aidha, anaeleza kwamba Idara ya Afya, imeanzisha timu ya wataalamu wa afya kuhakikisha wanatoa elimu kwa kinamama hao, ili waachane na matumizi ya dawa hizo kupitia vyombo vya habari, vikao vya halmashauri na vikao vya kata.

Vilevile, mratibu huyo anasema elimu hiyo inatolewa kupitia mkusanyiko wa msiba baada ya maziko, ikiwa mjamzito amepoteza maisha kutokana na matumizi ya dawa hizo, kwa kuwakusanya wananchi waliopo msibani na kuwaelezea kuhusu madhara hayo.

Elimu nyingine anaitaja kupitishwa kwenye vikao vya kata, vituo vya afya, zahanati, wakunga na waganga wa kienyeji, wakiwataka wafuate taratibu za kutumia dawa rasmi za serikali, kupitia taratibu rasmi kama vile kwenye vituo vya afya.



Mratibu wa Huduma za Afya ya Uzazi na Mtoto, Mkoa wa Mwanza, Secilia Mrema. **PICHA: ANTHONY GERVAS.**

**FAMILIA**

Wanafamilia na ndugu ndiyo wanatajwa zaidi kuhusika na utengenezaji dawa za kienyeji kwa ajili ya kuongeza uchungu kwa mjamzito, lengo ni kwamba asikae muda mrefu wodini kusubiri kujifungua kwa machakato wa kitaalamu.

Secilia anasema, ni kawaida mjamzito anapokuwa katika mimba ya kwanza anajifungua baada ya kuwapo katika uchungu wa saa 12, lakini kwa mimba ya pili anatakiwa uchungu kukaa kuanzia saa sita hadi nane.

Angalizo lake linalochukua sura ya onyo, ni kwamba mjamzito hapaswi kutumia dawa yoyote ambayo hajaandikiwa na daktari na akifanya hivyo tayari amesajiingiza katika hatari ya afya yake.

**KLINIKI JE?**

Mratibu huyo anasema, ni kanuni na sheria kwamba mjamzito anatakiwa kuhudhuria kliniki zote kama alivyoelekezwa katika kituo cha afya kila mwezi, ili kupata huduma iliyo sahihi hadi hatua ya kujifungua.

"Kwa sasa asilimia 93 ya kinamama wajawazito wanakwenda katika vituo vya kuhudhuria kliniki zao, lakini wanaofuata taratibu hadi mwisho ni asilimia 76," anasema.

> Kati yao, kinamama 39 wamefariki dunia kwa kutokwa damu nyingi na kinamama 10 wamefariki dunia kutokana na kuchanika mfuko wa kizazi.

**MWANZA ILIVYO**

Mratibu Secilia, anasema Mkoa wa Mwanza, una jumla ya vituo vya afya 52; kati yake vipo vituo 14 vipya vilivyoanzishwa na serikali kwa ajili ya kutoa huduma za upasuaji kinamama wajawazito wakati wa kujifungua na vingine vinane vya zamani, vinavyoendelea na huduma hiyo.

"Mkoa wa Mwanza tumeanzisha mkakati kabambe wa kufundisha watumishi 20 wa afya, kwa ajili ya kufanya utafiti kuhusu matumizi ya dawa hizo, kujua moja kwa moja asilimia za madhara yake," anasema.

Rai yake ni umma wa wajawazito uache kutumia dawa tofauti na ufuate ushauri wa daktari au mtaalam wa afya kutoka katika vituo vya afya na hospitali, kwa vile hazina kipimo.

***• Alhamisi wiki ijayo, simulizi ya ushuhuda.***

***• Mwandishi anapatikana kwa barua pepe: anthonygervas@yahoo.com na simu(+255) 0682 86 92 44.***

## Vimbunga pasua kichwa usalama mazingira dunia

• Marekani kila siku, hasara shilingi trilioni nyingi



Hali halisi ya madhara ya kimbunga kilichotokea katika pwani ya Beira, nchini Msumbiji. **PICHA: MTANDAO**

**Na Mwandishi Wetu**

VIMBUNGA ni tatizo. Huo kimsingi, ni mfumo wa upepo unaosafiri kwa kasi kubwa majini na hasa kwenye bahari na mara nyingi unapatikana katika ukanda wa kitropiki, ambao hali ya hewa yake inatawaliwa na joto.

Nadhani katika nchi jirani ukanda wa baharini, kama vile taifa la Msumbiji kwamba 'zimeonja'

Ni aina ya upepo unaokimbia kwa kasi ya maili 74 kwa sasa, ambayo ni sawa na kilomita 119 kwa sasa. Wataalamu wameipa jina 'tropical cyclone.'

Watafiti wa kisayansi wana hoja kwamba mabadiliko katika kiwango kilichofika sasa ni kwamba, vimbunga vinakimbia katika kiwango mara tatu, ikilinganishwa na ilivyokuwa miaka 100 iliyopita.

Kuna juhudi kadhaa zimekuwa zikifanyika kukabili vimbunga hivyo, ingawa bado hakujapatikana mafanikio yenye uhakika.

Hadi sasa, vimbunga hivyo vinaingia katika hesabu ya kuwa vyanzo vya asili vyenye uharibifu mkubwa katika jamii' zikitawaliwa na Kimbunga Katrina, kilichotokea mwaka 2005, ambacho zaidi ni nchini Marekani.

Huko kunatajwa kutia hasara Dola za Marekani bilioni 125 (shilingi trilioni 287.5) ambayo ni kiasi cha wastani wa asilimia moja ya Pato la Taifa la nchi hiyo.

Swali kubwa la kitaalamu linalotawala hivi sasa, ni namna gani mtu anapigana dhidi ya vimbunga baina ya eneo moja na lingine, pia usalama wa mali zao.

Katika kukagua athari hizo za vimbunga vya kila siku, watafiti wanasonga mbali kukagua madhara kiuchumi, kwamba haishii katika mali tu, bali hata ardhi inavyoharibiwa.

Kwa kufuatilia uhalisia kupitia vigezo mbalimbali, watafiti wamebaini athari za vimbunga imeogezeka kwa wastani wa asilimia 330, kwa kila muongo mmoja unaopita na chanzo kikuu ni ongezeko la joto

Pia, mtazamo wa watafiti kufafanua uhalisia ulipo ni kwamba mbinu na mitazamo yao katika kupata majibu ya uhalisia huo, bado ni sahihi zaidi katika kupata ukweli ulivyo.


Watafiti Wamarekani waliifuatilia kimbunga mwaka juzi na kuathiri wastani wa watu milioni 1.1 katika makazi ya watu yenye ukubwa wa kilomita za mraba10, 000.

Kimbunga Dorian kilichotokea hivo karibuni huko jimboni Florida, mwezi Septemba ilitia hasara ya kasi kikubwa sana cha pesa.

**Kwa mujibu wa taarifa za mtandao.**

AFYA

# Ilikojificha saikolojia afya ya mtoto, urithi baba na mama



Distributed via ippmedia

Huu ndio urafiki wa utatu; baba, mama na mtoto kila mmoja katika nafasi yake, mlengwa mkuu wa kwanza ni mtoto. **PICHA: MTANDAO.**

**Na Tatu Tambile**

MTOTO ni zao la baba na mama. Baada ya kuzaliwa, mchakato ambao mama ni mhusika mkuu, ni sahihi kumbebesha kwa asilimia zote mama pekee tu?

Ni swali linalozalishwa na mazoea ya baadhi ya kinababa, wenza wao wanapojifungua na kutingwa na malezi ya 'kichanga' wao wanajielekeza 'nje' ya ndoa na wengi wanaangukia katika majibu ya utetezi "mama kahamisha upendo kwa mtoto."

Swali ni kwamba, iwapo mama anahamishia upendo kwa mtoto, je baba anahamishia upendo wapi, ilhali mtoto ni wa pamoja?

Inaenda mbali, kwanini asihamishie upendo wa mtoto wake mpya, ili wakae pamoja na mke kulea familia kwenye shida na raha? Je, si jukumu la baba kumbembeleza au kufurahi na mtoto anapolia au kucheza naye wakati wa kumlisha?

Nikiri, kuna baadhi ya wanaume wanawajibika ipasavyo katika malezi ya watoto, kuanzia wanapokuwa tumboni.

Ni Jukumu la wazazi wote katika malezi ya watoto, lakini kulikoni baadhi ya wanaume kutoa sababu za kuhalalisha 'uchepukaji' na kuitelekeza familia kwa madai 'hawapendwi kama mwanzo' kwa kisa mama kahamishia mapenzi kwa watoto.

> Wanaume wasiwaachie majukumu ya malezi, kinamama pekee yao, badala yake ushirikiano wa wazazi wote unatakiwa.

Mtafiti maarufu wa malezi nchini Poland,Jozef Augustiyn, aliwahi kutoa ufafanzi kwamba: "Baba wengi hufikiri kuwa wao ni wazazi bora, kwa sababu wanachuma fedha kwa ajili ya familia."

Hapo ndipo inapozaa swali jingine, je hilo ndilo jukumu la baba? Ukweli ni kwamba, watoto hawathamini na hawamzingatii baba kulingana na kiasi cha fedha anachochuma, bali sura ya upendo, kutoka kwake. Zawadi inachukua nafasi ya baadaye.

### UPENDO UNAVYOUNDWA

Ushirikiano wa baba na mama katika malezi, ndio unaoleta usawa mbele ya mtoto. Malezi hayahitaji kuegemea upande mmoja. Cha msingi, ni kutambua malezi ni jukumu la wazazi wote.

Malezi ya baba yanawasaidia watoto kuwatambua wazazi. Hatua ya awali kabisa, ambayo mtoto anaimarishwa katika kutambua wanaume, ni watu gani, wana mienendo ipi, wanaonekanaje kupitia ushiriki wa baba kwenye malezi ambaye kwao humuona kama mfano wa kuigwa.

Kupitia baba, mtoto anapata uelewa wa namna ya kulinda, kutoa uhuru, kufanya kazi kwa bidii na ukomo wa mamlaka na wanapata mafunzo kuhusu namna ya kuwa 'baba bora' kwa mtoto wa kike.

Mchango wa baba katika malezi unasaidia kujenga upendo kwa mtoto anapozaliwa. Ni upendo unaoumbwa katika jitihada za malezi na yanamfanya mtoto kumuamini baba yake.

Ni jambo linalomjengea mtoto uwezo kukabiliana na changamoto mbalimbali. Mara nyingi, mtoto mwenye uhusiano mbaya na baba huangukia msongo wa mawazo, japo mama yake yupo.

Mtoto anatawaliwa na hisia za upweke, hasa pale anapowaona wenzake wanahushirikiana na wazazi wao kikamilifu.

Mara nyingi, wanajikuta wakijiingiza kwenye makundi mabaya kitabia; matumizi ya dawa za kulevya, pombe ikiwa sehemu ya 'kutapatapa' kuondoa msongo wa mawazo.

Kuna kanuni ya kinadharia inayotamka "Mtoto hawezi kuzaliwa bila ya baba." Pia mtoto kwenye malezi, hawezi kukamilika bila uwapo wa baba na mama."

Inaelezwa, wazazi kutoshiriki ipasavyo malezi ya watoto, kunachangia kwa kiasi kikubwa kutokea ukatili dhidi ya watoto, mifano hai ikiwapo ya ulawiti na ubakaji. Kwa ujumla, si mwelekeo mzuri.

Takwimu za Jeshi la Polisi za mwaka 2018, zinaonyesha ukatili wa kijinsia kwa watoto umeongezeka kutoka matukio 13, 457 hadi kufikia matukio 14,419.

Hiyo, inaelezwa kuwa sawa na ongezeko la asilimia 6.6, ambayo matukio mengi yana visababishi vya wazazi na walezi, ikiwamo ushiriki mdogo wa kinababa katika malezi, unywaji pombe kupindukia na migogoro katika ndoa.

Kwa kutambua hilo, serikali ilizindua ajenda ya kitaifa, mnamo Juni 16, mwaka huu kwenye Siku ya Mtoto wa Afrika, uliofanyika Katoro mkoani Geita, ikiwa ni mkakati wa serikali kuikumbusha Jamii ya Watanzania, wajibu wa wazazi na walezi kuhusu umuhimu wa malezi bora ya watoto.

Lengo kubwa la ajenda hiyo ni kuhahakikisha wajibu wa malezi chanya unatekelezwa na kila mwanajamii anahusika, zikiwamo taasisi za kidini mna kiserikali, wanahabari, watunga sera na sheria katika ngazi zote za kijamii kwa ujumla.

### WIZARA MAMA

Akizungumza kwenye kongamano na vyombo vya habari, kuhusu ajenda ya kitaifa ya wajibu wa wazazi na walezi katika malezi na matunzo ya familia, Mkurugenzi wa Maendeleo ya Watoto, kutoka Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Mwajuma Magizwa, ana ufafanuzi.

Katika hotuba yake kwa niaba ya waziri mwenye dhamana, anawataka wazazi na walezi kuwa mstari wa mbele kuwalea watoto na kuwapa mwongozo na maadili mema, badala ya kuwaachia wengine jukumu hilo.

Pia, anakumbusha wanaume wasiwaachie majukumu ya malezi, kinamama pekee yao, badala yake ushirikiano wa wazazi wote unatakiwa.

Mkurugenzi Msaidizi wa Watoto (Familia na Elimu ya Malezi),Tausi Mwilima, anaeleza serikali ilianzisha na kuzindua ajenda ya kitaifa wajibu wa wazazi na walezi, katika matunzo ya familia ili kuikumbusha jamii umuhimu wa malezi bora, kwa kuhakikisha wazazi wote wanahusika katika malezi ya watoto.

Serikali ilianzisha ajenda hiyo baada ya kuona changamoto ya ukatili kijinsia, watoto wanaohusika ni wa karibu kwao, hivyo ni ajenda itakayosaidia kuhamasisha jamii wajibu wake katika matunzo na malezi;baba na mama kushirikiana kulea.

Kimsingi, ni msisitizo unaowekwa katika maeneo makuu matano: matunzo, ulinzi, mawasiliano, kujenga familia; na upendo.

Ni maeneo yanayotajwa kufanyiwa kazi kwa watoto na vijana watakuwa salama katika maeneo mbalimbali na kutengeneza kizazi bora na imara, chenye watu wenye maadili na uzalendo kwa taifa.

AFYA

MIAKA 25 CCBRT

# Ilianzia kule na sasa iko hapa

• Yasimama kwa walemavu, kinamama

Na Sabato Kasika

NOVEMBA 8 mwaka huu, Hospitali ya CCBRT, iliadhimisha miaka 25 tangu ilipoanza kutoa huduma za afya nchini, ikiwa imefanikisha lengo lake kwa zaidi ya asilimia 40, kupunguza vifo vya mama na mtoto.

Aidha, hospitali hiyo kuanzia mwaka 2010 ilianza kutoa huduma za afya kwa kushirikiana na baadhi ya hospitali, vituo vya afya na zahanati mkoa Dar es Salaam, ikiwalenga watu maalum.

Watu hao ni wenye ulemavu au walio katika hatari ya kupata ulemavu. Kinachofanyika ni kutambua inaleta matokeo mazuri na muda mrefu, huku tiba na uzazi salama inazuia ulemavu wa maisha.

CCBRT ilianza kutoa huduma za afya katika mifumo ya afya ya uzazi mkoani Dar es Salaam kwa kushirikiana na timu ya afya ya mkoa na manispaa zote tano, pia timu za afya za hospitali mbalimbali.

Mkurugenzi Mtendaji Mkuu wa CCBRT, Dk. Brenda Msangi, anasema wavifikia vituo 23 vya umma, hivyo kuakisi maana halisi ya ubia katika utoaji huduma ya afya.

Anavitaja kuwa ni: Kituo cha Afya Rangi Tatu; Hospitali ya Rufani Temeke; zahanati na' Round Table' na zahanati ya Majimatitu wilayani Temeke. Wilaya Kigamboni, kuna Hospitali ya Vijibweni, Kituo cha Afya Kigamboni na zahanati ya Kimbiji.

Dk. Brenda anasema, upande wa wilaya ya Ilala, wanashirikiana na Hospitali ya Rufani Amana; Hospitali ya Chanika.

Pia, mbali na Hospitali ya Taifa Muhimbili, Dk Brenda anataja Kituo cha Afya Buguruni na zahanati za Kitunda, NBC Tabata na Kiwalani.

Kwa upande wa wilaya ya Kinondoni, anataja Hospitali ya Rufani Mwananyamala; zanahati za Kunduchi, Kawe, Mwenge, Tegeta na Tandale. Mkurugenzi huyo anasema, katika Wilaya ya Ubungo, wanashirikiana na Kituo cha Afya Sinza na Kituo cha Afya Kimara.

### KAZI INAVYOFANYIKA

Brenda anasema, vituo hivyo vina vifaa tiba na maboresho yamefanyika kwenye miundombinu ya utoaji huduma za afya na uwezo wa wafanyakazi kufanya kazi, hivyo kuwezesha huduma salama na zinazofikika kiurahisi kwa kinamama na watoto.

"Mifumo kama ya rufaa imeimarishwa, ili kupunguza msongamano hasa kwenye hospitali kubwa na kwamba vituo vinakusanya takwimu sahihi na zenye ubora kwa kutumia mifumo ya kisasa kama vile mpango wa kutambua changamoto za vifo vya watoto wachanga," anasema.

Dk. Brenda anafafanua hiyo inawasaidia watoa huduma kuelewa sababu za vifo, hivyo wanavizuia visitokee, huku akisisitiza upatikanaji damu safi na salama unazidi kuboreka, kuhakikisha kinamama na watoto wachanga wanahudumiwa kila penye hitaji ya dharura.

Anafafanua kuwa uongozi wa hospitali, husika unashirikishwa na kumiliki mifumo ya kuboresha ubora wa huduma na kwa kushirikiana na hospitali hizo 23, CCBRT huhesabu kufuatilia kila kifo na sababu yake. Anasema, ukaguzi wa vifo ni nyenzo ya thamani katika kuendeleza kujifunza na kushirikishana matendo bora kitabibu, huku akijivunia mafanikio kupungua vifo vya kinamama vitokanavyo na uzazi, Dar es Salaam.

Dk. Brenda anasema ni utaratibu uliosaidia kupunguza vifo vya wajawazito na watoto jijini kwa zaidi ya asilimia 40 katika kipindi cha miaka 25, tangu kuanzishwa kwake nchini.

"Pamoja na mafanikio haya, CCBRT itaendelea kufanya kazi za kuboresha huduma za afya ya uzazi mkoani Dar es Salaam hadi wanawake wote wapate mazingira ya uzazi yaliyo salama, yenye staha na ubora," anasema.

Anasema, sasa waposherehekea miaka 25 ya huduma na kujiandaa kwa safari nyingine ya miaka 25, wanawashukuru watoa huduma wabia hao 23 kwa kuendelea kuwa na hamasa na kujitoa katika huduma bora.



Rais wa Bodi ya Hospitali ya CCBRT, Dk.Wilbrod Slaa, akizungumza na Mkurugenzi Mtendaji Mkuu wa hospitali hiyo, Dk. Brenda Msangi. **PICHA ZOTE NA MPIGAPICHA WETU**

> **Tangu kuanzishwa kwake mwaka 1996 kimeweza kuhudumia watoto wenye ulemavu na familia zao zaidi ya 10,000 na kuwarejeshea matumaini.**




Baadhi ya wananchi wakisubiri huduma katika Hospitali ya CCBRT.

### MALENGO YAJAYO

Meneja Uendeshaji Mradi wa Kujenga Uwezo wa CCBRT, Yohana, Kasawala, anasema, wanajenga Hospitali ya Rufani itakayokuwa na uwezo wa kuhudumiwa kinamama 12,000 kwa mwaka.

"CCBRT na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tumeingia ubia kwa ajili ya ujenzi wa hospitali ya mama na mtoto, ambayo itakuwa hospitali ya rufaa kwa ajili ya kupokea shida ngumu za kinamama wajawazito Mkoa wa Dar es Salaam na kanda yote ya mashariki," anasema Kasawala.

INAENDELEA UK.20

AFYA

# TB, VVU ZILIVYOSIMAMA PABAYA

• Asilimia kubwa vijana wanaumia • Mabinti wengi wasimama pabaya • Kila siku 200 wanaumia kwa VVU



Hafla ya kubadilishana nyaraka za mkataba wa Mpango wa Kukabiliana na Ukimwi na Kifua Kikuu, kati ya shirika la Amref na Hospitali ya Benjamin Mkapa, Dodoma, chini ya ufadhili wa Mfuko wa Dunia. **PICHA: TOVUTI YA WIZARA AFYA.**

**Na Yasmine Protace**

KIMSINGI, si ugonjwa mpya katika jamii nyingi duniani, ikiwamo Watanzania. Lakini, wagonjwa wake wako wapya kila kukicha. Hicho ni kifua kikuu au maarufu TB wa katika tamko la kitaamu 'tuberculosis.'

Ugonjwa huo kitaalamu unaelezwa kusababishwa vimelea visivyoonekana kwa macho viitwavyo 'mycobacterium tuberculosis' vinavyopatikana kwenye hewa inayotolewa na mtu mwenye ugonjwa wa kifua kikuu.

Hivyo, jamii imekuwa ikishauriwa kuchunguza afya zao na inapotokea mtu anakuwa na maambukizi ya TB, ni hatua nzuri ya awali kumuwezesha kupona kwa njia ya matibabu rasmi.

> **Kuugua kifua kikuu, sio kwamba mgonjwa hawezi kupona.**

Uelewa mdogo kwa baadhi ya jamii nao wamekuwa wakihusisha ugonjwa huo kuwa ni tatizo zaidi. Mantiki inayowatawala ni kauli potofu 'maradhi hayo hayatibiki.'

Hapo ndipo inaobuka kundi linalosafiri kuelekea kwenye tiba ya kienyeji, ambako hakuna matokeo mazuri, wenapoteza maisha, kwa sababu ya kukosa tiba sahihi.

Kwa mujibu wa miongozo ya serikali na hata Shirika la Afya Duniani (WHO), dawa za kutibu maradhi hayo zimekuwa zikitolewa bure katika vituo vya afya na baadhi ya wagonjwa wanapatiwa dawa na mahudhurio ya kliniki, inayowezesha kutambuliwa maendeleo ya wagonjwa.

Mbali na kliniki, wagonjwa wanapatiwa ushauri nasaha na kunufaika na hatua za matibabu yanayoendana nayo. "Kuugua kifua kikuu, sio kwamba mgonjwa hawezi kupona," inasema.

**KUTOKA WIZARANI**

Serikali kupitia Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, ina mikakati ya kutokomeza kifua kikuu nchini, ikiwa ni sehemu ya malengo ya pamoja na wanachama wa nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika(SADC), ifikapo mwaka 2030.

Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Dk. Zainab Chaula, anasema: "Ajenda yetu kubwa ya kwanza, ni kujadili namna ya kuutokomeza ugonjwa wa Kifua Kikuu. Tunataka inapofika Mwaka 2030 nchi zote zilizo katika Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika zinatokomeza ugonjwa wa kifua kikuu."

Ni kauli yake alipofungua Mkutano wa Makatibu Wakuu na Wataalamu wa Afya wa SADC, walipojadili ajenda 13 zinazohusu masuala afya, maradhi na maambukizi ya ukimwi na virusi vya ukimwi, ukimwi, malaria, kifua kikuu na usambazaji dawa.

Dk. Chaula anasema Tanzania kupitia Bohari Kuu ya Dawa nchini (MSD), imepewa jukumu la kusambaza dawa, vifaa na vifaa tiba katika nchi wanachama wa SADC, akiitafsiri kwamba:

"Tanzania imepewa heshima kubwa ya kusambaza dawa, vifaa na vifaa tiba, kupitia Bohari kuu ya Dawa katika nchi zilizo kwenye Jumuiya ya Maendeleo ya Afrika Kusini."

Pia, anasema suala la 'Afya ya Mama na Mtoto' na chanjo ni baadhi ya ajenda za kujadiliwa kati ya nchi wanachama wa SADC, ikiwa ni njia ya kuboresha sekta hiyo ya afya.

Mkurugenzi Mtendaji wa Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (Tacaids), Dk. Leonard Maboko, anasema ni takribani watu 200 huambukizwa virusi vya ukimwi kila siku, kati yao watu 80 ni vijana wenye umri kati ya miaka 15 hadi 24. Katika kundi hilo, watu 60 ni vijana wa kike.

"Katika siku moja, watu 200 wanaambukizwa VVU, 80 ni vijana wenye umri wa miaka 15 hadi 24, lakini changamoto zaidi ni kwa vijana wa kike, kwa sababu katika vijana 80 wanaopata maambukizi, vijana wa kike ni 64.

"Hivyo, kama serikali tunahakikisha kwamba tunawawezesha wasichana walio katika mazingira magumu kiuchumi kupata mahitaji yao ya muhimu na waweze kukaa shuleni," anasema Dk. Maboko.

Katika mkutano huo, wenye wajumbe wa nchi 16 za Tanzania imekuwa mwenyeji ikipokea wenyekiti kutoka nchi ya Namibia.

## Miaka 25 ya CCBRT, ilianzia kule na sasa iko hapa

**INATOKA UK.19**

Kasawala anasema, CCBRT inaamini katika ushirikiano miongoni mwa wadau ili kufanikisha lengo la kupunguza vifo vya akina mama na watoto, hivyo juhudi kuhakikisha hilo linafanikiwa zinaendelea.

Anasema, mafanikio katika kuimarisha mfumo wa afya kwa kiasi kikubwa yanatokana na ushirikiano bora na wa kusaidiana kutoka kwenye mamlaka ya mkoa na manispaa. Kasawala anasema, kwa sasa wanajenga hospitali ya rufani itakayopokea wagonjwa wa aina tano, wakiwamo kinamama wanakumbana na changamoto nyingi wakati wa kujifungua.

"Hawa ni wale, ambao hutokwa na damu nyingi wakati wa kujifungua hata kupata kifafa," anasema, huku akiwataja walengwa wengine ni wasichana wanaojifungua katika umri mdogo, walemavu wasiosikia na wasioona, pia wa viungo vingine.

"Unajua katika suala la kujifungua, wale ambao wanapata ujauzito wakiwa na umri mdogo, viungo vyao huwa havijakomaa, hawawezi kujifungua katika njia ya kawaida, wanaweza kupata mtindio wa ubongo na fistula," anasema.

Kasawala, anawataja wenye uwezo kifedha wasiotaka kuhangaika, nao watakaokuwa na sehemu yao kupata huduma hospitalini.

**NENO SERIKALINI**

Waziri wa Afya, Jinsia na Watoto, Ummy Mwalimu, aliyekuwa mgeni rasmi kwa niaba ya Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan, anaipongeza CCBRT kuadhimisha umri huo nchini.

Anakiri kuifahamu vyema na changamoto nyingi tangu ilipoanza na jinsi imekuwa ubia na hospitali mbalimbali nchini kama vile Bombo ua jijini Tanga, Seko Toure Mwanza, Mnazi Mmoja Zanzibar, Kabanga Kigoma, Bagamoyo na Ikwiriri za mkoani Pwani.

Makamu wa Rais anaeleza, ni ishara namna inaonyesha namna imekuwa bega kwa bega na serikali, hivyo anaipongeza kazi yake, ikiwamo kituo chake cha mjini Moshi, kinachofanya kazi nzuri.

"Tangu kuanzishwa kwake mwaka 1996 kimeweza kuhudumia watoto wenye ulemavu na familia zao zaidi ya 10,000 na kuwarejeshea matumaini," anasema waziri Ummy.

Ummy anasema, mradi wa kuwajengea uwezo watumishi kwenye vituo vya afya na zahanati 23 katika manispaa zote tano za Mkoa wa Dar es Salaam umekuwa na mafanikio makubwa.

Anaeleza kwamba mradi, umewekeza kiasi kikubwa cha miundombinu, ukarabati wa wodi za wazazi, ikiwamo ununuzi wa vifaa tiba vyenye thamani ya Sh. bilioni 1.8, vyumba maalum vya watoto njiti, vyoo maalum kwa wenye ulemavu, utambuzi wa mapema wa watoto wenye ulemavu na kinamama wenye fistula ya uzazi.

"Kwenye fistula, wastani wa kinamama 800 kwa mwaka walipata huduma ya upasuaji, na takwimu zinaonyesha kinamama takriban 2000 hadi 3000 hupata fistula ya uzazi nchini," anasema.



## HABARI MBEYA

# Parachichi kuibeba Tanzania kimataifa

**Na Nebart Msokwa**, MBEYA

TAASISI ya Utafiti wa Kilimo (Tari) Kituo cha Uyole jijini Mbeya, imeanza mikakati ya kuimarisha kilimo cha maparachichi ili zao hilo liwe miongoni mwa mazao yanayoitambulisha Tanzania kimataifa.

Akizungumza na waandishi wa habari, Mkurugenzi wa Tari Uyole, Dk. Tulole Bucheyeki, alisema zao hilo lina uwezo wa kustawi mahali popote nchini na hivyo inawezekana kuwa moja ya mazao bora ya nchi.

Alisema watafiti wamegundua aina saba za zao hilo ambazo zinastawi katika maeneo mbalimbali na kwamba endapo mtu anahitaji kulima anashauriwa aina ya mbegu ya kutumia kulingana na mkoa au sehemu alipo na aina ya hali ya hewa ya mahala hapo.

Bucheyeki alisema zao hilo linasoko kubwa duniani kutokana na kuwa na matumizi mengi ikiwamo kutumika, kama chakula na kutumika kwenye viwanda kama mafighafi ya kuzalisha bidhaa mbalimbali.

"Tuna mbegu hapa inaitwa Hasi, ina uwezo wa kuzaa matunda 800 mpaka 1,200 kwa mwaka na kwa ekari moja unaweza ukapanda miche 72 na endapo yakazaa vizuri mkulima ana uwezo wa kuingiza Sh. milioni 17 mpaka Sh. milioni 18 kwa mwaka," alisema Dk. Bucheyeki. Alisema taasisi hiyo imezalisha mbegu nyingi ambazo wakulima wanatakiwa kwenda kuzinunua kwa ajili ya kupanda kwenye maeneo yao.

Alisisitiza kuwa zao hilo mbali na kuwa la kibiashara, lakini linatumika kama chakula ambacho kinaweza kikasaidia kupambana na magonjwa yakiwamo ya udumavu kwa watoto.

Kwa Mkoa wa Mbeya zao hilo linastawi zaidi katika Wilaya za Rungwe na Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya ambako kuna hali bora ya hewa ambako mbegu ya Hasi inastawi vizuri.



Wanachama wa mtandao wa wajasiriamali wadogo wa Naza Group, wakiwa wamekusanyika kwenye duka la mmoja wa wanachama wa mtandao, Franciscar Leonald, katika eneo la Kabwe, jijini Mbeya hivi karibuni, kwa lengo la kumpongeza kwa kuanzisha biashara, ambapo walimpongeza kwa kununua bidhaa anazouza. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Washauri kutumia mitandao kujijenga

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WATANZANIA wameshauriwa kutumia mitandao ya kijamii kwa ajili ya maendeleo ikiwa ni pamoja na kufanya biashara na badala ya kuandika matusi na kusambaza vitu ambavyo havina tija kwao na kwa taifa.

Ushauri huo ulitolewa juzi na wajasiriamali wadogo jijini Mbeya ambao ni wanachama wa mtandao wa Naza Group wakati walipokuwa wanampongeza mwenzao Francisca Leonard kwa kuanzisha biashara.

Walisema mitandao ya kijamii ina faida kubwa endapo itatumika vizuri na kwamba inasaidia haichukui muda mwingi na hivyo kuwafaa hata waajiriwa kuanzisha biashara na kuziendesha bila kuingilia muda wa waajiri wao.

Mwanzilishi wa mtandao huo, Nazarena Myenzi, alisema ni mwajiriwa lakini anautumia muda wake wa ziada kufanya biashara kwa kuzitangaza kupitia kwenye mtandao huo kwa ajili ya kujiongezea kipato.

Alisema awali alianza na watu 50 lakini mpaka sasa mtandao huo umetimiza miaka miwili ukiwa na wanachama 500 wakiwamo watumishi wa umma ambao pia ni wajasiriamali na wanauza bidhaa tofauti

Alisema awali alikuwa anautumia mtandao huo kutangaza bidhaa zake pekee lakini baadaye akaamua kuwashawishi na wenzake kuanzisha biashara na wakaitikia.

"Tunautumia huu mtandao kutangaza bidhaa, kuhamasishana na kufarijiana pamoja na kutiana moyo katika biashara, lakini tunawasaidia wanachama kuimarisha biashara zao hasa wachanga ili na wao wainuke," alisema Myenzi.

Alisema walibaini kuwa asilimia 70 ya wajasiriamali biashara zao zinakufa baada ya mwaka mmoja wa kuanzishwa kutokana na kutokuwa na mtandao wa wateja na kwamba ndiyo maana waliamua kuanzisha utaratibu wa kuinuana.

Mwanachama Janeth Mgeni alisema mara nyingi watu wanaitumia mitandao kama sehemu ya kupotezea muda na kuongea vitu ambavyo havina manufaa na kuwashauri kubadili fikra kwa kuitumia mitandao hiyo kibiashara.

Alisema vijana ndilo kundi kubwa ambalo linatumia zaidi mitandao na ndiyo wanaoweza kufanya vizuri endapo litatumia vizuri mitandao hiyo.

Kwa upande wake Francisca ambaye alikuwa anapongezwa kwa mafanikio alisema mtandao wa Naza Group umekuza biashara yake huku akiwasisitiza vijana kuacha kuitumia vibaya mitandao.

Alisema mbali na kwamba watu wengi hawaitumii vizuri mitandao, lakini wanajikuta wakikumbana na mkono wa sheria hasa baada ya serikali kutunga sheria ya makosa ya mtandaoni, inayowabana wasio na matumizi bora.

# 120 waokolewa kwenye uzururaji

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

VIJANA takribani 120 mkoani Mbeya, wameunganishwa katika vikundi vya ujasiriamali na kuondolewa kwenye maisha ya uzururaji.

Shirika lisilo la kiserikali la Struggle for Helping Others (Shop), lenye makao yake jijini Mbeya ndilo lililowaunganisha vijana hao waliokuwa wazururaji, walevi na vibaka.

Waliletwa pamoja na mradi wa muungano wa vijana kupitia vikundi katika kujiletea maendeleo.

Aidha, shirika hilo limewapatia elimu ya kujitambua vijana wengine 5,000 wa kata sita za jiji la Mbeya kwa njia tofauti ikiwamo matamasha, bonanza, midahalo na kwa njia ya redio ili wajitambue na kujiunga katika vikundi vya uzalishaji.

Hayo yalisemwa juzi na Katibu wa Shop, Olaisi Ole Seenga, wakati wa mkutano kati ya vijana hao, wadau mbalimbali waliofanikiwa kiuchumi pamoja na taasisi za kifedha.

Alisema mradi huo unatekelezwa katika kata sita za Jiji la Mbeya ambazo ni Iyela, Isyesye, Ilemi, Ilomba, Maanga na Ruanda na kwamba vijana hao wameungana katika vikundi sita ambavyo sita vimeshasajiliwa.

"Hawa vijana tumewafundisha mambo mbalimbali ikiwamo uchambuzi wa sera ya maendeleo ya vijana ya mwaka 2007, kwa sasa baadhi ambao walikuwa hawaaminiki katika jamii wanaaminika na wanashirikishwa kwenye miradi ya maendeleo," alisema Ole Seenga.

Aliongeza kuwa baadhi ya vijana hao wameanzisha miradi yao ambayo inawaingizia kipato na kwamba inasaidia kuondoa utegemezi miongoni mwa vijana hao. Mwenyekiti wa vijana hao, Boaz Mwasitu, alisema lengo lao ni kuona vijana wote ndani ya Jiji la Mbeya wanajiunga kwenye vikundi na kuwa na miradi ya kujiingizia kipato.

Alieleza kuwa wanakabiliwa na changamoto ya upatikanaji wa maeneo ya kuanzisha miradi yao kwa maelezo kuwa Jiji la Mbeya halina sehemu zilizotengwa za kutosha kwa ajili ya uwekezaji.

Mwasiti alisema baadhi ya vijana hao wanamiliki vitega uchumi vyao zikiwamo pikipiki za abiria (bodaboda) biashara ndogondogo huku wakijiandaa kuanzisha mradi huo wa pamoja.

"Tunafanya jitihada za kuiomba serikali itupatie eneo kwenye viwanja vya maonyesho ya wakulima Nanenane, ili kurahisisha namna ya kuhudumia mradi wetu, tuna maono mazuri lakini yanakwamishwa na changamoto mbalimbali ikiwamo ufinyu wa bajeti," alisema Mwasitu.

Akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Ofisa Tawala wa Wilaya hiyo, Hamimu Mwambelile, alilipongeza shirika la Shop kwa kubuni mradi huo ambao umesaidia kuwafanya vijana wajitambue na kuanza kuwa wabunifu.

Aliuomba uongozi wa shirika hilo kupanua mradi huo na kuzifikia kata zote 36 za jiji la Mbeya na kisha kuanza kuutekeleza hata katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya. Aliwataka vijana kuchangamkia fursa mbalimbali zinazotolewa na serikali ili wajikwamue kiuchumi ikiwemo kuchangamkia mikopo ya asilimia 10 kwa ajili ya vijana, wanawake na watu wenye ulemavu inayotolewa na halmashauri.



# Tume ya Haki za Binadamu yawaita wenye malalamiko

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

WANANCHI wametakiwa kutoa malalamiko yao kwenye ofisi za Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora baada ya Rais John Magufuli kuteua mwenyekiti mpya wa bodi pamoja na makamishna wapya hivi karibuni.

Kauli hiyo ilitolewa na Mwenyekiti wa Bodi ya Tume hiyo, Jaji mstaafu Mathew Mwaimu, alipokuwa akizungumza na kutambulisha bodi kwa wafanyakazi wa tume hiyo jijini hapa juzi.

Jaji Mwaimu alisema wananchi waendelee kupeleka malalamiko yao kwenye ofisi za tume hiyo ili yaweze kushughulikiwa baaada ya tume hiyo kukaa miaka miwili bila kuundwa.

"Ni kweli ofisi zetu zilikuwapo na wafanyakazi walikuwapo, lakini kuna mambo yanayohitaji maamuzi ya Tume, hivyo uwapo wake sasa utayashughulikia," alisema.

Alisema bodi hiyo iliteuliwa na Rais John Magufuli Novemba 4, mwaka huu na wameanza kazi rasmi baada ya kuapishwa, hivyo wananchi wategemee huduma nzuri kwao kwa kushirikiana na wafanyakazi wa tume hiyo.

Aliongeza kuwa kutokana na kutokuwapo kwa tume hiyo kwa muda wa miaka miwili kuna baadhi ya maamuzi yaliyokwama yalihitaji kikao cha bodi, hivyo uwapo wake utawezesha vikao hivyo kufanyika haraka.

Mwenyekiti huyo alisema jukumu kubwa la tume hiyo ni kulinda na kukuza haki za binadamu pamoja na kuangalia hali ya utwala bora hapa nchini.

Aliwajulisha wananchi kuwa tume hiyo inafanyakazi ya kushughulikia malalamiko kwa mujibu wa sheria, taratibu na kanuni na tume hiyo sio mwisho wa maamuzi yakishindikana yanapelekwa mbele zaidi.

Pia alimtambulisha makamu mwenyekiti wake kuwa ni Mohamed Khamis Hamadi na makamishna ni Khatibu Mwinyi Mwinyichande.

Aliwataja makamishna wengine wa bodi hiyo ni Amina Twalib Ally, Thomas Masanja, Nyanda Shuli na Fatuma Rashidi Khalifan.

Katibu wa Tume hiyo, Fatuma Muya, alisema ofisi hiyo ina matawi katika mikoa ya Dar es Salaam, Pemba, Unguja, Lindi, Mwanza na Makao Makao Makuu Dodoma.

Muya alisema ofisi hiyo ina rasilimali ya wafanyakazi waliopo kwenye ofisi hizo wapatao 143 na aliahidi kushirikiana na tume hiyo katika kuwahudumia wananchi.

Alibainisha kuwa malengo ya ofisi ni kuwa na jengo kubwa ambalo litawawezesha wafanyakazi wote kuhamia makao makuu Dodoma na kwa sasa wataendelea kuzitumia ofisi zote za Dodoma na Dar es Salaam.


Distributed via ippmedia

Mwenyekiti wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Jaji mstaafu Mathew Mwaimu (wa pili kushoto), akizungumza na wafanyakazi pamoja na Makamishna wa Tume hiyo, jijini Dodoma juzi. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Wanawake, vijana, wenye ulemavu watakiwa kuingia kwenye uongozi

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WANAWAKE, vijana na watu wenye ulemavu, wametakiwa kuona kwamba ni wakati sasa wa wao kushika nafasi mbalimbali za uongozi, kwa kuwa wao ni sehemu muhimu ya kuleta mabadiliko chanya ndani ya jamii na taifa kwa ujumla.

Hayo yalibainishwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa na Mbunge wa Bukoba Vijijini, Jasson Rweikiza, wakati akizindua kampeni ya kitaifa ya kuhamasisha wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kuelekea katika uchaguzi wa Serikali za Mitaa unaotarajiwa kufanyika Novemba 24, mwaka huu.

Kampeni hizo zitakazoendeshwa na Asasi ya Ushiriki Tanzania ambayo ni muungano wa asasi za kiraia 23, lengo ni kuhamasisha na kuinua uelewa wa wananchi juu ya masuala mbalimbali kuelekea katika chaguzi mbalimbali zinazotarajia kufanyika hapa nchini. Rweikiza alisema makundi ya wanawake, vijana na walemavu yamekuwa na ushiriki mdogo katika masuala ya uchaguzi, ambapo wengi wao wamekuwa hawana uelewa wa kutosha juu ya kushiriki katika kuchagua au kuomba kuchaguliwa.

"Ni matumaini yangu kuwa kampeni hii itasaidia kuongeza uelewa kwa makundi haya ili kuongeza namba ya ushiriki wao katika chaguzi mbalimbali," alisisitiza Rweikiza.

Aliongeza: "Vijana ni kundi kubwa ndani ya jamii, hivyo kushiriki vizuri katika mchakato wa uchaguzi kutasababisha kupata viongozi watakaojali maslahi yao."

Akizungumzia ushiriki wa wanawake katika ngazi ya uamuzi kupitia ajenda ya 50 kwa 50, Rweikiza, alisema Tanzania imepiga hatua kubwa ukilinganisha na baadhi ya mataifa jirani yanayoizunguka.

Mwenyekiti wa mtandao wa Ushiriki Tanzania, Israel Ilunde, alisema kampeni hizo zitajikita katika mambo muhimu ya kujenga jamii kuwa na uelewa wa kutosha katika ushiriki wao katika masuala ya uchaguzi.

Aliyataja baadhi ya mambo hayo ni kuhamasisha na kuinua ushiriki wa wanawake, vijana na walemavu katika kujitokeza kuomba nafasi katika ngazi za uamuzi ili nao washiriki kikamilifu katika kuzungumzia masuala yanayowahusu.

Alisema jambo lingine ni kushawishi uboreshaji wa utendaji kazi wa vyombo vya ulinzi katika chaguzi mbalimbali, pamoja na kushawishi serikali kuona umuhimu wa kuziwezesha tume za uchaguzi za NEC na ZEC kuwa na ofisi hadi ngazi za wilaya.

Kaimu Mkurugenzi kitengo cha huduma kwa watu wenye ulemavu kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu, Philbert Kawemama, alizitaka asasi hizi za kiraia kuhakikisha kuwa zinaingiza suala la walemavu katika programu na bajeti zao ili kuleta ufanisi.

Mkurugenzi wa Kituo cha Amani, Haki na Msaada wa Kisheria (PLAJC), Jaluo Kalede, alisema kampeni hizo zinalenga kuwaleta viongozi wa serikali, wadau mbalimbali pamoja na mashirika yasiyo ya kiserikali kuwa na mshikamano kuelekea zoezi la kupiga kura ili kuendelea kudumisha amani.

# Bunge laombwa uwapo wa azaki

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

MUUNGANIKO wa mashirika yasiyo ya kiserikali (TANGO), umeliomba Bunge kuhakikisha sheria zinazokinzana na uwapo wa uhai wa azaki ikiwamo ukuaji wao kama sekta ya kiraia, zinarekebishwa ili zifanye kazi kwa uhuru.

Hayo yalibainishwa na Mkurugenzi Mtendaji wa TANGO, Ngunga Tepani, wakati wa kikao cha pili cha mwaka kwa wenyeviti na makatibu wa kamati za kudumu za Bunge, kilichoandaliwa na shirika hilo jijini hapa.

Tepani alisema baada ya mjadala huo, kuna haja ya kupitia kwa pamoja ili kutengeneza mikakati ya kufanya kazi pamoja kimfumo unaotokana kwa lengo la kutekeleza mambo yaliyoazimiwa.

"Baada ya mjadala huu kuna haja ya kukutana pamoja ili kutengeneza namna ya kushirikiana katika utendaji wa kazi tunazofanya katika jamii," alisema Tepani.

Alisema lengo ni kutekeleza majukumu ya wananchi hivyo hakuna sababu ya kupingana kinachotakiwa ni kukaa nchini na kujadiliana kuona namna gani serikali na asasi za kiraia zinachangia maendeleo katika taifa.

Alifafanua zaidi kuwa kuwapo kwa utaratibu wa kutambua kumbukumbuku za mpango kazi na kuongeza kuwa kukiwapo na utaratibu huo, TANGO wanaamini watapiga hatua katika kutatua changamoto zilizopo sehemu mbalimbali nchini.

Mbali na hilo, TANGO imeomba miswada yote iandike kwa lugha ya Kiswahili ili watu wengi waweze kuchangia na kutoa maoni yao juu ya nini kifanyike.

"Kwa miswada mipya hata mabadiliko ya sheria yanayofanywa muda utolewe wa kutosha ili taifa lipate sheria bora ambayo itawasaidia kuleta maendeleo," alisema Tepani.

Alisema wanaliomba Bunge liwaunge mkono kama sekta ya kiraia ili kuwasaidia upatikanaji wa urahisi wa taarifa ambazo zinawasaidia utendaji kazi wao katika maeneo mbalimbali nchini.

Mbunge wa Chemba, Juma Nkamia, alisema asasi za kiraia zinapaswa kushirikiana na wabunge katika majimbo yao ili kuhakikisha wanafanikisha kile walichokusudia kwenda kufanya katika jimbo husika.

Alisema baada ya mjadala huo, wana imani kila asasi itakwenda kutekeleza majukumu yao kiufanisi kwa kushirikiana na wabunge.



# Lipumba awaita waliokimbia CUF

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MWENYEKITI wa Chama cha Wananchi (CUF), Prof. Ibrahim Lipumba, amewataka wanachama wa chama hicho waliokikimbia chama hicho na kujiunga na vyama vingine, warudi kwa kuwa kina misingi madhubuti kidemokrasia.

Aliyasema hayo baada ya kukabidhi kadi zaidi ya 80 kwa wanachama wapya waliojiunga na chama hicho katika Tawi la CUF Kilimahewa wilayani Magharibi 'A' Unguja.

Alisema CUF ya sasa itaendelea kusimamia sera zake za kuundwa kwa chama hicho kwa kusimamia haki sawa kwa wote, ikiwamo ya vijana kupata ajira.

Aliwataka wanachama hao kutofuata mkumbo wa mtu yeyote ambaye amekihama chama hicho.

"Usiwe kwenye chama kwa kuwa Lipumba yumo kwenye chama, baki kwenye chama kwa kufuata misingi iliyokuwa bora na demokrasia iliyokuwa imara na kuacha kupumbazika kwa baadhi ya viongozi wenye kutaka kubaki katika chama na kufuata uamuzi wao tu," alisema.

Prof. Lipumba alidai CUF bado ina wanachama wengi, hivyo waliohama na kwenda kujiunga na vyama vingine, wanapaswa kurudi ili kuendelee kutengeneza ushindi wa chama katika uchaguzi mkuu ujao.

Mtaalamu huyo wa uchumi pia aliwataka viongozi wa chama hicho kuendelea kukipigania ili matawi yaliyopokwa yarudi katika mikono yao.

Prof. Lipumba alisema siasa za Tanzania na Zanzibar kwa sasa zipo vizuri na zinastahiki kuungwa mkono licha ya kuwapo kwa vikwazo ambavyo alidai vinatatulika bila kuathiri taifa.

Aliwataka vijana wa chama hicho kutokuwa waoga, akidai wengi wao sasa wanaogopa kuzungumzia ilhali ni haki yao ya kikatiba.

Alisema malengo ya kuanzishwa kwa CUF ni pamoja na kujenga uchumi unaotoa ajira kwa vijana wote na kutoa elimu kwa kila mtu aliyefikia umri wa kupata elimu.

Naibu Katibu Mkuu wa CUF, Faki Suleiman Khatib, aliwataka vijana wa chama hicho kushirikiana kwa pamoja na viongozi wao ili kuleta maendeleo katika chama.



Mafundi wakikarabati sehemu ya kivuko cha waenda kwa miguu katika Barabara ya Morogoro, eneo la Kimara Bucha, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOHN BADI**

Distributed via ippmedia

# Wapata jibu gharama ujenzi taasisi za umma

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar ina mpango wa kuanzisha shirika au kampuni ya ujenzi itakayovishirikisha vikosi vyake vya ulinzi ili kupunguza gharama za ujenzi wa majengo ya taasisi za umma.

Imesema utaratibu wa kutumia kampuni na washauri elekezi wa nje ya nchi katika kusimamia majengo ya taasisi za serikali unapaswa kuepukwa kwa kuwa unasababisha kutumia gharama kubwa.

Akizungumza baada ya kumaliza ziara yake ya kukagua miradi ya maendeleo Mkoa wa Kaskazini Unguja, Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Ali Iddi, alisema upo ushahidi wa wazi unaoshuhudiwa na serikali na watendaji wa taasisi za umma jinsi vikosi vya ulinzi vya serikali vinavyowajibika vyema wakati vinapopewa tenda za ujenzi wa majengo ya taasisi mbalimbali.

Alisema serikali inaona sasa ni wakati mwafaka nguvu zao zikaunganishwa ili kuleta tija na faida zaidi.

Balozi Iddi alisema wahandisi wa vikosi hivyo wanastahili kupongezwa kwa uzalendo wao uliowafanya kuaminika na kupewa kazi za ujenzi.

Alisema serikali iliamua kujenga nyumba za kudumu badala ya kuwapa fedha wananchi kama fidia ambazo hatima yake zingeishia katika matumizi mengine ya kawaida.

Mkuu wa Mradi wa Ujenzi wa Nyumba za Wananchi wa Dundua, Mkoa wa Kaskazini Unguja, Hawa Natepe, alisema mradi huo unahusisha nyumba 31 zinazosimamiwa na Mamlaka ya Udhibiti na Usimamizi wa Mafuta (Zura).

Hawa alisema nyumba hizo zinajengwa kwa ushirikiano kati ya Jeshi la Magereza na Kikosi cha Kuzuia Magendo (KMKM). Ufyatuaji wa matofali kwa ajili ya nyumba hizo, ulifanywa na Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU).

Miradi mingine ambayo imetembelewa na Balozi Iddi ni pamoja na wa ujenzi wa gati ya mafuta na gesi huko Dundua na ujenzi wa tangi la kuhifadhia maji safi na salama katika Kijiji cha Kitope.

# Wanafunzi chekechea kufundishwa kidigitali

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

NAIBU Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Simai Muhammed Said, amesema serikali inakusudia kuingiza teknolojia ya kidigitali katika mitaala ya elimu ya maandalizi na msingi ili wanafunzi wajifunze matumizi ya teknolojia hiyo.

Akifungua kongamano la matumizi ya teknolojia ya kidigitali mjini Unguja, Said alisema wizara ina wajibu wa kuwaandaa wanafunzi kuanzia ngazi ya awali kufahamu matumizi hayo.

Alisema ili kutekeleza azma yake hiyo, wizara imeandaa sera ya matumizi ya Tehama katika elimu, itakayokuwa mwongozo na dira ya kuendeleza matumizi yake. Alisema wizara kwa kushirikiana na washirika mbalimbali wa maendeleo, imechukua hatua ya kuongeza matumizi ya Tehama kama nyenzo ya kufundisha na kujifunza.

Naibu waziri huyo alisema wizara kwa sasa inajenga vituo vya ubunifu vya matumizi ya teknolojia katika kufundisha masomo ya sayansi kwenye shule 22 za sekondari kwa Unguja na Pemba ili kuimarisha na kuongeza ubora wa ufundishaji wa masomo hayo na kuongeza vituo vyengine 20.

Alisema mageuzi hayo ya kielimu yanahitaji kuimarisha miundombinu, ikiwamo ya shule na kupata vifaa sambamba na kutoa mafunzo kwa walimu katika ngazi hizo ili wawe na ufahamu wa matumizi ya teknolojia hiyo.

Alisema hatua za maendeleo zilizofikiwa katika nchi mbalimbali, zilitokana na kukua kwa teknolojia hasa katika kurahisisha mawasiliano baina ya watu.

Kwa kutambua hilo, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ilianzisha huduma mbalimbali zikiwamo za kifedha na kijamii kwa kutumia mitandao, akitolea mfano kulipia umeme kwa njia ya mtandao.

Mkurugenzi wa Idara ya Teknolojia na Mawasiliano wa wizara hiyo, Omar Said Ali, alisema kupitishwa rasmi kwa sera ya Tehama ya mwaka 2019, kumeipa nguvu wizara kuendelea na mkakati wa kukuza matumizi yake ili kuanzisha miradi itakayokuza ubunifu na fursa za ajira ndani na nje ya nchi.

Kongamano hilo lilihudhuriwa na wakurugenzi na maofisa kutoka serikalini na taasisi binafsi, viongozi wa kampuni za huduma za mtandao, wahadhiri wa vyuo vikuu vya Zanzibar, walimu na wanafunzi.

# Miradi 13 ya kipaumbele yatinga kwa wawekezaji

**Na Mwandishi Maalum**

TANZANIA imewasilisha miradi 13 ya kipaumbele kwa wawekezaji wa kimkakati wanaoshiriki kongamano la Jukwaa la Uwekezaji Mjini Johannesburg, Afrika Kusini.

Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango, aliyemwakilisha Rais John Magufuli, kwenye jukwaa hilo, alisema mradi wa ujenzi wa kiwanda cha kutengeneza dawa mchanganyiko kitakachogharimu zaidi ya Dola za Marekani milioni 408 umewavutia wawekezaji wengi.

Aliwataja wawekezaji waliovutiwa na mradi wa ujenzi wa kiwanda hicho kitakachojengwa Kibaha mkoani Pwani, kitakachokuwa na uwezo wa kuzalisha zaidi ya aina 230 za dawa kwamba wanatoka Korea, Uturuki, taasisi za fedha za kimataifa na kwamba hadi kufika mapema mwakani (2020) mwekezaji mmoja au zaidi watakuwa wamepatikana kwa ajili ya kuanza kujenga mradi huo.

"Pamoja na kupunguza tatizo la uhaba wa dawa na dawa bandia zinazoingizwa nchini, kiwanda hiki pia kitazalisha ajira kwa Watanzania," alisema Dk. Mpango.

Dk. Mpango alisema serikali inatenga zaidi ya Sh. bilioni 230 kwenye bajeti kila mwaka kwa ajili ya kununua dawa, huku mahitaji halisi ya dawa nchini ni takriban Sh. trilioni 1.4 ndio maana mkazo umewekwa kwenye ujenzi wa kiwanda hicho kitakachotatua changamoto za upatikanaji wa dawa nchini.

Alifafanua kuwa miradi mingine 12 iliyowasilishwa mbele ya wawekezaji hao iko katika hatua za maandalizi na iko katika sekta za nishati ya umeme unaotumia nguvu ya maji, viwanda vya kuchakata pamba ili kuiongezea thamani na hatimaye kuzalisha nguo, ambavyo vinaendana na dhamira ya serikali ya ujenzi wa uchumi wa viwanda.

Meneja Miradi kutoka Bohari ya Dawa ya Taifa, Mhandisi Fredrick Pondamali, alieleza kuwa usanifu wa mradi huo wa kiwanda cha kuzalisha dawa mchanganyiko umekamilika pamoja na viwanda vingine viwili zaidi vinavyotafutiwa wawekezaji.

Alisema kuwa mradi wa kiwanda cha kuzalisha dawa ulichaguliwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika kwa lengo la kuupeleka mbele ya wawekezaji ili uweze kupata fedha kutokana na umuhimu wake kwa Tanzania na nchi jirani.

Jukwaa hilo la Uwekezaji Afrika linalofanyika kwa mwaka wa pili sasa limeandaliwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika AfDB kwa kushirikiana na wadau wake mbalimbali, ambapo mwaka huu limevuta wawekezaji wa kimkakati zaidi ya 4,000 kutoka kila pembe ya dunia ikiwa na lengo la kuongeza uwekezaji kwenye ujenzi wa miundombinu ili kuchochea kasi ya mabadiliko ya kiuchumi katika nchi za Bara la Afrika.




Mwenyekiti Mtendaji wa Motisun Group, Subhash M. Patel (kushoto), akikabidhiwa zawadi na Mkuu wa Kitengo cha Mauzo na Masoko wa East Africa Television, Roy Ronald, baada ya kufanyiwa mahojiano na vituo hivyo East Africa TV/Radio, jijini Dar es Salaam, ambavyo vinaendesha kampeni ya 'Kibiashara Zaidi' ikiwa na lengo la kuchochea ukuaji wa shughuli za kibiashara nchini. **PICHA: EATV/ RADIO**

# Madiwani waikataa kampuni ya umeme

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

BARAZA la Madiwani la Halmashauri ya Ushetu wilayani Kahama, limemtaka Meneja wa Shirika la Umeme Tanzania (Tanesco) kuiondoa kampuni ya Angelique International Co L.t.d inayojihusisha na kupeleka umeme kwenye vijiji 54 vya halmashauri hiyo.

Kampuni hiyo ilitakiwa kupeleka umeme kwenye vijiji hiyo tangu mwaka 2017, lakini mpaka sasa limeupeleka kwenye vijiji 14 na kusababisha baadhi ya wawekezaji kushindwa kwenda kuwekeza.

Kauli hiyo ilitolewa na madiwani katika kikao cha kawaida, ambapo walisema wawekezaji wameshindwa kwenda kuwekeza katika halmashauri kutokana na kukosekana kwa umeme wa uhakika.

Diwani wa Nyankende, Doa Limbu, alisema, mkandarasi wa kampuni hiyo alifunga mkataba wa kupeleka umeme vijiji 54 Septemba 10, mwaka 2017 na kuwahakikishia madiwani kuwa ifikapo mwaka 2018 vijijiji vyote 54 vitapata umeme, ahadi ambayo hajatekeleza.

Naye Paulo Sai Diwani wa Kisuke, alisema, serikali imepiga marufuku makandarasi kuwauzia wananchi nguzo, lakini mkandarasi wa kampuni hiyo amekuwa akiwauzia wananchi nguzo kwa Sh. 200,000.

Pia alisema, wananchi wamekuwa wakitozwa Sh. 10,000 kwa ajili ya kufungiwa mita za umeme, na kuongeza kuwa imekuwa ikisababisha baadhi ya wananchi wenye uwezo kushindwa kufungua viwanda vya usindikaji wa matundu na nafaka kwa kuwa na michango mingi badala ya ile ya 27,000 iliyoko kisheria.

Diwani wa Kinamapula Sharifu Samuel alisema, wananchi wamefikia hatua ya kutishia kuharibu miundombinu ya umeme hiyo kutokana na umeme huo kutowasaidia. Akijibu malalamiko hayo Meneja Masoko wa Tanesco makao makuu, Mussa Chowo, alisema mkandarasi yuko nje ya muda wa utekelezaji wa mradi huo, na ni kwa sababu ya changamoto ya baadhi ya maeneo kuwa na mvua nyingi na magari yaliyobeba nguzo za umeme kushindwa kufika kwa kuhofia kutitia au kuzama.

Hata hivyo, alisema kama mkandarasi anawatoza wananchi kiasi kikubwa zaidi ya Sh. 27,000, ni vyema wakamripoti kwenye vyombo vya sheria.

## Msaada wa Japan kuwapa fursa wajawazito

**Na Gurian Adolf,** KALAMBO

SERIKALI ya Japan imetoa msaada wa vifaa vya upasuaji wajawazito watakaohitaji huduma hiyo vyenye thamani ya Sh. milioni 139 katika wilaya za Kalambo na Nkasi mkoani Rukwa.

Mashine hizo zilikabidhiwa jana katika Kituo cha Afya Mwimbi wilayani Kalambo na Balozi wa Japan nchini, Takeda Katshotoshi, ambapo mashine hizo zitahudumia kinamama waliopo katika vijiji 40 vya Tarafa ya Mwimbi.

Akikabidhi msaada, Balozi alisema zimetolewa na serikali ya Japan kutokana na mahusiano mazuri yaliyopo kati yake na Tanzania na hivyo anaamini zitakuwa msaada kwa kinamama waliokuwa wanalazimika kusafiri umbali mrefu kufuata huduma za upasuaji.

Akipokea msaada huo, Mkuu wa Wilaya ya Kalambo, Julieth Binyura, alisema msaada huo umetolewa wakati mwafaka kwani hivi sasa serikali imejikita katika kuboresha huduma za afya kwa kujenge hospitali za kisasa pamoja na kuweka vifaa tiba.

Alisema wanawake wanaoishi katika kata tisa, vijiji 40 wapatao 75,000 watakaohitaji huduma za upasuaji wakati wa kujifungua watapata huduma hiyo kwa kutumia mashine hizo zilizopo katika kituo hicho cha afya.

Alisema kabla ya kupatikana kwa mashine hizo, wanawake waliokuwa wanahitaji kujifungua kwa njia ya upasuaji walikuwa wanalazimika kusafiri kilometa 140 ili kufika katika vituo vinavyotoa huduma hizo.

Mganga Mfawidhi wa Kituo cha Afya Mwimbi, Sospiter Mpuya, alisema tangu kituo hicho kimepokea mashine hizo Aprili mwaka huu na kuanza kutoa huduma, wanawake 62 wamefanyiwa upasuaji na kukutwa na watoto hai 61.

Alisema kuwa mtoto mmoja alipoteza maisha wakati huduma ikiendelea, lakini bila kuwapo mashine hizo huenda idadi ya vifo vya wanawake wanaohitaji kufanyiwa upasuaji na watoto wanao zaliwa kwa njia hiyo ingekuwa kubwa.

Naye Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kalambo, Magreth Kakoya, alisema halmashauri hiyo imetenga Sh. milioni kumi kwa ajili ya kuzifanyia matengenezo mashine zitakapoharibika ili kuhakikisha huduma hazikosekani.

Mmoja wa wanawake waliokuwapo katika hafla hiyo, Joyce Sikazwe, aliishukuru serikali ya Japan kwa kutambua kuwa kinamama wa Tarafa ya Mwimbi wanahitaji mashine hizo ili kuokoa maisha yao na watoto wao.

## Ukarimu unaongeza muda wa maisha

**CARFONIA,** Marekani

WANASAYANSI na wasomi katika kituo cha utafiti wanasema kuwa mtu anaweza kufanya mambo mengi zaidi ya ukarimu na kuongeza muda wa kuishi.

Wafanyakazi wa taasisi ya ukarimu ya Bedari iliyopo Chuo Kikuu cha California, huko Los Angeles (UCLA) wamesema wako tayari kwa ajili ya utani.

"Tukiangalia upande wa kisayansi. Ni kama tuko kwenye mzunguko, hapa tunazungumzia upande wa kisaikolojia na kibaiolojia," Daniel Fessler, Mkurugenzi wa taasisi hiyo alieleza.

Rais wa zamani wa Marekani, Barack Obama alisema, "Kuwa jasiri ni ukarimu. Hakuna ubaya kwa mtu kuwa dhaifu au kuwa na huruma.

"Mtu kuwajali watu wengine si udhaifu. Ni jambo jema, tunapaswa kujali wengine kwa kuwa na uadilifu na kuwajali wengine kwa heshima."

Ellen DeGeneres aliwahi kuzungumzia ukarimu wakati akizungumzia urafiki wake na George Bush na alisema, "Ninaposema kuwa mkarimu, unapaswa kuwa mkarimu kwa wengine, simaanishi kama watu wanafikiria sawa na vile wanavyotenda. Ninachomaanisha ni kwamba uwe mkarimu kwa kila mtu bila kujali." **BBC**

## Trump, Erdogan wakutana kwa mazungumzo

**WASHINGTON,** Marekani

RAIS wa Marekani, Donald Trump, anamkaribisha jana Rais wa Uturuki, Recep Erdogan katika Ikulu ya White House wakati ambapo nchi hizo zina mvutano kutokana na uvamizi wa kijeshi wa Uturuki nchini Syria.

Lakini, hatua ya Uturuki ya kununua mfumo wa Urusi wa kujilinda na makombora.

Wakuu hao wanakutana mwezi mmoja baada ya Uturuki kuanzisha mashambulizi ya kijeshi Kaskazini Mashariki mwa Syria yaliyoruhusiwa na Trump na kuibua ukosoaji mkali wa Bunge la Marekani lililotaka Uturuki kuwekewa vikwazo vikali.

Ikulu ya White House iliweka wazi kwamba lengo la Marekani ni kuzuia kurejea upya kwa waasi wa kundi linalojiita Dola la Kiislamu, IS na si kukatisha uhusiano na wana mgambo wa Kikurdi wa nchini Syria.

Rais Erdogan alikiri ziara hiyo inafanyika wakati kukiwa na uhusiano mbaya kati ya washirika hao wa jumuiya ya kujihami ya Ulaya, NATO. **DW**

# WHO yaidhinisha chanjo ya kwanza ya ebola

**DRC,** Congo

SHIRIKA la Afya Duniani, (WHO) imeidhinisha chanjo dhidi ya ebola ambayo ni ya kwanza duniani.

Dawa hiyo inayoitwa Ervebo iliyotengenezwa na kampuni ya MERCK Pharmaceuticals, ilikuwa ikitumika kwenye hatua za majaribio nchini Jamhuri ya Demokrasia ya Congo (DRC), lakini sasa WHO inasema kuna ushahidi unaoonesha kuwa chanjo hiyo inafanya kazi.

Hii ni hatua moja kubwa kwa sababu inamaanisha kuwa dunia kwa sasa ina dawa ya kwanza ya kuzuia Ebola. Kabla ya kuidhinishwa dawa hiyo hupitia kwenye awamu mbalimbali ya masuala ya usalama wa dawa na umadhubuti.

**Serikali ya nchi hiyo iliomba ruhusa kutumia dawa hiyo wakati utafiti ukiendelea kufanyika.**

Lakini chanjo hiyo imekuwa ikitumika tangu mwaka jana ili kupambana na milipuko miwili ya Ebola nchini DRC.

Serikali ya nchi hiyo iliomba ruhusa kutumia dawa hiyo wakati utafiti ukiendelea kufanyika.

Na ushahidi uliokusanywa wakati huo ndio ulioshawishi mamlaka za udhibiti kuwa dawa hizo zilikuwa zikifaa kwa matumizi dhidi ya virusi vya Ebola.

Chanjo hiyo itapatikana sokoni kuanzia katikati ya mwaka ujao.

Awali data za shirika la afya duniani (WHO) zilionyesha kuwa chanjo ya Merck ilikuwa na ufanisi kwa kiwango cha asilimia 97.5 kwa wale waliopatiwa chanjo, ikilinganishwa na wale wasiochanjwa.

WHO inasema chanjo hii imethibitisha kuwa salama na yenye ufanisi dhidi ya Ebola, lakini majaribio zaidi yanahitajika kabla dawa haijapatiwa leseni. **BBC**




Karibu watu 1,800 wamefariki kutokana na ebola nchini DRC katika kipindi cha mwaka mmoja uliopita. **PICHA : MTANDAO.**

## Sintofahamu aliyeanguka kwenye ndege

**NAIRIBI,** Kenya

MAMLAKA ya Usimamizi wa Viwanja vya Ndege Kenya (KAA) imepuuzia habari zilizochapishwa na Shirika la Utangazaji la Sky News la Uingereza kwamba Paul Manyasi aliyeanguka kutoka kwenye ndege ya Kenya Airways ni Mkenya.

Shirika hilo la habari lilisema uchunguzi wao umebaini mwanaume huyo huenda ni Manyasi kutoka Kakamega, Magharibi mwa Kenya.

Sky News walisema mwanamume huyo alikuwa anafanya kazi na kampuni ya Colnet Kenya ambayo imepewa kazi ya kufanya usafi katika uwanja wa ndege wa kimataifa wa Jomo Kenyatta, Nairobi.

Lakini, KAA imesema hakuna mtu kama huyo aliyewahi kufanya kazi JKIA.

Hatua yao ya kukanusha kuhusu uwepo wa Manyasi imezua maswali kuhusu nani hasa aliyejificha kwenye ndege hiyo na kuanguka kabla ya kutua Heathrow, London.

Baadhi ya maswali yaliyojitokeza ni pamoja na utambulisho halisi wa mwanamume anayezungumziwa baada ya anayedaiwa kuwa baba yake kudai mtoto wake yuko hai.

Sky News walisema walipata kidokezo cha kwanza kutoka kwa dereva wa teksi za Uber kwa jina Kamau aliyewajulisha kwamba yupo mfanyakazi wa kampuni ya kufanya usafi ya Colnet aliyetoweka kipindi hicho.

Alisema baadhi ya wafanyakazi walizungumzia kutoweka kwa mfanyakazi huyo.

Baadaye walikutana na mwanamke mfanyakazi wa Colnet ambaye hakutaka kutambuliwa, ambaye aliwaambia kwamba mwenzake, Paul Manyasi alitoweka mwishoni mwa Juni. **BBC**

# Utafiti wa Mzumbe waibua makubwa kilimo mkataba

**Na Romana Mallya**

CHUO Kikuu cha Mzumbe (MU) kimetoa utafiti 15 wa kilimo cha mkataba ambao umebaini kina tija na kinaongeza uzalishaji na kutaka kitumike kwenye mazao mengine yakiwamo ya chakula ili kufikia uchumi wa kati.

Mratibu wa Mradi wa Kilimo cha mkataba (POLICOFA), Dk. Mursali Milanzi, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati wakijadili kuhusu utafiti ambao umefanywa na watafiti wa chuo hicho. Dk. Milanzi alisema mradi wa kilimo cha mkataba ambao ni sehemu ya pili umejikita katika mazao matatu ambayo ni alizeti, miwa na tumbaku.

"Mambo yaliyojitokeza katika utafiti, tumeona katika tumbaku kumesaidia wakulima na maeneo ambayo kilimo hiki kinafanyika kuna maendeleo ya uwekezaji yanayotokana na kuongezeka kwa kipato," alisema.

Pia tumebaini kampuni ambazo zinanunua tumbaku zimewekeza kwenye maeneo ya miundombinu ambako wananunua zao hilo.

"Katika kilimo cha alizeti, tumeona kwamba wakulima wanaingia kwenye mnyororo wa thamani ili waunganishwe na wanunuzi duniani na wanapata uelewa mzuri kutokana na huduma za ugani zinazotolewa na kampuni zinazonunua alizeti na kujua mbegu gani zinazoweza kutumia na kuleta tija na kipato," alisema.

Dk. Milanzi alisema kwa upande wa miwa, wameona wakulima wananufaika kwenye kupata masoko na pembejeo za kilimo.

Alisema utafiti umeonyesha kilimo cha mkataba ni muhimu kwa sababu maeneo husika yanafaidika na wananchi nao wananufaika.

"Juhudi za nchi hii kwa miaka mingi zilikuwa ni kuhakikisha wakulima wadogo wanaondoka kwenye umaskini, mfano mpango wetu wa pili wa maendeleo unazungumza kutoka uchumi wa chini kwenda uchumi wa kati.

"Kwa hiyo, mfumo huu wa mkataba unaweza kusaidia kujiondoka kwenye hiyo hali, kwa sababu matokeo yanatuonyesha kilimo cha mkataba ni muhimu kwa nchi na mwananchi mmoja mmoja.

"Bila shaka serikali ikiongeza juhudi ya kuweka utaratibu mzuri wa mazao yote ya chakula na ya biashara yakaingia huku itawasaidia wakulima na nchi kwa ujumla."

Alisema ili mtu aingie huko, wengi wanatakiwa kupitia vyama vya msingi vya ushirika ambavyo sasa hivi wizara husika, inataka viimarishwe ili kusaidia wakulima.

"Matatizo wanayoyapata wakulima, vile vyama vya msingi havifanyi kazi kwa utaratibu mzuri, havikuwa na tija haviwasaidii wakulima, tunaamini juhudi za serikali inayofanya, vikiimarishwa kilimo cha mkataba kitakuwa na manufaa makubwa.

"Kilimo cha mkataba kinaweza kuonekana hakina manufaa kwa sababu vyama vya ushirika havijakaa vizuri."

Naibu Makamu Mkuu wa Chuo (Taaluma), Prof. Ganka Nyamsogoro, akimwakilisha Makamu Mkuu wa Chuo hicho, alitaka kilimo cha mkataba kiende kwenye mazao mengine ili kuwezesha nchi kufikia uchumi wa kati.

Mkatibu wa kwanza wa mradi huo ulioanza mwaka 2011, Prof. Joseph Kuzilwa, ambaye kwa sasa ni mstaafu wa chuo hicho, alisema kuna haja ya kuwa na mfumo ambao wakulima na wanunuzi watajiona ni wanufaika.


Distributed via ippmedia

Mkurugenzi Mkuu wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), Dk. Samuel Gwamaka (kulia), akishiriki zoezi la uteketezaji wa mifuko mbadala iliyo chini ya kiwango baada ya kukamatwa jijini Mwanza juzi, kwa mmiliki ambaye ni kiwanda cha Jin Yuan Investment. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Dawa bandia aina saba zakamatwa

**Na Devota Mwachang'a**

MAMLAKA ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA) kupitia ukaguzi maalum imekamata dawa bandia aina saba zenye thamani ya Sh. 12,495,500 ikiwamo aina ya Sulphadoxine Pyrimethamine (SP) za kutibu malaria.

Ukaguzi maalumu (operesheni) uliofanyika Oktoba kufuatia taarifa ya kuwapo kwa matukio kadhaa ya dawa duni na bandia katika baadhi ya nchi zilizopo katika Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC).

Hayo yamebainishwa na Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa TMDA, Akida Khea, alipotoa taarifa ya matokeo ya ukaguzi maalum (operesheni) wa dawa, vifaa tiba, vitendanishi, dawa asili na tiba mbadala kwa wanahabari Dar es Salaam jana.

Alitaja majina ya dawa hizo bandia ni Sonaderm Cream 10g (Clobetaso Proprionate, Miconazole, Nitrate & Gentamicin Sulphate, Gentrisone Cream 10g ( Betamethasone, Propri-onate, Clotrimazole& Gentamycin Sulfate), Sulphadoxine Pyrimethamine, ALPRIM (Sulfamethoxazole 400mg +, Trimethoprim 80mg) tablets. Nyingine ni Homidium Chloride, Cold Cap na TEMEVAC NDV strain 1&2 ambayo ni chanjo ya kuku kwa ajili ya ugonjwa wa mdondo.

Aidha, Khea alisema pamoja na kubainika kwa uwapo wa dawa hizo bandia, zipo dawa halisi na zisizosajiliwa na TMDA zenye majina ya dawa halisi. Kwa majibu wa Khea, mamlaka imekamata dawa na vifaa tiba visivyosajiriwa vyenye thamani ya Sh. 48,959,110 pamoja na vifaa tiba duni vyenye thamani ya Sh. 640,000.

Khea alisema wahusika kwenye maeneo yaliyokutwa na dawa bandia na vifaa tiba visivyosajiliwa wamefikishwa katika vyombo vya usalama ambapo jumla ya majalada 19 ya kesi yamefunguliwa dhidi yao katika vituo mbalimbali vya polisi nchini, watafikishwa mahakamani kwa majibu wa Sheria ya Chakula, Dawa na Vipodozi Sura 219 na sheria nyingine za nchi.

# Bonite yakabidhi zawadi kwa washindi wake

**Na Mary Geofrey**

KAMPUNI ya Bonite Bottlers Ltd ya Moshi, mkoani Kilimanjaro, inayozalisha vinywaji baridi, imekabidhi zawadi kwa washindi wa droo ya kwanza ya shindano la Maji ya Kilimanjaro kwa wateja wa mikoa ya Dar es Salaam, Pwani na Morogoro.

Jumla ya wateja 45 walishinda katika droo iliyochezeshwa Novemba 7, mwaka huu, kati yao 15 walishinda pikipiki kila mmoja, 15 Televisheni kila mmoja na wengine 15 walishinda moja katoni 50 za maji kila mmoja.

Akizungumza na waandishi wa habari jana kabla ya kukabidhi zawadi hizo kwa washindi, Meneja Mauzo na Masoko wa Bonite Bottlers Ltd (BBL), Christopher Loiruk, alisema shindano hilo lilizinduliwa Oktoba 7, mwaka huu na lengo ni kuwashukuru wateja wao kwa kuendelea kutumia maji ya Kilimanjaro.

Alisema washindi waliokabidhiwa zawadi zao walishinda katika droo iliyochezeshwa wiki iliyopita na kuhusisha kanda tano katika mikoa hiyo mitatu kulingana na mgawanyo walioweka ili shindano hilo liwanufaishe wakazi wote wa mikoa hiyo.

Alisema Kanda A ilihusisha maeneo ya katikati ya jiji la Dar es Salaam, Kariakoo, Upanga na Kigamboni; kanda B inahusisha maeneo ya Tabata, Ilala, Mbagala, Kurasini na Mkuranga wilayani Kisarawe.

Alisema kanda C ilihusisha maeneo ya Sinza, Mwenge, Kinondoni na Tegeta, kanda D ni maeneo ya Mbezi Beach, Mikocheni, Masaki na Kibaha na kanda E inahusisha maeneo ya Manzese, Kimara, Makumbusho, Bagamoyo na Mkoa wa Morogogoro.

"Bado tunaendelea na shindano letu la kuwapata washindi wa awamu ya pili, ambao watashinda pikipiki 15, watashinda Televisheni 15 na maji ya Kilimanjaro katoni 50 kila mmoja," alisema Loiruk.

Aliyataja majina ya washindi 15 waliokabidhiwa pikipiki kwa majina na walikotoka katika mabano kuwa ni Isdory Asenga (Kibaha), Manford (Kariakoo), Zubeda Mpili (Mbagala), Ayoub Moukiwa (Uwanja wa Taifa), Gasper Urassa (Palestina), Omega Bupamba (Boko), Mary Goodluck (Dar es Salaam), Debora Njau (Kunduchi), Michael Tesha (Kinyerezi), Godlizen Sam (Masaki), Mary Shokole (Bagamoyo), Alex Mrina (Manzese), Misriya Asnee (Juwata), Sophia Omary na Juma Mbanga (Morogoro).

Aliwataja washindi wengine 15 wa televisheni ni Flora Shirima (Agrey), Gabriel Kavina (Banana), Johari Mussa (Tabata), Mary Kimaro (Ilala), Geofrey (Mwananyamala), Erasmos Mwacha(Tegeta), Innocent Adelin (Sinza), Nabel Abdallah (Sinza), Yona Mwanja (Kibaha), Tarimo (Mikocheni), Suzani (Manzese), Mary Joseph (Manzese), Mary Munishi (Morogoro), Antony Chami (Soko), Varelian Mallya (Morogoro).

Wengi 15 waliokabidhiwa katoni 50 za maji kila mmoja ni Kenan (Ungindoni), Agnes Massawe (Tabata), Erick Mroso (Kariakoo), Stellah Sanga (Tabata), Godfrey Sebastian (Sinza), Agnes Pascal (Tegeta), Praxeda Paschael (Kinyerezi), Tedi Jeimwami (Kawe), Francis Marandu(Msasani), Jason (Shekilango), Mussa omiro (Kijitinyama), Neema Roita (Mzumbe), Sera Mkasholika (Kingo), Haridy Naganga (Kihonda) na Cornelus (Msasani).

Baadhi ya washindi hao, waliushukuru uongozi wa maji ya Kilimanjaro kwa kuwapa zawadi hizo na kuahidi kuendelea kutumia huduma hiyo yenye viwango vya hali ya juu nchini.

## TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

### NYUMBA/VIWANJA

**NYUMBA 2 ENEO MOJA ZINAUZWA** Zipo Ukonga Mombasa. Ya mbele Jengo wa kisasa vyumba 4 nyingine chumba na sebule 4 kiwanja robo eka. Za kupaua. Bei maelewano. Piga simu: 0719 619444 / 0782 574669.

**VIWANJA VITATU VINAUZWA,** NO.1-1341-1890 SQM NO. 2-1342- 1391 SQM NO.3 1343- 1556 SQM BLOCK A KISUKURU-TABATA. SIMU. 0754 857523/0786 857523

### NAFASI ZA KAZI

**Wanahitajika wanaume wenye umri kuanzia miaka 30 hadi 45** kwa nafasi za udereva (Ikiwemo Class C, C1, C2 na C3). Wanahitajika wanawake wenye umri kuanzia miaka 25 hadi 35 kwa nafasi za mauzo (sales za bidhaa). Mshahara wa kuvutia utatolewa. Mawasiliano piga 0714 634 046. Piga simu kuanzia saa mbili asubuhi hadi saa kumi jioni tu.

### 2 ACRE YARD FOR RENT


Facing New Julius Nyerere International Airport. Call: +255 754 375 967. Email: **gold@goldtz.net**

### MCHANGANYIKO

**MONKAL I INSULIN**:Inawasaidia wagonjwa waliogua kisukari kwa muda mrefu,inarejesha kongosho ktk utoaji ute mchungu na sukari kuwa normal balance 4- 5- 6, iko katika mfumo wa maji na vidonge,husaidia mmengenyo wa chakula,tiba lishe,gout,uzazi,tumbo la vidonda na kuunguruma na kujaa gesi n.k :0713293988/0758078280.

*Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe*

### KUPOTEA KWA VYETI



**JOSEPH HUSSEIN JOHN** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S0784-0342 kilichotolewa na AIRWING SEKONDARI mwaka 2007. Cheti cha Diploma chenye index namba 2013/D00647 kilichotolewa na UNIVERSITY OF UDSM COMPUTING CENTRE mwaka 2013.

Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha polisi.

**Taarifa ya polisi: GBT/RB/4880/18.**

115516502

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M. 1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**
**Katika Mahakama ya Mwanzo: JIJINI TANGA**
**Usimamizi wa Mirathi No. 159/2019**

Ombi la SALIMU PASHUA kuteuliwa msimamizi wa mirathi ya Marehemu MWANAMVUA SALIMU SHABANI

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya Marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 21/11/2019.

kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia wa Marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa. **Tarehe 01/11/2019**

HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA MWANZO
TANGA MJINI

115516602

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M. 1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**
**Katika Mahakama ya Mwanzo: PONGWE**
**Usimamizi wa Mirathi No. 18/2019**

**Ombi la ABDALLA MOHAMED GUIDO** kuteuliwa msimamizi wa mirathi ya Marehemu MOHAMED ALLY GUIDO

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya Marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 25/11/2019.

kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia wa Marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa. Tarehe 11/11/2019

HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO
PONGWE

115516702

---

### KUPOTELEWA KWA KADI YA KADI YA GARI


JOHN ADAM HAULE anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya Toyota Landcruiser T 745 ABD yenye Chassis namba HZJ750001715 na Injini namba, IHZ0006308.

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

Taarifa ya polisi:
**KIL/HAI/RB/465684/2019.**

115516802

### VYETI VIMEPOTEA



**FULGENCE FREDRICK MUZAMBELE** anatangaza kupotelewa na vyeti vya CHETI CHA FORM FOUR chenye **No. S.1530-0054** kilichotolewa na NACTE mwaka 2012, CHETI CHA UUGUZI chenye **No.71332** kilichitolewa na chuo cha St. Gasper Nursing School mwaka 2019, CHETI CHA UKUNGA **NO.60602** kilichotolewa na chuo cha St. Gasper Nursing School mwaka 2019 pamoja na Leseni ya UUGUZI NA UKUNGA **NO. 51982** kilichotolewa na St. Gasper Nursing School mwaka 2019.

**Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi.taarifa ya polisi: NM/RB/631/2019**

115516402

### KUPOTEA KWA CHETI



**IRENE GEOFREY SHILLA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0491/0025** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **KILOMENI GIRLS SECONDARY** mwaka 2014. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/KIJ/RB/464162/2019.**

115515502

### KUPOTEA KWA CHETI



**THOMAS M.K ZACHARIA** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S115/0116** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 1994 katika shule ya Sekondari KAHORORO. Yeyote atakaeion atoe taarifa kituo chcochote cha Polisi.
Polisi Taarifa: **KAG/KYA/RB/222356**

115515202

### KUPOTEA KWA KADI YA KADI

PROJECT HEALTHY CHILDREN LIMITED anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili T 141 DKS TOYOTA HILUX.

eyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi:
**DAR/SEL/RB/464703/2019.**

115516302

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KTK MAHAKAMA YA MWANZO MJINI**
**ILIYOPO MOROGORO**
**TANGAZO LA KUITWA SHAURINI**
**SHAURI LA MADAI NAMBA: 261..2019**
**Mdai: ZUHURA SAID MAYANDA**

**DHIDI YA**

| | |
|---|---|
| **Mdaiwa:** | **MOSHI HABIBU** |
| **Kwa:** | **MOSHI HABIBU WA CHAMWINO** |
| **Ombi la Mdai:** | **ZUHURA SAID MAYANDA** |
| **Madai ya:** | **PESA SHILINGI 2,170,375/=** |

Unatakiwa kuudhuria hapa mahakamani ktk shauri tajwa hapo juu bila kukosa.Shauri limepangwa kusikilizwa mnamo tarehe 19 mwezi 11 mwaka 2019 saa 02:30 Asubuhi.

Angalia kama hukuudhuria/hamkuudhuria siku iliyotajwa hapo juu.Mahakama ikidhibitisha kama umepokea/mmepokea kuitwa shaurini,hii itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa /mmeshindwa.

Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya mahakama hii leo tarehe 13 mwezi 11 mwaka 2019.

HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO MJINI
MOROGORO.

115516202

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**
**Katika mahakama ya mwanzo**
**CHAMWINO MOROGOR**
**Usimamizi wa mirathi No;70/2019**

**Ombi la NEEMA JAMES KIGUNE Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu MARRY JOHN CHIWALA**

**Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 10/12/2019 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.**

**Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 11/11/2019**

Sahihi ya Hakimu.
RESIDENT MAGISTRATE
MOROGORO

115516102

### KUPOTEA KWA CHETI



**SCOLASTICA KASHAMAKULA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S2120.0015** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **SHULE YA SEKONDARI KATUMA** mwaka 2014. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **MBE/MBE/RB/434179/2019.**

115515802

### KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**LINUS MAEMBA CHUWA** anatangaza kupotelewa na kadi ya Pikipiki yenye namba za usajili **T 492 ASK – HONDA.**

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi:
**DAR/OST/RB/455542/2019.**

115515702

### KUPOTEA KWA RESULT SLIP/HATI YA MATOKEO



**SHEYNAZ SAID CHITUNDU** anatangaza kupotea kwa Result slip/Hati ya matokeo ya kidato cha nne yenye index namba **S4104/0042** iliyotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2017 katika shule ya Sekondari **LORD BADEN POWELL MEMORIAL.** Yeyote atakaeion atoe taarifa kituo chcochote cha Polisi.
Polisi Taarifa: **DAR/GOG/RB/466321/2019**

115515402

### KUPOTEA KWA RESULT SLIP/HATI YA MATOKEO



**DAUD ADAM BWAKI** anatangaza kupotea kwa Result slip/Hati ya matokeo ya kidato cha nne yenye index namba **S.0130.0545** iliyotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2019 katika Shule ya Sekondari **MAUA SEMINARY.** Yeyote atakaeion atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Polisi Taarifa: **9910810670450**

115515302

### KUPOTEA KWA KADI

**HAMISI O. SALEHE** anatangaza kupotea kwa kadi ya **BAJAJ aina ya TVS** yenye namba ya usajili **MC 576 AJT** iliyotolewa na Mamlaka ya Mapato Tanzania . Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

Polisi Taarifa:
**DAR/GOG/RB/418035/2019**

115515102

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# JUNINHO AMUITA BENZEMA LYON



**LYON,** Ufaransa

MKURUGENZI wa Soka wa Klabu ya Lyon, Juninho, amemtaka mshambuliaji wa Real Madrid, Karim Benzema, kumalizia kipindi chake cha uchezaji kwenye klabu ya Ligi Kuu ya Ufaransa, Ligue 1.

Benzema mwenye umri wa miaka 31, alitokea akademi ya Lyon na aling'ara kwenye Ligue 1 kabla ya kujiunga na Madrid kwa ada ya uhamisho ya euro milioni 35 Julai mwaka 2009.

Mfaransa huyo amefunga mabao 233 pale Madrid, akiwasaidia miamba hao wa Hispania kushinda mataji mawili ya LaLiga na manne ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Juninho, ambaye alicheza pamoja na Benzema pale Lyon, anamtaka mshambuliaji huyo kurudi kwenye klabu hiyo.

"Matarajio yangu ni kuona Karim anamaliza kipindi chake cha kucheza soka pale Lyon," akisema wakati wa mahojiano yake ya televisheni ya nchini Brazil ya OLTV.

"Anatoka pale, anahisia na pale. Nafikiri itakuwa vizuri zaidi kumalizia kipindi chake cha kucheza soka.

"Tunaweza kumpa mshahara kama wa pale Real Madrid, lakini tutahitaji muda zaidi.

"Tuliwasiliana kwa ujumbe wakati nikiwa hapa Brazil. Nahisi kwamba akirudi pale atakuwa na wakati mzuri zaidi.

"Nataka aje na kucheza na sisi kwa kipindi cha miaka miwili au zaidi, na pia kuwafundisha wachezaji vijana."

Distributed via ippmedia

# Koeman amtaka Depay kusepa Lyon

**AMSTERDAM,** Uholanzi

MEMPHIS Depay iwapo ataondoka Lyon na kujiunga na "klabu kubwa" kunaweza kuwa faida kwa kikosi cha Uholanzi, kwa mujibu wa kocha Ronald Koeman.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25, alisajiliwa kwa miamba hao wa Lyon Januari mwaka 2017 na amerudi kwenye kiwango chake baada ya kuwa na wakati mgumu wa kipindi cha miezi 18 kule Manchester United.

Alifunga mabao 29 katika misimu yake miwili ya Ligi Kuu ya Ufaransa, Ligue 1, na ana mabao saba ndani ya mechi 10 msimu huu, huku akiwa anahusishwa na mpango wa kutakiwa na klabu kadhaa kubwa, ikiwamo Tottenham.

Ingawa kwa sasa inatambulika kwamba Lyon ni moja ya klabu kubwa, bosi huyo wa Uholanzi, Koeman anaamini Depay ataimarika zaidi kama atakwenda timu mpya mwakani.

"Anacheza pale Lyon na kuna wakati anakuwa nahodha," alisema Koeman Jumanne wakati akizungumza na waandishi wa habari.

"Ukweli ni kwamba, hachezi klabu kubwa duniani na hilo lina matokeo kwa timu ya taifa. Lakini kama atapata nafasi ya kuichezea moja ya klabu kubwa duniani, itakuwa na faida kubwa kwa Uholanzi.

"Ndio, bado Lyon pia ni klabu kubwa ambayo mara zote inacheza kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya. Lakini ukweli ni kwamba, hilo halimsaidii kwenye timu ya taifa."





# *Man United yajitosa tena kwa Ibrahimovic*

**MANCHESTER,** England

KLABU ya Manchester United inafikiria kumrejesha mshambuliaji wake wa zamani, Zlatan Ibrahimovic wakati wa dirisha dogo la uhamisho la Januari, kwa mujibu wa ESPN.

Nyota huyo wa zamani wa kimataifa wa Sweden mwenye umri wa miaka 38, anatazamiwa kuwa mchezaji huru mwishoni mwa Desemba na ingawa AC Milan imepewa nafasi zaidi ya kumchukua lakini inatabiriwa na Man United huenda ikatoa ofa.

Zlatan aliondoka Old Trafford mwaka 2018 kwenda LA Galaxy ya Marekani baada ya kuichezea United kwa mafanikio katika vipindi viwili, lakini upatikanaji wake wa bure unaweza kuishawishi United irudi tena wakati huu kiwango chake bado kikiwa juu.

Man United imekuwa na tatizo kwenye safu yake ya ushambuliaji na baada ya kuwapiga bei mastaa wake akiwamo Romelu Lukaku.

## Vieira aishauri Arsenal kumpa muda Emery

**LIONDON,** England

NAHODHA wa zamani wa Arsenal, Patrick Vieira amesisitiza Unai Emery anastahili kupewa muda zaidi hapo kwa 'Washika Bunduki' hao.

Presha imekuwa kubwa kwa Emery baada ya kichapo cha mabao 2-0 kwenye Ligi Kuu ya England na Leicester City.

Arsenal tayari imepitwa pointi nane kwenye nne bora baada ya mechi 12 na imeshinda mechi moja tu katika mechi saba zilizopita kwenye mashindano yote.

Wakati inaaminika kwamba vigogo wa klabu hiyo wapo nyuma ya Emery, ambaye aliteuliwa kuchukua mikoba ya Arsene Wenger kipindi cha msimu wa 2017-18, kuna presha kubwa kutoka kwa mashabiki wa Arsenal ambao wanaamini kocha huyo hana uwezo wa kuiongoza timu hiyo.

Vieira, ambaye aliiongoza Arsenal kushinda mataji matatu ya Ligi Kuu, amesema sasa ni wakati wa klabu kuungana na kuwa pamoja na kocha huyo wa zamani wa Paris Saint-Germain katika kipindi hiki.

"Ni kweli kwamba, Arsenal wanapitia kipindi kigumu," alisema akiwaambia waandishi wa habari Jumatatu.

"Lakini sijaangalia mechi zao zote, hivyo siwezi kuzungumzia kuhusu mechi zao.





Distributed via ippmedia

## MODRIC AITAMANI SERIE A

**MADRID,** Hispania

KIUNGO wa Real Madrid, Luka Modric amebainisha kwamba alitaka kucheza soka nchini Italia na amefunguka kwamba, anaweza kucheza kwenye ligi hiyo ya Serie A kwa siku za usoni.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 34, alipewa tuzo ya Kiatu cha Dhahabu Jumanne, ikiwa ni zaidi ya mwaka baada ya kushinda tuzo ya Ballon d'Or kwa kiwango bora kwenye Kombe la Dunia mwaka 2018.

Hata hivyo, Modric ameanza mechi tatu za Ligi Kuu ya Hispania, LaLiga, msimu huu kwa Madrid na awali alikuwa akihusishwa na mpango wa kutua kwa klabu za jijini Milan, Inter na AC.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Croatia, amesema alikuwa anafuatilia Ligi ya Serie A na huwa anaifurahia Italia, na sasa ana uwezekano wa kuhamia huko siku za usoni.

"Naipenda Italia, ni jirani na Croatia," alisema akiiambia Sky Sport. "Nafuatilia Ligi ya Serie A kwa sababu wachezaji wenzangu wengi wa timu ya taifa wanacheza kule.

"Waitaliano wanavutia na wana hamasa kama sisi watu wa Croatia."

Modric aliongeza: "Tutaona kama siku moja nitacheza nchini Italia. Siwezi kuzungumza sana kuhusu hili kwa sababu kwa sasa mimi ni mchezaji wa Real Madrid.

"Napenda kuwa hapa Real na kwa sasa naona majaliwa yangu sehemu nyingine."

Modric amekuwa Madrid tangu mwaka 2012, wakati alipotua hapo akitokea Tottenham, na amecheza zaidi ya mechi 300 kwa klabu yake.

# *David Villa atangaza kustaafu soka rasmi*

**BARCELONA,** Hispania

NYOTA wa zamani wa Hispania na Barcelona, David Villa ametangaza kwamba atastaafu rasmi kucheza soka la ushindani mwishoni mwa mwaka huu.

Villa, ambaye atatimiza umri wa miaka 38 mwezi ujao, ametangaza Jumatano kwamba atastaafu mwisho wa msimu huu kule katika klabu ya Vissel Kobe.

Mshambuliaji huyo amefunga mabao 12 katika mechi 26 alizoichezea klabu hiyo kwenye Ligi Kuu ya nchini Japan, J.League, klabu ambayo alijiunga nayo baada ya kucheza kule New York City, Marekani.

"Asante kwa kiwango bora @ Guaje7Villa," iliandika klabu ya Vissel Kobe kwenye ukurasa wake wa Twitter, wakati ikithibitisha kwamba Villa atastaafu mwishoni mwa msimu huu.

Villa alifurahia kipindi kizuri cha kucheza soka akianzia pale klabu ya Sporting Gijon kabla ya kuhamia Real Zaragoza na baadaye Valencia.

Baada ya kufunga mabao zaidi ya 100 pale Valencia, Villa alijiunga na Barcelona kwa misimu mitatu – akishinda mataji mawili ya Ligi Kuu ya Hispania, LaLiga na Ligi ya Mabingwa Ulaya, kabla ya kuhamia Atletico Madrid.

Villa baadaye alitumia misimu minne akiwa na klabu ya New York City na akakaa kwa muda pale Melbourne City kabla ya kuelekea nchini Japan.

Pia ameichezea Hispania mechi 98, akishinda taji la Euro 2008 na Kombe la Dunia mwaka 2010, na anashikilia rekodi ya kufunga mabao mengi kwa timu ya taifa, akitikisa nyavu mara 59.

Villa alishinda Kiatu cha Dhahabu kwenye michuano ya Euro 2008, huku akifunga mara tano kwenye Kombe la Dunia mwaka 2010.

Ilithibitishwa Jumanne kwamba Villa yupo tayari kuwekeza kwenye klabu ya Queensboro FC.



HABARI MICHEZO

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# SALAH KUIKOSA KENYA LEO KUFUZU AFCON 2021

## Vipimo vya kitabibu vimethibitisha hayupo tayari pia kuivaa Comoros baada ya...

**CAIRO,** Misri

MSHAMBULIAJI wa Liverpool, Mohamed Salah ameachwa katika kikosi cha Misri kinachojiandaa kuivaa Kenya na Comoros kwenye mechi ya kuwania kufuzu fainali za Mataifa ya Afrika (Afcon) 2021 kutokana na jeraha la kifundo cha mguu 'enka' linaloendelea kumsumbua.

Misri itaikaribisha Kenya mjini Alexandria leo katika mechi yake ya kwanza ya hatua ya makundi ya kuwania kufuzu Afcon kabla ya siku nne baadaye kusafiri kuelekea Moroni tayari kuvaana na Comoros.

**Salah amekuwa akisumbuliwa na tatizo hilo tangu Liverpool ilipoibuka na ushindi dhidi ya Leicester City mwezi uliopita, wakati akiwa katika harakati za kumpita kiungo wa timu hiyo, Hamza Choudhury.**

Mshambuliaji huyo mwenye umri wa miaka 27, alionekana kuwa katika maumivu tena Jumapili wakati wa mechi dhidi ya Manchester City.

Aliguswa na Fernandinho wakati Liverpool ikishinda 3-1, na mwanzo alilazimika kuendelea kulala chini kabla ya dakika ya 87, na alionekana mguu umefungwa wakati wote.

Salah alijiunga na nyota wenzake wa kimataifa Jumatatu wiki hii, lakini Chama cha Soka Misri (EFA) kimetangaza Salah hatacheza dhidi ya Kenya ama Comoros.

"Vipimo vya kitabibu vimethibitisha Salah hayupo tayari kuivaa Kenya na Comoros," taarifa rasmi kupitia ukurasa wa Twitter wa EFA ilisomeka.

Salah ana mabao tisa katika mashindano yote Liverpool msimu huu, ikiwamo matano katika mechi saba zilizopita.

## ZISIKUPITE

### MBAPPE APANIWA MADRID

REAL Madrid inafikiria kuweka rekodi ya dunia kwa kutoa ofa ya pauni milioni 340 kwa mshambuliaji wa Paris St Germain, Kylian Mbappe, 20. ***(Le Parisien via Calciomercato)***

### RONALDO KUTOADHIBIWA JUVE

CRISTIANO Ronaldo hatapigwa faini na Juventus kwa kitendo alichokionyesha baada ya kufanyiwa mabadiliko katika mchezo wa pili, bali mshambuliaji huyo wa kimataifa wa Ureno mwenye umri wa miaka 34, atakuwa akitarajiwa kuomba radhi kwa wachezaji wenzake. ***(Gazzetta dello Sport, in Italian)***

### CAMAVINGA AIVUTIA MAN CITY

MANCHESTER City ipo tayari kutoa changamoto ya kuinasa saini ya kinda mwenye kipaji wa Rennes, Eduardo Camavinga, 17, baada ya kiungo huyo mzaliwa wa Angola kuvutia mwanzoni mwa msimu wa Ligue 1. ***(90min)***

### BARCA NAYO KWA HAALAND

BARCELONA inavutiwa na mshambuliaji wa Salzburg, Erling Braut Haaland, 19, kama mbadala wa Luis Suarez, 32, lakini haipo tayari kufika dau la pauni milioni 85 zinatotakiwa na klabu hiyo ya Austria. ***(ESPN)***

### LAMPARD AKOMALIA NIDHAMU

KOCHA Frank Lampard ameweka sheria kali ili kuleta nidhamu katika kikosi cha Chelsea baada ya kuweka faini ya pauni 2,500 kwa wachezaji wanaochelewa mazoezini. ***(Mirror)***

### XHAKA ASAKA NYUMBA ITALIA

KIUNGO wa Uswisi, Granit Xhaka, 27, amekuwa akitafuta nyumba Italia kabla ya kupendekeza kujiunga na AC Milan katika dirisha la Januari baada ya kuvuliwa kitambaa cha unahodha Arsenal. ***(RSI via Star)***

### LORENZO KUMRITHI ERIKSEN

TOTTENHAM imemweka alama kiungo wa Roma, Mtaliano Lorenzo Pellegrini, 23, kama mbadala sahihi wa Christian Eriksen. ***(Football Italia)***

### MATIC ATAKA KUSEMA UNITED

NEMANJA Matic anataka kuondoka Manchester United, ikiwezekana mapema Januari, na Italia ikiwa kituo sahihi kwake kinachofuata kwa kiungo huyo Mserbia mwenye umri wa miaka 31. ***(Telegraph)***

### POCHETTINO MAJARIBUNI

KOCHA wa Tottenham, Mauricio Pochettino anaweza kutimuliwa kama Spurs itapoteza mechi dhidi ya West Ham baada ya mapumziko ya mechi za kimataifa. ***(Telegraph)***

### ATAKIWA KUSTAAFIA LYON

LYON inamtaka mshambuliaji wa Real Madrid, Karim Benzema, 31, kumalizia soka lake sehemu alipoanzia - na klabu hiyo ya Ufaransa. ***(Mundo Deportivo, in Spanish)***

### DEPAY AKATAA TETESI SPURS

MSHAMBULIAJI wa Lyon na Uholanzi, Memphis Depay, 25, amesema "hataki kuzungumzia kuhusu tetesi" baada ya kuhusishwa na kujiunga na Tottenham kwa pauni milioni 50. ***(Football.London)***

## HABARI MICHEZO

# KASEJA: STARS YA WOTE, NJOONI TAIFA

**Na Focus Nicus**

WAKATI mjadala wa kuachwa kipa wa Simba, Aishi Manula katika kikosi cha Taifa Stars ukizidi kupamba moto, huku Juma Mgunda akiandamwa kwa kauli yake dhidi ya mlinda mlango huyo, Juma Kaseja amesema timu hiyo ni ya Watanzania wote na hawana budi kuungana pamoja Uwanja wa Taifa kesho.

Mashabiki wa soka nchini wamekuwa wakilalamika kwa kitendo cha Manula kutoitwa Stars, huku Mgunda akilaumiwa kwa kauli yake aliyoitoa alipoulizwa kwa nini kipa huyo hakujumushwa katika kikosi hicho.

Kikosi cha Stars kilichopo kambini kujiandaa na mechi dhidi ya Equatoria Guinea kuwania kufuzu fainali za Mataifa ya Afrika (Afcon) 2021, baada ya kutangazwa, Mgunda aliulizwa kwa nini Manula hakujumuishwa katika timu hiyo na kujibu "hawaangalii sura", kauli ambayo imezua mjadala mzito kwa mashabiki, mitandao ya kijamii na hata kwa baadhi ya vyombo vya habari.

Hata hivyo, Mgunda ametolea ufafanuzi vizuri akieleza kuwa hakuwa na lengo baya kwa Manula na kwamba alinukuliwa vibaya kwa kuchukuliwa sehemu fupi ya mazungumzo yake kwani alikuwa akiimaanisha wameita kikosi hicho kulingana na mahitaji ya sasa na kwamba bado wanaheshimu mchango wa kipa huyo na kwamba huu si mwisho kwake kukitumikia Stars.

Lakini Kaseja akizungumzia timu hiyo alisema Taifa Stars ni ya wachezaji wote walioitwa na wasiotwa kuitumikia kwa sasa, lakini pia ni ya Watanzania wote, na kwamba huu ni wakati wakuungana pamoja kwenda kuisapoti uwanjani.

"Timu hii ni ya Watanzania wote, waliopo ndani ya kikosi na ambao hawakuitwa, cha muhimu kwa sasa ni kushirikiana kuelekea katika mechi yetu dhidi ya Equatorial Guinea," alisema.

Licha ya Kaseja kuruhusu mabao mengi katika klabu yake (nane) ukilinganisha na Manula (matatu) kwenye Ligi Kuu msimu huu hadi sasa, mlinda mlango huyo wa KMC FC, amekuwa katika ubora wa hali ya juu na inaonekana kinachomuangusha klabuni ni safu yao ya ulinzi.

Kaseja amefanya kazi kubwa kwa kuiwezesha Stars kutinga hatua ya makundi ya kuwania kufuzu fainali za Kombe la Dunia Qatar 2022 pamoja na michuano fainali ya Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN) itakayofanyika nchini Cameroon mwakani.


Distributed via ippmedia

Wachezaji wa timu ya Villa Squad, wakifanya mazoezi katika Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Msuva atoa neno Equatorial Guinea

**Na Shufaa Lyimo**

MCHEZAJI wa timu ya Taifa, Taifa Stars ambaye pia anacheza soka la kulipwa nchini Morocco, Simon Msuva, amesema amejipanga vizuri kuhakikisha anasaidiana vema na wenzake kuisambaratisha Equatorial Guinea katika Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam kesho.

Stars itaikaribisha Equatorial Guinea katika mechi hiyo ya kwanza kwao kuwania kufuzu fainali za Mataifa ya Afrika (Afcon) nchini Cameroon 2021.

Akizungumza jana asubuhi na gazeti hili, Msuva alisema atayatumia vizuri maelekezo ya mwalimu ambayo anaamini yatamsaidia kuipa matokeo Stars.

"Kikubwa ni kufuata na kumsikiliza mwalimu kwa makini pindi anapokuwa anafundisha," alisema Msuva.

Aidha, mchezaji huyo aliwataka Watanzania kujitokeza kwa wingi uwanjani ili wawape sapoti, na kuongeza bila wao hawawezi chochote.

"Naomba Watanzania waje kwa wingi uwanjani ili watupe sapoti katika mchezo huu, lengo ni kuibuka na ushindi nyumbani," alisema Msuva.

Alisema mchezo huo utakuwa mgumu na wenye ushindani kutokana na kila timu kuhitaji kuanza kwa ushindi.

"Tunamuomba Mungu atusaidie tupate matokeo mazuri nyumbani kabla ya kwenda Libya," alisema Msuva anayeichezea Difaa El-Jadida inayoshiriki Ligi Kuu Morocco.

# *Zanzibar Queens yajigamba Cecafa*

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

WAKATI timu ya Taifa ya Wanawake ya Zanzibar, Zanzibar Queens ikitarajia kutua jijini Dar es Salaam leo ikitokea visiwani hapa, tayari kwa ajili ya michuano ya Afrika Mashariki na Kati (Cecafa Challenge) kwa wanawake inayotarajiwa kuanza kutimua vumbi Jumamosi wiki hii, benchi la ufundi la timu hiyo limetamba kufanya kweli.

Awali michuano hiyo ilipangwa kuanza kutimua vumbi Novemba 14, mwaka huu, lakini ikasogezwa mbele kwa siku mbili ili kutoa nafasi ya kutosha kwa timu ya Taifa ya Tanzania (Taifa Stars) ambayo kesho itaikaribisha Equatorial Guinea katika mechi ya kuwania kufuzu fainali za Mataifa ya Afrika (Afcon) nchini Cameroon 2021.

Katika michuano hiyo ya Cecafa, ambayo itafanyika kwenye Uwanja wa Chamazi, Zanzibar Queens itaanza kutupa karata yake dhidi ya Burundi katika mechi yake ya Kundi A, ambalo linazijumuisha pia Kilimanjaro Queens (Tanzania Bara)na Sudan Kusini.

Kocha Mkuu wa kikosi hicho, Mohmed Salah aliliambia Nipashe kuwa kikosi chake kinakuja jijini Dar es Salaam kushindana na si kushiriki michuano hiyo.

Salah alisema wamefanya maandalizi mazuri ikiwa ni pamoja na kucheza mechi mbili za kirafiki dhidi ya timu za wanaume na kupoteza zote ambapo walifungwa mabao 4-0 dhidi ya Kombaini ya Wilaya ya Mjini kabla ya kukung'utwa 7-0 dhidi ya Jangombe Boys U-21.

Alisema kikosi hicho kitaondoka leo visiwani hapa kikiwa na wachezaji 20 pamoja na benchi la ufundi lenye viongozi watano.

Aliwataja wachezaji 20 wanaounda kikosi hicho kuwa ni makipa watatu ambao ni Khadija Sale Ali, Khajra na Zena Yunus, huku kwa upande wa mabeki wakiwamo Mwajuma Abdallah, Aziza Mwadini, Merry Charles, Neema Suliman, Warda Abdul-hakim, Riziki Abdallah na Warda Halid.

Viungo ni Sabahi Hashim, Iptsam Salum, Nasrin Mohmed, Farida Khamis, Pili Suleiman na Hawa Ali, wakati washambuliaji ni Hafidha Juma, Neema Machano, Siwazui Mrisho na Riziki Abubakar.

**MSIMAMO LIGI KUU BARA**



| | P | W | D | L | F | A | PTS |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. Simba | 9 | 7 | 1 | 1 | 16 | 3 | 22 |
| 2. Kagera Sugar | 10 | 6 | 2 | 2 | 14 | 8 | 20 |
| 3. Lipuli | 10 | 5 | 3 | 2 | 18 | 10 | 18 |
| 4. Prisons | 10 | 3 | 7 | 0 | 11 | 7 | 16 |
| 5. Namungo | 10 | 5 | 1 | 4 | 9 | 8 | 16 |
| 6. JKT Tanzania | 10 | 4 | 3 | 3 | 8 | 8 | 15 |
| 7. Mtibwa Sugar | 11 | 4 | 3 | 4 | 10 | 11 | 15 |
| 8. Ruvu Shooting | 11 | 4 | 3 | 4 | 9 | 10 | 15 |
| 9. Alliance | 10 | 3 | 5 | 2 | 8 | 7 | 14 |
| 10. Mbao | 11 | 3 | 5 | 3 | 9 | 9 | 14 |
| 11. Azam | 7 | 4 | 1 | 2 | 7 | 4 | 13 |
| 12. Polisi TZ | 9 | 4 | 1 | 4 | 9 | 10 | 13 |
| 13. Coastal Union | 10 | 3 | 2 | 5 | 8 | 9 | 11 |
| 14. Mwadui | 11 | 2 | 5 | 4 | 7 | 10 | 11 |
| 15. Yanga | 5 | 3 | 1 | 1 | 6 | 4 | 10 |
| 16. KMC | 8 | 2 | 2 | 4 | 5 | 8 | 8 |
| 17. Biashara Utd | 10 | 2 | 2 | 6 | 6 | 11 | 8 |
| 18. Mbeya City | 10 | 1 | 5 | 4 | 7 | 16 | 8 |
| 19. Ndanda | 9 | 1 | 4 | 4 | 6 | 9 | 7 |
| 20. Singida Utd | 11 | 0 | 4 | 7 | 4 | 15 | 4 |

# Michezo

Alhamisi Novemba 14, 2019

Nipashe




Salah kuikosa Kenya leo kufuzu Afcon 2021 UKURASA 30


Distributed via ippmedia

Mchezaji wa Timu ya Taifa (Taifa Stars), Simon Msuva, akitoa darasa la soka kwa vitendo kwenye kliniki ya michezo ya watoto wa Shule ya Kimataifa ya Laurent jijini Dar es Salaam jana. Kliniki hiyo iliandaliwa na Taasisi ya Afrisoccer. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Ndayiragije, Samatta waishtukia E' Guinea

●●● Wasema dawa ni Taifa Stars kukimbiza mwanzo mwisho ili kuweza kuibuka na ushindi, lakini...

**Na Faustine Feliciane**

LICHA ya kukiri kutowafahamu vizuri wapinzani wao, Equatoria Guinea, Kocha Mkuu wa Taifa Stars, Etienne Ndayiragije pamoja na nahodha wa timu hiyo, Mbwana Samatta, wamesema wanapaswa kushuka dimbani katika mechi hiyo kwa tahadhari kubwa kutokana na wachezaji hao kulelewa katika mataifa yaliyosonga mbele kisoka barani Ulaya.

**Stars itaikaribisha Equatorial Guinea kesho katika Uwanja wa Taifa kwenye mechi ya kwanza ya hatua ya makundi kuwania kufuzu fainali za Mataifa ya Afrika nchini Cameroon 2021.**

Wakizungumza na gazeti hili jana wakati wa kliniki ya soka kwa watoto iliyofanyika Shule ya Kimataifa ya Laurent jijini Dar es Salaam, Ndayiragije yeye alisema wapinzani wao hao wana wachezaji wengi waliozaliwa nje ya nchi hiyo na kupata nafasi ya kukuzwa katika vituo vikubwa vya soka barani Ulaya.

Alisema hawategemei mchezo mwepesi na watahitaji kupambana muda wote wa mchezo ili kuweza kupata matokeo chanya.

"Ninachoshukuru wachezaji wangu wapo katika hali nzuri, kila mmoja ana morali kuelekea mchezo wetu, lakini lazima tuelewe kuwa wapinzani wetu nao wana timu nzuri na wachezaji wazuri, lakini pamoja na yote ni lazima tuutumie vema uwanja wetu wa nyumbani katika kampeni hizi za kufuzu tena Afcon," alisema kocha huyo raia wa Burundi, Ndayiragije.

Aidha, alisema kikubwa ni Watanzania kuiunga mkono timu yao na kuwasapoti wachezaji wao waweze kufanya vema kwenye mchezo huo utakaochezwa kesho kwenye Uwanja wa Taifa majira ya saa moja usiku.

Kwa upande wake, Samatta alisema kwa ujumla hawawafahamu vizuri wapinzani wao kisoka, lakini hakuna mchezo mwepesi ndani ya uwanja ila hawataki kufanya makosa ya kudondosha pointi kwenye uwanja wa nyumbani kama ilivyokuwa kwenye kampeni yao ya kufuzu fainali za mwaka huu ambapo Stars ilianza kwa kutoa sare dhidi ya Lesotho katika mechi iliyopigwa Uwanja wa Chamazi.

"Kwenye safari yetu, kufuzu fainali za mwaka huu tulianza na sare ya nyumbani dhidi ya Lesotho, sare ile ilitusumbua na kutupa kazi, lakini safari hii tunataka kuanza vema," alisema Samatta, ambaye ni nahodha katika klabu yake ya KRC Genk ya Ubelgiji.

Samatta, alisema kwao kama wachezaji kila kitu kinaenda sawa na wanafuatilia maelekezo ya makocha wao kuhakikisha wanapata ushindi kwenye mchezo huo wa kesho.

Kikosi cha Taifa Stars pamoja na benchi la ufundi jana kilikuwa sehemu ya mafunzo hayo ya soka kwa watoto wenye umri kuanzia miaka 5-16, huku wakishiriki kwa pamoja uwanjani.

Mafunzo hayo yaliandaliwa na kuendeshwa na Taasisi ya Afrisoccer ya jijini Dar es Salaam.

## Aussems afunguka Simba anayoitaka

**Na Somoe Ng'itu**

KOCHA Mkuu wa mabingwa watetezi, Simba, Mbelgiji Patrick Aussems, amesema ameamua kuwapa wachezaji wake mazoezi tofauti kwa sababu anataka warejee Ligi Kuu Tanzania Bara wakiwa na kasi mpya.

Akizungumza na gazeti hili jana, Aussems, alisema amekuwa akibadilisha programu za mazoezi kwa nyakati tofauti kutokana na kuhitaji kuona wachezaji wote wanakuwa imara na tayari kupambana kutetea ubingwa wanaoushikilia wa ligi hiyo.

Aussems (pichani chini) alisema pia mazoezi anayowapa yanawafanya wachezaji wote wanakuwa tayari kwa mchezo, hata kama wapo baadhi yao ambao hawajacheza mechi au wamecheza michezo isiyozidi mitatu.

"Tunajua ligi ni ngumu, kila timu inajipanga kufanya vizuri, kwa sasa kila upande hautaki kubaki nafasi za chini, ni ngumu kutumia wachezaji wale wale, na kila mechi ina mipango yake, tuko hapa kwa ajili ya kusaka matokeo mazuri na hili ndio lengo namba moja," Aussems alisema.

"Tunaongoza ligi, pia sisi ni mabingwa watetezi, ni jukumu letu kuhakikisha tunailinda heshima tuliyonayo, ni rahisi kuipoteza na ni ngumu kuifikia, lakini hakuna kisichowezekana kwenye soka."

Vinara hao wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba watashuka dimbani Novemba 24, mwaka huu, kucheza dhidi ya Ruvu Shooting kutoka Pwani ambayo katika mechi yake ya kwanza msimu huu iliwafunga watani wa 'Wekundu wa Msimbazi, hao, Yanga kwa bao 1-0.



GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >